DHIMA YA NYIMBO ZA BONGO FLEVA ZIHUSUZO RUSHWA KATIKA KULETA MABADILIKO KWA JAMII

Na

Edomu Secondina Sanga

Tasnifu hii imetolewa kwa ajili ya kukamilisha mahitaji ya shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2015

ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii inayoitwa **Dhima ya Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo Rushwa katika kuleta mabadiliko kwa Jamii** na anapendekeza kwamba inafaa kukubaliwa na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa tunzo ya shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili.

……

Profesa. Frowin Paul Nyoni

(MSIMAMIZI)

Tarehe…….

IKIRARI

NA

HAKI MILIKI

Mimi **Edomu Secondina Sanga** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia, na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

Saini……

© Hairuhusiwi kunakili wala kuzalisha kazi hii bila kibali cha muhusika au kibali toka Chuo Kikuu cha Dodoma.

SHUKRANI

Nianze kwa kumshukuru mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu aliyenipa nguvu, uhai, afya na uvumilivu hata nikaweza kuifanya kazi hii kwa kiwango kinachostahili.

Pili, nimshukuru kwa nafasi ya pekee Profesa. Frowin Paul Nyoni, huyu ndiye msimamizi wangu wa utafiti huu. Natambua majukumu mengi na mazito ya kikazi na ya kifamilia aliyonayo lakini alichukua na alitumia muda wake mwingi pia katika kuisoma na kutoa mchango wake ili kuleta ufanisi wa kazi hii, tangia tulipoianza katika hatua ya pendekezo la utafiti mpaka wakati wa uandishi wa tasnifu hii. Hakika mchango wake nina uthamini sana.

Tatu, nawashukuru pia walimu wangu, Profesa Joshua S. Madumulla, Profesa Lakshmanan, Dkt Elias M. Songoyi, Dkt Rafiki Y. Sebonde na Bw. Athuman Ponera ambao wamenifundisha katika Chuo Kikuu cha Dodoma na kunipa misingi thabiti ya Fasihi ya Kiswahili.

Nne, nichukue pia nafasi hii kumshukuru Mkuu wa Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pamoja na timu yake kwa ujumla kwa kutoa kibali cha kuruhusu kutumika kwa makavazi yanayopatikana katika Maktaba yao. Pia kutoa maelekezo yaliyo kuwa muhimu kwangu katika zoezi zima la ukamilishaji wa andiko hili.

Tano, shukrani zangu za dhati ziwaendee wale wote walionipa ushirikiano katika kipindi chote cha ukusanyaji wa data za utafiti huu, ni vigumu kuwataja mmoja mmoja kutokana na idadi yao kuwa kubwa lakini kwa uchache wao, namshukuru ndg, Kwame Elly Anangisye (katibu wa mbunge jimbo la Mbeya Mjini), Mkuu wa

shule ya sekondari Sinde- Mbeya, Mwl Eston A. Mbilinyi wa Sinde sekondari- Mbeya pamoja na wanafunzi wa kidato cha tatu shule ya sekondari Sinde- Mbeya. Namshukuru pia mkurugenzi wa Kiss Library iliyopo Mwanjelwa Mbeya. Lakini nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sikutumia nafasi hii kumshukuru Bw. Deogratias J. Kiswaga kwa msaada wake katika mambo ya kiufundi wa kielektroniki katika mchakato wa uandishi wa kazi hii.

Sita, nawashukuru pia ndugu na jamaa ambao kwa namna moja ama nyingine wamekuwa msaada kwangu katika hatua mbalimbali za uandishi wa kazi hii tangu hatua ya mwanzo ya kuandika mada ya utafiti mpaka hatua ya mwisho ya uandishi wa tasnifu hii.

Saba, namshukuru kwa nafasi ya pekee mama yangu mzazi, Bi S.B.Sanga kwa kunizaa na kunilea katika hatua mbalimbali za makuzi ya binadamu. Hakika anastahili sifa, kwani yeye ndiye dira ya maisha yangu.

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa familia yangu Mke wangu kipenzi Leah S. Msigala, wanangu Samuel E. Sanga na Maureen E. Sanga, ndugu na jamaa kwa jumla kwani maombi na ushauri wao vimenisaidia hata nimeweza kukamilisha kazi hii.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga katika kuchunguza **Dhima ya Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo Rushwa katika kuleta Mabadiliko kwa Jamii**. Bongo Fleva ni nyimbo za kizazi kipya nchini Tanzania. Nyimbo hizi huwa na dhamira mbalimbali ambazo hulenga kuelimisha na kuburudisha jamii inayokusudiwa na msanii. Njia ya nyimbo huwa bora zaidi kwani huwafikia sehemu kubwa ya jamii. Kutokana na umuhimu wa nyimbo jamii hupata mwitikio na kuifanya jamii kupata mabadiliko na kuifanya jamii mpya yenye maadili mema. Nyimbo mara nyingi husadifu mazingira ya jamii anapoimbia msanii na zinalenga vyema katika kutambulisha utamaduni wetu kwa kuyaweka mambo yetu.

Utafiti huu uliongozwa na malengo ya aina mbili ambayo ni lengo la jumla la utafiti ambalo lilikuwa kuchunguza dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii. Pia malengo mahususi matatu, Kwanza kukusanya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa na wasanii mbalimbali katika Jamii, Pili kuchunguza na kuainisha dhima zinazopatikana katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa, na Tatu kuchunguza mwitikio wa jamii kuhusiana na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

Utafiti huu katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa tulizozisikiliza na kuzitumia kama kifani chetu tulibaini dhima mbalimbali kama vile kuelimisha, kuarifu, kukemea, kuadili, kuonya, ukombozi, kudhihaki uoga, kutia hamasa, kupitisha amali za jamii na kutumika kama rekodi ya matukio muhimu katika jamii.

Utafiti huu ulifanyika maktabani na uwandani, maeneo mbalimbali ya halmashauri ya jiji la Mbeya yalitumika katika kukusanya data. Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zilikusanywa na kuwekwa katika maandishi, kisha kuchambuliwa na kupata

dhima zinazopatikana katika nyimbo kwa mabadiliko ya jamii. Mwitikio wa jamii kuhusiana na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa na mwisho mabadiliko yaliyopatikana kutokana na nyimbo.

Uchambuzi wa data umefanywa kwa kutumia mkabala wa U-marx, Matokeo yanaonesha U-marx unajikita katika kuleta mabadiliko kwa kujua historia ya jambo na kuelewa tatizo kisha kuliunda upya kwa namna bora zaidi tofauti na awali. Pia nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zimewekwa katika maandishi.

YALIYOMO

ITHIBATI YA MSIMAMIZI i
IKIRARI NA HAKI MILIKI iii
SHUKRANI iv
TABARUKU vi
IKISIRI vii
YALIYOMO ix
ORODHA YA PICHA xiii
VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIKA xiv
MAANA YA ISTILAHI MBALIMBALI ZA UTAFITI xvi

SURA YA KWANZA : UTANGULIZI 1
1.1 Utangulizi 1
1.1.1 Sifa za Bongo Fleva 1
1.1.2 Matawi ya Bongo Fleva 2
1.1.3 Faida za Bongo Fleva 3
1.2 Usuli wa Tatizo 5
1.3 Tamko la Utafiti 8
1.4 Malengo ya Utafiti 8
1.4.1 Lengo la Jumla 8
1.4.2 Malengo Mahsusi 8
1.7 Nadharia ya Utafiti 9
1.8 Upeo wa Utafiti 11
1.9 Hitimisho 12

SURA YA PILI :MAPITIO YA KAZI MBALIMBALI 13
2.1 Utangulizi 13
2.2 Maandiko Mbalimbali kuhusu Fasihi Simulizi 13
2.3 Maandiko Yanayohusu Fasihi na Dhima zake katika Jamii 15

2.4 Maandiko mbalimbali yanayohusu Nyimbo na Dhima zake kwenye Jamii 17

2.5 Maandiko Kuhusu Nyimbo za Bongo Fleva na Dhima zake kwa Jamii..... 23

2.6 Pengo la Utafiti 25

SURA YA TATU :MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI 26

3.1 Utangulizi..... 26

3.2 Utaratibu wa Utafiti..... 26

3.3 Eneo la Utafiti 26

3.4 Walengwa wa Utafiti..... 27

3.4.1 Jamii ya Watafitiwa..... 27

3.4.2 Sampuli na Usampulishaji..... 27

3.4.2.1 Sampuli Lengwa..... 28

3.4.2.2 Sampuli Holela..... 28

3.4.2.2.1 Sampuli ya Wanafunzi 28

3.4.2.2.2 Sampuli ya Vijana..... 28

3.4.2.2.3 Sampuli ya wazee..... 29

3.5 Ukusanyaji wa Data 29

3.5.1 Zana za Kukusanyia Data..... 29

3.5.1.1 Redio na Kinyonyeo (*Flash*)..... 30

3.5.1.2 Maswali ya Usaili (Hojaji)..... 30

3.5.1.3. Daftari na Kalamu..... 31

3.5.1.4 Kamera na Kinasa Sauti..... 31

3.5.1.5 Simu ya Mkononi..... 31

3.5.1.6 Ngamizi (*Computer*) 31

3.5.2 Mbinu zilizotumika katika Ukusanyaji wa Data..... 31

3.5.2.1 Udurusu wa Nyaraka..... 32

3.5.2.2 Mahojiano 32

3.6 Mchakato wa Ukusanyaji na Udhibiti wa Data 33
3.7 Uchakataji wa Data 33
3.8 Vikwazo vya Utafiti 34

SURA YA NNE: MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI 35
4.1 Utangulizi 35
4.2 Nyimbo za Bongo Fleva Zihusuzo Rushwa 35
4.3 Dhima ya Nyimbo za Bongo Fleva Zihusuzo Rushwa kwa Mabadiliko ya Jamii 38
4.3.1 Kuelimisha 40
4.3.2 Kuonya 43
4.3.3 Kuadili 46
4.3.4 Kukemea 50
4.3.5 Kuarifu 53
4.3.6 Kuburudisha 56
4.3.7 Kutia hamasa 57
4.3.8 Kupitisha Thamani za Jamii 60
4.3.9 Ukombozi 61
4.3.10 Kudhihaki Uoga 65
4.3.11 Kutumika kama rekodi ya matukio muhimu ya kihistoria 69
4.4 Lugha 70
4.4.1 Lugha fiche 70
4.4.2 Lugha wazi 73
4.4.3 Kuchanganya lugha 74
4.5 Mwitikio wa Jamii kuhusu Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo Rushwa 75
4.6 Mabadiliko ambayo Jamii inayapata kutokana na Kusikiliza Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo Rushwa 77

SURA YA TANO : HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 81
5.1 Utangulizi 81
5.2 Muhtasari wa Tasnifu 81
5.3 Utoshelevu wa Mkabala tulioutumia 82
5.4 Mchango Mpya wa Utafiti huu 83
5.5 Maoni na mapendekezo 83
5.5.1 Maoni na Mapendekezo Kutokana na Utafiti huu 83
5.5.1.1 Kuhusu Kuienzi Fasihi 83
5.5.1.2 Kuhusu Mtazamo Hasi juu ya Bongo Fleva 84
5.5.2 Mapendekezo ya Mtafiti 85
MAREJELEO 88
VIAMBATISHO 90
A: HOJAJI KWA WASIKILIZAJI WA BONGO FLEVA KATIKA JAMII.. 90
B: NYIMBO ZA BONGO FLEVA ZIHUSUZO RUSHWA. 91

ORODHA YA PICHA

Picha 1: Baadhi ya zana zilizotumika katika kufanikisha mchakato mzima wa uandishi wa utafiti huu. (Chanzo: Utafiti, 2013) 29

Picha 2: Mtafiti akiwa katika moja ya maktaba za muziki zilizopo katika maeneo ya Mwanjelwa Jijini Mbeya (Chanzo: Utafiti, 2013). 36

Picha 3: Baadhi ya wanafunzi walioshiriki mjadala kuhusu nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Wanafunzi hawa ni kutoka shule ya sekondari Sinde iliyopo katika halmashauri ya Jiji la Mbeya (Chanzo: Utafiti, 2013)..... 39

VIFUPISHO VYA MANENO YALIYOTUMIKA

R&B	*Rhythm and Blues*
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TAMWA	*Tanzania Media Women's Association*
MC	*Master of Ceremony*
DKT	Daktari
EPA	*External Payment Arreas*
FT	*Featuring*
TBS	*Tanzania Bureau of Standards*
RPC	*Region Police Commander*
CHADEMA	Chama cha Demokrasia na Maendeleo
TAKUKURU	Tasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa
DJ	*Disco Joker*
BOT	*Bank of Tanzania*
NECTA	*National Examination Council of Tanzania*
CD4	*Cluster of Differentiation 4*
UDSM	*University of Dar Es Salaam*
TV	*Television*
MV	*Moving Vessel*
UKIMWI	Ukosefu wa Kinga Mwilini
JK	Jakaya Kikwete
HIV	*Human Immune Virus*
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
TAZARA	*Tanzania and Zambia Railway*
CCP	Chuo Cha Polisi

THT	*Tanzania House of Talents*
NMB	*National Microfinance Bank*
PCM	*Physics Chemistry Mathematics*
PCB	*Physics Chemistry Biology*
TCU	*Tanzania Commission of Universities*
ATM	*Automatic Teller Machines*
CCM	Chama Cha Mapinduzi
CUF	*Civil United Front*
TFF	*Tanzania Football Federation*
TMK	Temeke
Y2K	*Y up to K*
TOT	*Tanzania One Theatre*
KKT	Kanisa la Kilutheri Tanzania
TVT	Televisheni ya Taifa
TPC	*Tanzania Police Commander*
KCMC	Kilimanjaro Christian Medical Centre
TRA	*Tanzania Revenue Authority*
TIA	*Tanzania Institute of Accountancy*
DNA	*Deoxyribonucleic Acid*
ICU	*Intensive Care Unit*
CD	*Compact Disc*
COSOTA	*Copyright Society of Tanzania*

MAANA YA ISTILAHI MBALIMBALI ZA UTAFITI

Wimbo

Wimbo ni kila kinachoimbwa. Hivyo hii ni dhana pana inayojumuisha tanzu nyingi. Hata baadhi ya tanzu za kinathari, kama vile hadithi, huweza kuingia katika kundi la nyimbo pindi zinapoimbwa. Mambo muhimu yanayotambulisha nyimbo ni pamoja na muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji, muziki wa ala; matini au maneno yanayoimbwa, hadhira inayoimbiwa; muktadha unaofungamana na wimbo huo, kwa mfano sherehe, ibada, kilio na yanayofanana na hayo (Mulokozi, 1996:64).

Bongo Fleva

Kietimolojia, Bongo Fleva ni neno linalotokana na muunganiko wa maneno mawili ya lugha mbili tofauti, kuna neno la Kiswahili 'Bongo' na kuna neno lugha ya Kingereza 'Flavor'. Bongo maana yake ni akili na Flavor, ambalo katika Kiswahili limetoholewa matamshi yake na kuwa Fleva, hufasiliwa kama ladha. Kwa hiyo, fasili ya kwanza ya muziki wa Bongo Fleva ni ladha zitokanazo na matumizi ya akili. Hata hivyo hii ni fasili finyu ya Bongo Fleva, fasili pana na inayofaa ni ile ya kisitiari. Katika mtazamo huu, Bongo hurejelea jiji la Dar es Salaam au Tanzania kwa ujumla. Istilahi hii ilizuka tu kama sehemu ya utashi wa matumizi ya lugha ya Kiswahili, hasa kutokana na kuongezeka kwa hali ngumu katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam, ambapo ili mtu aweze kujikimu anahitaji kutumia akili na maarifa mengi zaidi kuliko ambavyo angetumia akiwa pembezoni mwa miji hiyo mikubwa (Kadallah 2010). Kwa hiyo, Bongo Fleva ni aina ya muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania unaojumuisha aina mbalimbali za nyimbo zenye vionjo vya Kimagharibi na Kiafrika, aghalabu, muziki huu hurekodiwa kingamizi na vifaa mbalimbali vya kielektroniki

Dhima

Dhima ni wajibu pamoja na uwezo wa kufanya jambo; madaraka, wadhifa. (TUKI, 2004:63)

Dhima ya Nyimbo kama sehemu ya fasihi hufafanuliwa kwa njia mbalimbali na wahakiki mbalimbali. Msikilizaji au msomaji wa kazi ya fasihi huweza kupata funzo tokana na kazi hiyo kama ile ya kuelimisha, kuonya, kukemea, kuarifu, kutia hamasa, kuadili, kudhihaki uoga, ukombozi wa kifikra, kupitisha amali za jamii, kutumika kama rekodi ya matukio muhimu ya kihistoria n.k

Rushwa

Rushwa ni fedha au kitu cha thamani kinachotolewa na kupewa mtu mwenye madaraka au mamlaka ya jambo fulani ili mtoaji apatiwe upendeleo; kwa maneno mengine rushwa huitwa chai, chauchau, chirimiri, kiinikizo, kilemba, chichiri, hongo, mrungura, kadhongo, mvugulio, mlungula (TUKI, 2004:353). Rushwa inaeleweka kama aina yoyote ya matumizi mabaya ya madaraka kwa ajili ya mtu binafsi au kikundi cha watu ambao wanaweza kuwa wa sekta binafsi au sekta ya umma. Rushwa huweza kuwa katika namna nyingi kama vile rushwa ya vitu, fedha au ngono. Rushwa huwa ni kitendo cha pande mbili yaani mtoa rushwa kwa upande mmoja na mpokea rushwa kwa upande mwingine.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu “dhima ya nyimbo kwa mabadiliko ya jamii” mifano kutoka nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Sura hii imegawanywa katika sehemu nane, sehemu ya kwanza inaeleza utangulizi wa sura hii, sehemu ya pili usuli wa tatizo la utafiti, sehemu ya tatu inaeleza malengo ya utafiti, sehemu ya nne inaeleza juu ya maswali ya utafiti, sehemu ya tano inaeleza umuhimu wa utafiti, sehemu ya sita inaeleza mawanda ya utafiti, sehemu ya saba inaeleza nadharia ya utafiti, sehemu ya nane inahusu upeo wa utafiti na mwisho sura ya tisa ni hitimisho.

1.1.1 Sifa za Bongo Fleva

Nyimbo za Bongo Fleva kama muziki umeshika kasi sana nchini Tanzania katika miaka ya 1990 hadi sasa. Fasihi hii hupendwa sana na vijana na ambao huitumia katika kuelezea matatizo yao. Utanzu huu kama muziki unazo sifa zinazo ubainisha, nazo pia zimeainishwa na Majembe (1998), Chachage (2002) na Omari (2008, 2009). Sifa hizo ni pamoja na;

Mosi, matumizi ya lugha ya mseto hasa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza, au Kiswahili na lugha nyingine ya kitamaduni yaani lugha ya kikabila. Hii hufanyika ili kuleta ujumi wa kisanaa, kufikisha ujumbe uliyo kusudiwa na msanii na vilevile kutambua nafasi ya lugha nyingine katika mawasiliano.

Pili, kuimba kunakoenda sambamba na matendo ya mwili, yaani matumizi ya viungo vya mwili katika utendaji wake, katika hili waimbaji na wachezaji huzitumia sehemu

za miili yao kwa kuzizungusha katika kucheza, mathalani, kuzungusha mikono, mabega, kichwa, na kiuno.

Tatu, kuchanganya tamaduni katika vipengele vya uvaaji na mwonekano ambapo wasanii wa kiume huvalia mashati au fulana kubwa, viatu vikubwa na suruali zinazobana, kusuka nywele na kuvaa hereni. Wakati kwa wasanii wa kike huvalia nguo zinazowabana na fupi na pengine kuacha baadhi ya sehemu za miili yao wazi, kama vile mapaja, tumbo, na mgongo.

Nne, ni matumizi ya majigambo. Wasanii kupenda kujisifia wao kupendwa na wanawake wengi na hata mashabiki, kuwa na kipaji cha hali ya juu cha kuimba na kuwavutia mashabiki wao kwa kiwango kikubwa.

1.1.2 Matawi ya Bongo Fleva

Jina kuu la nyimbo za Bongo Fleva kama muziki nchini Tanzania, ni muziki wa kizazi kipya. Muziki huu unatalii nyanja zote za kimaisha kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni japo katika viwango na msisitizo usiolingana.

Aina za nyimbo zinazojitokeza katika muziki wa Bongo Fleva ni nyimbo za kufokafoka, nyimbo za taratibu (R&B), zuku (*zouk*), charanga, nyimbo za kihindi, rumba, raga, ngoma za asili, taarabu, na nyimbo za kikongo (Bolingo). Katika mazingira ya kawaida, Bongo Fleva inajitambulisha kama muziki wa vijana au kizazi kipya ukijitofautisha na aina nyingine za muziki wa dansi.

Aina mbalimbali za muziki unaoimbwa na vijana na kutiwa vionjo kadhaa umekuwa ukiitwa Bongo Fleva hata kama nyimbo zinazoimbwa ziliimbwa na muziki wa dansi, taarabu, rege, rumba, au ngoma za asili. Kutokana na nyimbo za Bongo Fleva kuwa na utaratibu wa kuzingatia uchezaji, melodi, na midundo ya muziki fulani. Mnenuka

(2010) anapendekeza uainishaji wa nyimbo hizo kama ifuatavyo; fokafoka, tongozi, mchaziki, mchangageni, mchangasili, mchangadini, na mchangalela.

Akifafanua mgawanyo huo anaeleza kuwa, Bongo Fleva ni mwamvuli wenye tanzu na vipera au kumbo na tanzu kadha wa kadha. Kufokafoka ni muziki ambao vyombo vinapigwa huku msanii akizungumza na kuimba kwa kufuata ridhimu fulani. Tongozi ni muziki ambao umeibuka hivi karibuni ambapo mwimbaji hutongoa au hughani mashairi aliyotunga au aliyotungiwa ambapo kuna mapumziko yanayojazwa na kiitikio kinachoimbwa. Mara nyingi kiitikio hubeba wazo kuu linalojadiliwa katika muziki. Mchaziki ni mchanganyiko wa vionjo vya Bongo Fleva na aina nyingine za muziki unaopigwa hapa Tanzania kama vile dansi, taarabu, mduara na aina nyingine za muziki kadiri itakavyoendelea kujitokeza. Mchangageni ni mchanganyiko wa melodi na ridhimu za kigeni zinazoimbwa kwa lugha ya Kiswahili, lugha za kigeni, mchanganyiko wa lugha, au lugha za jamii mojawapo ya Tanzania. Mchangasili ni mchanganyiko wa mahadhi ya ngoma za asili za Tanzania. Mchangadini ni aina ya muziki wa Bongo Fleva ambao huchanganya melodi na ridhimu za kidini hasa dini za kigeni. Mchangalela ni mchanganyiko holela ambao unakusanya vionjo mbalimbali.

1.1.3 Faida za Bongo Fleva

Ni dhahiri kuwa Bongo Fleva kama muziki kwa sasa umuhimu wake umekuwa wa kiwango cha juu kwa wasanii wenyewe, watengenezaji, wasambazaji, wamachinga, wazazi, na jamii kwa ujumla. Bongo Fleva kama muziki unatazamwa kama chombo muhimu cha kujikomboa kiuchumi na kisiasa miongoni mwa wasanii wake na jamii kwa ujumla.

Muziki wa Bongo Fleva umekuwa miongoni mwa vyombo muhimu vya kutolea elimu kwa jamii kama vile masuala ya afya, elimu, uchumi, utamaduni na siasa. Pia, umeleta maendeleo endelevu kwa vijana, kwani wengi wanajishughulisha na muziki huu ni wale ambao hawana elimu ya juu lakini wameweza kumudu na kujiendeleza kimaisha kutokana na kufanya muziki huu. Hivyo, wale wote wanaojishughulisha na sanaa hii wamefanikiwa kujikwamua kutokana na tatizo la ajira ambalo linawakumba vijana wengi, baadhi yao wameweza kujenga nyumba, kununua magari na kufungua studio zao za kurekodia muziki. Hali hii imewafanya wasanii kujiendeleza kimaisha na kielimu, na hivyo kujikomboa kiuchumi. Ubunifu na utunzi mzuri wa baadhi ya nyimbo zao huwafanya watu kununua nyimbo hizo na kuhudhuria matamasha yao na kuwaletea maendeleo ya kimuziki na kiuchumi.

Rushwa ni tatizo linalosumbua na kwa hali hiyo lina madhara mengi kutokana na kuwepo kwake katika jamii, Mojawapo ya athari zake ni pamoja na kutokuwepo kwa haki kwa watu wanaohitaji huduma mbalimbali kutoka kwa wale wenye dhamana ya kuwatumikia wananchi katika sekta binafsi au sekta za umma. Pia, kuwepo kwa rushwa katika jamii kunasababisha kutokuwepo kwa ufanisi wa majukumu kadha wakadha kwenye sekta binafsi na sekta za umma kwani wale wote wanaoweza kupata nafasi ni wenye uwezo wa kutoa rushwa na wale wasio weza kutoa rushwa hawatapata nafasi. Kutokana na huduma kupatikana kwa kuangalia uwezo wa kifedha ulionao, basi nafasi ya uwezo wa kiutendaji haipewi kipaumbele. Hii husababisha kuwakosa watu wenye uwezo mzuri wa kiutendaji na kusababisha kutokuwepo kwa ufanisi. Vilevile kuwepo kwa rushwa katika jamii kunasababisha kutokuwepo kwa maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni.

Rushwa ni changamoto katika jitihada za taifa kujiletea ustawi kwenye nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Hata hivyo kumekuwepo jitihada za makusudi za kupambana na kuzuia rushwa zinazofanywa na taasisi za serikali, mashirika binafsi na watu binafsi. Katika harakati za vita dhidi ya rushwa, mbinu anuai za uelimishaji juu ya madhara ya rushwa kwa ustawi na maendeleo ya taifa zinahitajika. Kupambana na kuzuia rushwa ni kitendo kinachohitaji ushiriki wa dhati wa wananchi. Njia mbalimbali zinaweza kutumika kukidhi haja hiyo mathalani, kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili waweze kutambua haki zao. Elimu ambayo huweza kutolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo ya nyimbo kupitia redio na katika matamasha ya wazi, vipeperushi, mabango, kauli mbiu. Njia nyingine ni kuingiza somo la rushwa katika mtaala, somo la rushwa na madhara yake lifundishwe kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu kwa hali hiyo walimu na wanafunzi wataanza kuelewa madhara ya rushwa tangu awali. Vilevile, njia ya kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza umasikini kote nchini. Umasikini na ufinyu wa kipato unasababisha watu kushawishika kutoa au kupokea rushwa.

1.2 Usuli wa Tatizo

Nyimbo ni kipera adhimu sana katika kazi mbalimbali za fasihi simulizi, aghalabu huweza kutumika katika vipera na tanzu nyingine za fasihi simulizi na andishi. Mathalani, huweza kutumika katika hadithi, semi, sanaa za maonyesho na mashairi katika kuwasilisha maudhui lengwa, hali hii hutokana na uwezo wake mkubwa katika kuvuta fikra za jamii kupokea maudhui lengwa yabebwayo na kazi yoyote ya fasihi. Aidha, hali hii hufanya jamii kuamini kwamba nyimbo zina uwezo wa kuleta mabadiliko kwenye jamii kwa sababu, kwa kawaida, husheheni mawazo mazito yenye kubainisha mahusiano na migogoro ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Kupitia nyimbo, jamii hubadilika, huburudika, hujifunza, huongolewa,

huomboleza na kupitisha amali zake na historia. Aidha, nyimbo huwa na uteule wake wa majukumu kwani hupitisha, hueleza, na huathiri hisia za ndani za watu. Mabadiliko hayo hutarajiwa kutokana na athari za nyimbo kwa binadamu, ambayo pia hutegemeana na dhima ya nyimbo kusudiwa na mtunzi wake kuwafikia hadhira ili wapate mabadiliko fulani. Kwa mfano, mtunzi huweza kutunga nyimbo za watoto ambazo huimbiwa ili washawishike kihisia kufanya jambo fulani, za sifa ambazo hutumiwa kusifu kitu au mtu katika jamii, za nyiso hizi huimbwa katika tohara. Pia, nyimbo za kazi huimbwa wakati wa kazi, za siasa hizi huchochea ari na kuimarisha jamii kisiasa, zamatanga ambazo huimbwa wakati wa kuomboleza kifo cha mtu katika jamii husika, Nkwera (1978), Simiyu (2011).

Kezilahabi (1981:119) anatuambia kuwa, nyimbo ni kipera cha Fasihi Simulizi ambacho kina historia ndefu. Nyimbo zimekuwa njia inayofaa kutolea mafunzo na maadili mbalimbali kwa wanajamii tangu zamani, kwa mfano nyimbo zilitumika katika mafunzo ya kijeshi, mafunzo ya kazi, dini, vita, shule, mikutano, kuliwaza wafiwa, hata kutukuza. Hivyo, maelezo ya Kezilahabi yanatubainishia kuwa nyimbo zimekuwa zikitumika kama utanzu muhimu katika nyanja za kijamii tangu zamani na hadhi yake imeendelea kuwa na athari katika mabadiliko ya jamii mpaka sasa.

Bongo Fleva ni nyimbo zinazojadili matatizo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yanayoikabili jamii. Ni nyimbo ambazo aghalabu hutoa ujumbe unaoelezea ukweli unaojitokeza katika jamii moja kwa moja na kwa uwazi, pia hutumika kama burudani kwa wanajamii. Nyimbo hizi huelezea matatizo ambayo hayajadiliki kwa urahisi katika jamii kupitia namna nyingine. Nyimbo za Bongo Fleva hupendwa na makundi mbalimbali ya watu katika jamii kama vile vijana,

wazee na hata watoto na ambao huzitumia kusikiliza na kuelewa matatizo yaliyomo katika jamii na ambayo yanajadiliwa na wasanii tofauti tofauti.

Msanii wa Bongo Fleva huweza kutalii na kujadili mambo mengi katika wimbo mmoja kwa wakati mmoja. Mambo hayo hujumuisha dhamira nyingi zilizobeba ujumbe tofautitofauti wenye lengo la kuelimisha jamii kutokana athari zinazoweza ikumba. Sanaa hii inayoimbwa na wasanii wengi wao ni vijana nchini Tanzania. Nyimbo hizi husikilizwa na makundi mbalimbali ya watu wa marika mbalimbali kama vile vijana, wazee na watoto. Makundi haya husikiliza ili kujifunza vilevile kama burudani.

Utanzu huu unakuwa na dhamira nyingi zenye malengo ya kuelimisha, kuonya, kuburudisha, kuadili, kuarifu, kuomboleza, kubembeleza, kutia hamasa, kuchapuza kazi, kupitisha thamani za jamii, hutumika kama rekodi za matukio ya kihistoria, ukombozi. Hivyo jamii hubadilika kupitia mafunzo yaliyomo katika nyimbo hizo.

Nyimbo za Bongo Fleva zimekuwa sehemu ya suluhisho la ajira kwa jamii kwani zimetoa ajira kwa makundi mbalimbali ya watu, kama watunzi, waimbaji, maprodyuza, wasambazaji, wauzaji kama machinga, wachezaji (stage shows) na hii imeipunguzia sana Serikali tatizo la ajira kwa kuwa hawa hujiajiri. Lakini pia nyimbo za Bongo Fleva zinasaidia katika kuelimisha na kuiburudisha jamii kwa ujumla kutokana na maudhui yaliyomo katika nyimbo hizo.

Pamoja na tafiti za akina Nkwera (1978), Kezilahabi (1981), Mulokozi (1996), Mdee (2009) na Simiyu (2011) kujadili utanzu wa nyimbo na dhima zake kwa jamii, katika kazi zao hawajagusia wala kujadili nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika kuleta mabadiliko kwa jamii. Hali hii ndiyo ilimsukuma mtafiti kuchunguza “dhima

ya nyimbo kwa mabadiliko ya jamii" kwa mifano kutoka nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

1.3 Tamko la Utafiti

Watafiti wengi, kwa mfano; Msuya na Lupokela (2011), Mnenuka (2010), Samwel (2010), wamechunguza kipera cha nyimbo za Bongo Fleva kwa kuangalia namna zinavyoweza kuwa na mabadiliko ya tabia kwa kuelezea ufaafu wake kwenye maadili na malezi. Haya yote yametokana na tafiti zilizobainisha kuwa nyimbo ni sehemu ya maisha ya binadamu na hushughulika na jamii katika nyanja za kiutamaduni, kiuchumi, na kisiasa, zikimsaidia binadamu katika kutatua matatizo yanayomkabili. Pamoja na wataalamu kuchambua mambo mbalimbali katika maandiko yao, suala la nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii halijashughulikiwa kwa kiwango cha kutosha. Hilo lilimsukuma mtafiti kuchunguza dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii.

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu unaongozwa na malengo ya aina mbili ambayo ni lengo la jumla la utafiti na malengo mahsusi ya utafiti kama ifuatavyo.

1.4.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii.

1.4.2 Malengo Mahsusi

(a) Kukusanya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa na wasanii mbalimbali katika jamii.

(b) Kuchunguza dhima zinazopatikana katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

(c) Kuchunguza mwitikio wa jamii kuhusiana na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

Maswali ya Utafiti

a) Je ni nyimbo zipi za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa katika jamii?

b) Je kuna dhima zipi zinazopatikana katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa?

c) Je jamii ina mwitikio gani kuhusiana na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa?

Manufaa ya Utafiti

a) Kusaidia kuamsha ari kwa wanajamii katika kupambana na kutokomeza rushwa nchini.

b) Kusaidia kutoa hamasa kwa wadau mbalimbali na wataalam wengine kufanya tafiti juu ya jambo hili kwa namna nyingine ili kuziba mapengo yaliyoachwa wazi.

c) Kusaidia jamii kuzijua nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

1.7 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya U-Marx katika uchambuzi wa taarifa. Nadharia hii iliasisiwa na mwanafalsafa wa Kijerumani Karl-Heinirich Marx, ambaye alizaliwa 05.05.1818, alifariki 14.03.1883. Karl Marx alikuwa msomi wa

siasa, uchumi na mwanamapinduzi aliyejulikana kama mwasisi wa ukomunisti. U-Marx unaiona jamii kuwa muungano wa miundo miwili inayohusiana na kutegemeana. Miundo hiyo ni muundo-msingi ambao unajumuisha michakato ya uhusiano wa kiuzalishaji mali pamoja na njia za uzalishaji. Kwa mujibu wa Karl Marx, katika uhusiano wa kiuzalishaji mali, mabepari huwanyonya wafanyakazi kwa kuwa humiliki njia za uzalishaji mali. Huu ni muundo wa kiuchumi unaozaa muundo wa juu wa utawala unaojumuisha siasa, itikadi, sheria, elimu, vyombo vya habari na dini. Muundo huu ndiyo unaoakisi, kulinda, na kuratibu muundo-msingi. Umarx ni falsafa yakinifu inayoangalia ulimwengu na vilivyomo kama vitu halisi na kwamba binadamu ndiyo chanzo cha mabadiliko. Aidha, U-marx unaamini kuwa mabadiliko hayafanyiki kwa urahisi, yanapaswa yafanywe hatua kwa hatua. Uyakinifu wa U-marx unajidhihirisha pia kihistoria, kuwa mabadiliko katika mfumo wa jamii hutokea wakati jamii inapofikia hatua fulani ya maendeleo inayoibua mgongano katika muundo-msingi na muundo wa juu wa utawala. Migongano hiyo huibuka kutokana na mahusiano ya kinyonyaji kati ya mabepari na wafanyakazi wao. Mabadiliko haya hutokea kwenye muundo-msingi.

Hata hivyo, kuna mwingiliano na kurithiana kwa miundo hii. Baadhi ya misingi ya U-marx ni mapambano ya kitabaka yanayosababishwa na uhusiano wa kinyonyaji kati ya wamiliki wa njia kuu za uzalishaji mali na wafanyakazi. Ulazima wa kufanya mapinduzi yanayowanyang'anya wanyonyaji nyenzo za uchumi na kuzikabidhi kwa matabaka ya wazalishaji. Mapinduzi ya kisoshalisti yanayoweka njia kuu za uzalishaji mali mikononi mwa umma.

Hivyo, utafiti huu ulitumia nadharia ya U-marx kwa kuwa hutathimini maendeleo ya historia ya binadamu pamoja na asasi zake kiuchumi, kisiasa, na kijamii na kwamba

dini, fikra na utamaduni wa jumuiya yoyote huwa ni itikadi na miundo maalum ya kitabaka ambayo ni zao la miundo na matabaka ya kijamii yaliyomo kwa wakati huo.

Msingi mkuu wa nadharia ya U-marx ni kwamba fasihi hueleweka katika misingi ya uhalisi wa kijamii hasa katika umilikaji mali. U-marx huchukulia fasihi kama umbo maalumu ambalo hupatikana katika historia, umbo hilo pia hupatikana katika hali yoyote ya jamii kwa sababu ya mahusiano maalumu ya kitabaka, kiutamaduni, kisiasa na kijamii hubebana na msingi uliopo. Mbinu kubwa ya U-marx ni kuchunguza jadi na kuunda upya mtazamo kuhusu yaliyopita kutokana na ithibati za kihistoria, kisha kudhihirisha uhalisi wa kazi fulani kama kielelezo cha jamii kwa njia ya kuelewa uhalisia.

Utafiti ulitumia misingi ya nadharia na mbinu ya U-marx kwa sababu utafiti huu umeangalia suala la rushwa na jinsi linavyounda utabaka kati ya mtoa rushwa anayeonekana ndiye mnyonge na mpokea rushwa anayeonekana ndiye mwenye nguvu. Kwahiyo nadharia hii ilitoa uwanda mpana wa kuitumia katika utafiti huu.

1.8 Upeo wa Utafiti

Utafiti ulishughulikia utanzu wa Fasihi simulizi katika kipera cha nyimbo, hususani nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Tulitumia nyimbo ishirini na sita (26) toka kwa wasanii Roma Mkatoliki, Feruzi Mrisho, Solo Thang, Nakaya Sumari, MwanaFA, Bonta, Profesa J, Mapacha, Weusi, Izzo B, Wagosi wa Kaya, Lady JD, Afande Sele, Kala Jeremiah, Sugu, Ommy Dimpos, Snura, Vitalis Maembe na Young D.

1.9 Hitimisho

Sura hii imetoa mwanga kwa kiasi kuhusu nyimbo za Bongo Fleva, ikieleza maana, sifa, matawi na faida zake. Pia rushwa imejadiliwa yakielezwa madhara yatokanayo, na namna ya kupambana na kuzuia rushwa. Vingine vinavyojitokeza katika sura hii ni usuli, malengo, manufaa, upeo, na mkabala uliotumika katika uchambuzi data za utafiti huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI MBALIMBALI

2.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza baadhi ya kazi mbalimbali zinazohusiana na mada yetu ya utafiti. Upitiaji wa kazi mbalimbali za watafiti hujumuisha usomaji wa kina wa vitabu, majarida, tasnifu za watafiti wengine kwa madhumuni ya kuchunguza jinsi watafiti hao walivyojadili juu ya nyimbo na dhima zake kwa jamii. Mapitio ya kazi mbalimbali humpa mwelekeo mtafiti kwa kumwonesha kama kuna pengo linalohitajika kuzibwa kutoka kwenye tafiti zilizotangulia. Upitiaji wa kazi mbalimbali za waandishi huambatana na uhakiki, uchambuzi na utoaji wa maoni juu ya kile ambacho mtafiti amebainisha ili kutumia mawazo yake kuboresha utafiti unaoshughulikiwa.

Kwa hivyo sura hii inaelezea wataalamu mbalimbali ambao wamejadili fasihi na nyimbo katika vitabu, majarida, makala na tasnifu mbalimbali. Sura hili imegawanyika katika sehemu tatu, sehemu ya kwanza inahusu maandiko yanayohusu fasihi kwa ujumla. Sehemu ya pili ni maandiko yanayohusu nyimbo na dhima zake kwenye jamii. Sehemu ya tatu ni maandiko yanayohusu nyimbo za Bongo Fleva na mabadiliko ya jamii.

2.2 Maandiko Mbalimbali kuhusu Fasihi Simulizi

Mulokozi (1996) anadai kuwa, Fasihi Simulizi ni fasihi iliyotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi. Hivyo, Fasihi Simulizi ni tukio linalofungamana na miktadha fulani ya kijamii na kutawaliwa na mwingiliano wa mambo sita ambayo ni fanani, hadhira,

fani inayotendwa, tukio, mahali na wakati. Anaendelea kusema kuwa tungo fupi fupi, kwa mfano nyimbo na baadhi ya majigambo huweza kutungwa kabla na kuhifadhiwa kichwani hadi wakati wa uwasilishwaji. Hata hivyo, fanani huwa na uhuru na kubadilisha matini ya tungo hizo wakati wowote ili kukidhi mahitaji ya muktadha wa utendaji. Maelezo ya Mulokozi yanatushawishi kukubali kuwa Fasihi Simulizi ndiyo ilichimbuka kutokana na nyimbo zenye kufungamana na mazingira ya jamii na shughuli zao za kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa.

Njogu (2006) anatuambia kwamba Fasihi Simulizi ina ubunifu na uhai wa kipekee wenye kutoa fursa njema yenye kuibua nadharia za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mtaalamu huyu anaifananisha Fasihi Simulizi na uti wa mgongo wa maendeleo ya binadamu, kwani ndani yake kuna masimulizi, maigizo, tathimini na mahusiano ya kijamii. Njogu ameongeza kwa kujadili juu ya mbinu za utungaji wa kazi za Fasihi hasa kipengele cha ubunifu ili kuvuta fikra za hadhira ambao ni muhimu kwa upokevu wa kazi yoyote ya Fasihi.

Ngure (2003) anasema kuwa Fasihi Simulizi ni sanaa inayotumia lugha, kazi hii ya sanaa itoayo maudhui yake kwa maneno ambayo hutamkwa au hutendwa. Kwa maana hiyo ili sanaa iwe fasihi simulizi lazima kuwe na sauti iliyobeba ujumbe au matendo yanayochukua nafasi ya sauti na kufikisha ujumbe kwa hadhira yake.

Kutokana na mabadiliko yanayoikumba Fasihi Simulizi hata maana zake zimekuwa zikibadilika ili ziendane na wakati ili kukidhi mahitaji ya jamii. Pia haipaswi kuangaliwa kimapokeo kama isiyobadilika kwasababu huenda sambamba na mabadiliko ya jamii.

Tanzu za Fasihi Simulizi ni nyingi na ni vigumu kuziainisha zote, wataalamu mbalimbali wamejaribu kuziainisha katika makundi yanayofanana ambayo ni hadithi, ushairi, semi na sanaa za maonesho Mulokozi (1996). Wakiziainisha tanzu hizo zinazoelekeana kwa karibu na kuziweka katika makundi tajwa hapo juu, pia wakabainisha vipera vya ushairi kama vile nyimbo na maghani.

Tukiangalia ushairi, wataalamu mbalimbali wameuelezea. Wataalamu hawa katika kueleza maana za ushairi wanatofautiana katika kusisitiza urari wa vina na mizani hawa ni wanamapokeo. Baadhi yao ni Abedi (1954), Robert (1958), na Mnyampala (1965). Kundi jingine la washairi ni la wale wasiosisitiza urari wa vina na mizani; hawa ni wanausasa. Baadhi yao ni Topan (1974), Kezilahabi (1976), na Mulokozi (1982). Vipera vya ushairi ni nyimbo na maghani. Kwa kuwa lengo la andiko ni kuangalia dhima ya nyimbo kwa mabadiliko ya jamii, hivyo halitajihusisha na maghani ambacho pia ni kipera cha ushairi simulizi bali litajishughulisha zaidi katika kuangalia nyimbo.

2.3 Maandiko Yanayohusu Fasihi na Dhima zake katika Jamii

Dhima ya Fasihi hufafanuliwa kwa njia mbalimbali kwa kulingana na majukumu yake kwa jamii. Wataalamu mbalimbali wamejadili hilo, mfano Sengo na Kiango (1973), Bgoya (1978), Eagleton (1983), Kezilahabi (1980), Msokile (1992), Syambo na Mazrui (1992), na wengine wengi. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa tunapojadili dhima ya Fasihi hatuna budi kuzingatia dhana mbili muhimu ambazo ni tabaka na itikadi. Tabaka ni makundi ya watu yanayounganishwa na uhusiano wa njia za uzalishaji mali na mfumo wa mamlaka katika jamii. Itikadi ni namna yale tusemayo na kuyaamini yanayohusiana na mfumo wa mamlaka na mahusiano ya kiutawala ya jamii tunamoishi.

Ili kuelewa vizuri uhusiano uliopo kati ya Fasihi na dhana hizo za tabaka na itikadi ni muhimu kwanza kukumbuka kuwa fasihi yoyote ile hufungamana na muktadha maalum. Muktadha ni mazingira ya kijiografia, kiutamaduni, kiuchumi, kisiasa na kiwakati. Hivyo basi kila kazi ya fasihi imefungamana na muktadha ulioizaa. Fasihi ni namna maalumu ya kuelewa na kuusawiri ulimwengu kulingana na hali ya maendeleo ya jamii inayohusika. Fasihi hudhihirisha aina fulani ya urazini na utambuzi wa hali ya maisha alionao mtunzi pamoja na wale anao wawakilisha.

Katika uhalisia kuna jamii za aina mbili, kuna zenye usawa wa mshikamano ambao huzijagawanyika katika matabaka hizi mara nyingi hukemea tabia za ubinafsi, uchoyo, majivuno, na kadhalika. Pia zipo jamii zenye mgawanyiko wa makundi na kufanya matabaka. Mahusiano ya watu hao hutawaliwa na mgawanyiko huo ambao mara nyingi hujengwa katika umilikaji wa rasilimali za jamii na mgawanyo mbaya wa mali ya jamii iliyopo. Mamlaka ya utawala katika jamii za aina hii aghalabu hushikwa na matabaka yanayomiliki uchumi, mawazo na maadili yanayotawala huwa ni ya matabaka hayo. Hivyo dhima ya fasihi katika jamii kama hiyo huonyesha mgawanyiko huo uliopo.

Fasihi huweza kuendeleza itikadi inayotawala ambayo inalinda maslahi ya wenye mali, au huweza kuipinga itikadi hiyo, ikichukua msimamo wa matabaka ya chini. Aghalabu kila tabaka huelemea upande wake. Kwa kuzingatia dhana za itikadi na tabaka ufafanuzi uliotolewa hapo juu na maoni ya wahakiki mbalimbali tuliyogusia, tunaweza kutoa muhtasari wa mambo muhimu yanayofaa kujumuishwa katika dhima ya fasihi. Hivyo fasihi inagawanyika katika maeneo kama itikadi, uchumi, utamaduni, siasa na falsafa.

Katika muktadha wa utafiti huu dhima ya fasihi simulizi katika kipera cha nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa ni kama kuelimisha, kuonya, kuadili, kukemea, kuarifu, kuburudisha, kutia hamasa, kupitisha thamani za jamii, ukombozi, kudhihaki uoga na kutumika kama rekodi ya matukio muhimu ya kihistoria. Hii ni katika kupambana na matabaka yaliyomo katika jamii ili kuleta mabadiliko.

2.4 Maandiko mbalimbali yanayohusu Nyimbo na Dhima zake kwenye Jamii

Nyimbo zina historia ndefu sana katika jamii zetu. Tunaweza kusema kwamba, nyimbo ndiyo tungo za kwanza kutumiwa na binadamu mara tu alipoanza kutumia lugha na kuweza kufanya kazi na kutoa hisia zake. Finnegan (1970:272-73) anachunguza na kujadili utanzu wa nyimbo na ushairi na kuona kuwa nyimbo ni utanzu muhimu kwa ustawi wa jamii kisiasa, kiutamaduni na hata kiuchumi. Katika ufafanuzi wake, ameonyesha kuwa nyimbo ni kipengele cha Fasihi Simulizi ambacho kilianza zamani na nyimbo zilitumiwa hata kabla ya vipengele vingine vya Fasihi Simulizi. Hata baada ya vipengele vingine kugunduliwa nyimbo zilitumika katika vipengele hivyo, navyo ni hadithi, semi na hata sanaa za maonyesho. Finnegan, katika ufafanuzi wake, ameonesha kuwa nyimbo ni utanzu wenye uwezo mkubwa kufikisha maudhui kwa jamii. Anasema,

> *It has been well said that oral poetry takes the place of newspapers among non literate peoples; songs can be used to report and comment affairs for political pressure for propaganda and to reflect and mould public opinion. This political and topical function can be an aspect of many of the types of poetry…. Topical songs often vivid personal picture of a general situation and the altitude to it as well as the specific events they comment (pg 272-73).*
>
> Imezungumzwa vema kuwa ushairi simulizi huchukua nafasi ya magazeti miongoni mwa jamii ya watu wasioelimika. Nyimbo zinawezatumika kutolea taarifa na maoni kwenye misukumo ya kisiasa kwa ajili ya propaganda na kuakisi, kuunda mawazo ya jumuiya, siasa na vitu vinavyoweza kuwa vya faida kwa ushairi mbalimbali…nyimbo hizo za kimaudhui zinakuwa zikitoa picha na

mtazamo halisi pamoja na matukio mahsusi yanayofanywa na nyimbo hizo (Tafsiri ya mtafiti).

Aidha, maelezo ya Finnegan yamefanana na Nkwera (1978) ambaye anaonesha kuwa nyimbo ni utanzu ulioanza enzi za wahenga ambao walitumia nyimbo katika ibada zao za matambiko, sherehe zao, ngoma zao na hata michezo mbalimbali ya watoto. Yeye amefafanua kuwa nyimbo ni kipengele ambacho kinapotumika katika jamii yoyote kinakuwa ishara tosha yenye kuashiria uhai wa jamii hiyo. Pia anasisitiza kuwa, nyimbo ni sehemu ya utamaduni wa jamii, na huimbwa kwa kufuata matukio yanayohusu jamii. Nyimbo huwa na ujumbe na dhima maalumu kwa jamii. Anaendelea kusema kuwa katika nyimbo kuna fumbo ambalo hutakiwa kupambanuliwa, mambo haya yanaweza kushabihiana na mazingira fulani ya maisha ya jamii. Kwa hiyo, Finnegan na Nkwera wamesisitiza kuwa nyimbo ni kipengele muhimu sana katika maisha ya binadamu ambacho ndani yake hubeba mafunzo ya hekima, malezi, ukombozi na hufikisha ujumbe kwa kutumia lugha yenye mvuto wa hisia na vionjo na picha dhahiri zaidi ya mwimbaji na mambo anayoeleza, nyimbo ni kielelezo fasaha zaidi kuliko maneno hayohayo yakitamkwa kwa mtindo wa mazungumzo ya kawaida. Utafiti wao haujagusia kabisa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kutokana na ukweli kwamba maandiko yao yaliandikwa wakati Bongo Fleva ilikuwa haijazaliwa. Lakini mawazo yao ni ya muhimu katika utafiti huu kwa sababu yanatoa dira kwa mtafiti kufikia malengo ya utafiti.

Naye Senkoro (1987:17), pamoja na kuelezea umuhimu wa nyimbo katika jamii na mazingira yao amefafanua kuwa nyimbo zina historia ndefu ya maisha ya jamii, na katika kushadidia hilo anaeleza kuwa,“Baada ya kuzuka kwa lugha, Fasihi ya mwanzo ilifuata. Hii haikutokana na Mungu, wala haikutokana na hisi tu. Fasihi hii

ilitokana na kazi alizofanya mtu katika kupambana na mazingira. Polepole, alianza kutunga maneno na sauti zilizofuatia mapigo ya zana za kazi. Baada ya muda alizitumia sauti hizo za mapigo ya zana za kazi kujiimbia nyimbo wakati wa kazi. Wimbo wa kazi ukawa ndiyo fasihi ya mwanzo”

Akieleza fasili ya ushairi, Senkoro (1988) anamnukuu Mnyampala, akisema kuwa ushairi ni msingi wa maneno yenye hekima tangu kale na ndicho kitu kilicho bora katika maongozi ya dunia, kwa kutumia lugha ya mkato na lugha nzito. Kwa kutumia fasili hii ya ushairi, ni wazi kwamba nyimbo zote hujengwa kwa lugha iliyojaa tamathali za semi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira husika. Maelezo ya maana ya ushairi yaliyotolewa na Mnyampala yanatoa mwanga zaidi katika kuelewa dhana ya nyimbo. Hata hivyo, si kweli kwamba kila wimbo huwasilisha maneno yenye hekima kwa kutumia lugha nzito.

Songoyi (1988) amechunguza juu ya mchango wa utanzu wa nyimbo za wasanii Kalikali na Mwinamila; ambapo, aliangalia athari za kimuktadha wa kiutendaji. anabainisha kwamba nyimbo zina mchango mkubwa katika mabadiliko ya jamii kwa kutazama shughuli, utamaduni, furaha, na matatizo ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii. Akifafanua zaidi, anaona kuwa mabadiliko ya jamii kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni yanayotokea yanachangiwa na sanaa ya utanzu wa nyimbo na ngoma. Aidha katika uchambuzi wa nyimbo za Kalikali na Mwinamila alichunguza maudhui na jinsi yanavyosaidia kuleta mabadiliko katika jamii lakini hakushughulikia nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwani utanzu huu umechomoza baadaye, ambapo ndiyo lengo la utafiti wetu huu ambalo ni kuchunguza dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii ili kuziba pengo.

Mulokozi (1996) anafafanua kuwa wimbo ni kila kinachoimbwa. Hivyo hii ni dhana pana inayojumuisha tanzu nyingi. Hata baadhi ya tanzu za kinathari, kama vile hadithi, huweza kuingia katika kundi la nyimbo pindi zinapoimbwa. Nyimbo ni tungo zinazoimbwa na huwa na mahadhi ya sauti inayopanda na kushuka. Tungo hizi huundwa na hutoa wazo kwa namna inayovuta hisia kutokana na mpangilio maalumu wa maneno yaliyoteuliwa kwa lugha ya mkato, matumizi ya picha, tamathali za semi zinazowasilishwa kwa njia ya wimbo au maandishi na mapigo ya silabi. Huweza kuambatana na ala za muziki kama vile ngoma, pembe, vugo, marimba, zumari, chapuo, kinanda, gitaa na kadhalika. Mambo muhimu yanayotambulisha nyimbo ni muziki wa sauti ya mwimbaji au waimbaji, muziki wa ala (kama zipo), hadhira inayoimbiwa, muktadha unaofungamana na wimbo huo, kwa mfano sherehe, ibada, msiba, ufugaji, uwindaji ndege shambani, kuvuna na yanayofanana na hayo, na matini au maneno yanayoimbwa. Kama alivyo Finnegan, Mulokozi (1996) amefanikiwa sana kueleza dhana na dhima za nyimbo.

Tofauti na Finnegan, Mulokozi ameenda mbele zaidi kwa kuziainisha nyimbo kulingana na matukio mbalimbali ya kijamii, anazigawa katika makundi manne muhimu ambayo ni tumbuizo, chapuzo, tukuzo na tendi/tenzi. Pamoja na kuimbwa nyimbo zina maudhui muhimu kwa ustawi wa jamii katika siasa, utamaduni na uchumi. Pia, anaendelea kueleza kuwa, nyimbo ni utanzu mkongwe katika jamii zote. Nyimbo ni chombo ambacho huwakuza watoto kiutamaduni kadri wanavyokua hadi wanapokutana na fasihi nyingine kama vile ngano. Nyimbo ni kiunganishi muhimu cha utamaduni kati ya kizazi kimoja na kingine. Kwa kuwa nyimbo hutumika kueleza utamaduni wa jamii fulani, basi nyimbo ni utamaduni wa jamii zote, utamaduni na jamii ni vitu viwili visivyoweza kutenganishwa sawa na pande mbili za shilingi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kuna muunganiko mkubwa kati

ya nyimbo na maisha ya kila siku ya jamii. Inaaminika kuwa katika shughuli za kila siku za mwanadamu tangu hapo kale hata sasa, kwa kiasi kikubwa hutawaliwa na nyimbo zenye hisia ya furaha au huzuni.

Naye Wamitila (2003) anashadidia kwamba nyimbo zina dhima kubwa kwa mabadiliko ya jamii kwa sababu hubeba mawazo mazito yenye dhamira ya kuonesha uhusiano wa jamii katika mambo mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Aghalabu shughuli nyingi za binadamu huambatana na nyimbo zinazobeba maudhui yanayoendana na muktadha wa shughuli husika katika jamii. Anaendelea kusema kuwa nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa sana kwa jamii. Hutumika katika kuburudisha watu, kuonya, kuarifu, kufunza, kuomboleza, kubembeleza watoto, kuchapuza kazi na kutia hamasa. Matumizi haya ya nyimbo huzifanya nyimbo kuwa na majukumu ya kutumiwa kama nyenzo muhimu ya kupitisha thamani za kitamaduni katika jamii mbalimbali. Hutumiwa kama rekodi za matukio muhimu ya kihistoria katika jamii, hutumiwa kuwahamasisha watu kushirikiana katika kuchangamkia jambo fulani. Kwa maana hiyo, nyimbo ni kiakisi kizuri cha fahari waliyo nayo watu katika utamaduni wao.

Ngure (2003) anaeleza kwamba wimbo ni utungo wenye mdundo na mahadhi yanayoweza kuimbika, nyimbo ni utanzu maarufu sana katika jamii. Anaona shughuli nyingi huambatana na nyimbo na hivyo kupitia nyimbo jamii hujifunza, huomboleza, hufarijika, na hutiana moyo.

Nui kuu za nyimbo za hapa Afrika Mashariki ni tumbuizo, tukuzo, chapuzo, tenzi/tendi. Wataalam waliojadili mgawanyo huo wa nyimbo ni pamoja na Nkwera (1978), Songoyi (1988), Mulokozi (1996), Kimera (2008), Shani (2008), na Sekile

(2011). Mgawanyo huu wa nyimbo umekuwepo katika kuangalia jamii kiutamaduni, kiuchumi, kisiasa, na kijamii.

Songoyi (2005), katika andiko lake amemnukuu Babalola anaeleza kuhusu fani na maudhui katika ushairi wa *Ijala* kwamba nyimbo zina mahadhi ya kishairi ambayo yanaelezea fikra na hisia mbalimbali zinazozunguka watu wa jamii fulani. Ingawa andiko hilo halikushughulikia nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa na dhima zake kwa mabadiliko ya jamii, jambo ambalo limemfanya mtafiti kuchunguza nyimbo hizo. Kazi hiyo imetoa fursa ya kutambua dhima inayofanywa na utanzu huu wa nyimbo za Bongo Fleva katika Fasihi Simulizi. Kazi hiyo imempa mtafiti msukumo unaotokana na maelezo ya kuwa nyimbo ni kiwakilishi cha hisia na fikra za watu na jamii. Hivyo, utafiti huu unalenga kuchunguza dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa ambayo imekuwa kikwazo kikubwa cha maendeleo katika jamii na mafanikio ya nyimbo hizo kifani na kimaudhui kwa mabadiliko ya jamii.

Naye Mdee (2009), anaeleza kwamba nyimbo ni tungo za ushairi zenye kutumia mahadhi, melodi, mapigo na muwala, hutambulishwa na mambo muhimu kama muziki wa ala (kama upo), matumizi ya maneno yanayoimbwa na muktadha unaofungamana na wimbo huo; kama vile, sherehe, ibada na msiba. Maelezo ya Mdee yanaonyesha namna nyimbo zinavyofungamana na shughuli na maisha ya jamii ya kila siku, mathalani, sherehe za kijamii, kiutamaduni, matatizo, mikasa, maovu na majanga yanayozikumba jamii kwa ujumla ikiwemo umasikini, magonjwa, unyanyaswaji wa kijinsia, ubaguzi na matabaka, rushwa likiwa ni mojawapo ya matatizo yaliyomo katika mazingira ya jamii za Tanzania kwa wakati huu.

Simiyu (2011) anaeleza kwamba nyimbo ni kiakisio muhimu kinachoashiria mabadiliko ya jamii katika maisha ya binadamu, maelezo yake yanaonesha kuwa na mashiko yanayoonesha mguso unaotokana na ujumbe kuwasilishwa kwa utanzu wa nyimbo. Anaendelea kusema, nyimbo husheheni mawazo mazito na hudhamiria kuonesha uhusiano wa kijamii, migogoro ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kupitia nyimbo jamii hubadilika, huburudika, hujifunza, huongolewa, huomboleza na hupitisha amali zake na historia. Aghalabu nyimbo huwa na uteule wake wa majukumu kwani hupitisha hueleza na kuathiri hisia za ndani za watu na zina historia kongwe sana kwani inakisiwa kwamba punde tu binadamu alipojifunza lugha basi alianza kuimba mashairi. Maelezo ya watafiti tangulizi yanatoa dira muhimu kwa utafiti wetu kwasababu ni vyanzo muhimu vya marejeleo katika utafiti wetu.

2.5 Maandiko Kuhusu Nyimbo za Bongo Fleva na Dhima zake kwa Jamii

Historia ya muziki wa Bongo Fleva hapa Tanzania inaanzia katika muziki wa Hip Hop, mnamo miaka ya 1980 mpaka 1990, na watoto wa kitanzania waliokwenda masomoni nchi za nje. Watoto hao walikuja na vifaa vya muziki wa kigeni kama vile kanda, video na majarida ya muziki kuhusu wasanii wa muziki wa Kimarekani, Kiingereza, na nchi nyingine za Ughaibuni. Wakati wa likizo, kama ilivyo kawaida ya maisha ya watu waishio mikoa ya pwani ya bahari ya Hindi, hususani Mkoa wa Dar es Salaam hupenda kukutana na marafiki katika fukwe za bahari hiyo kwa lengo la kujiburudisha. Katika sherehe hizo madijei waliokuwa wakipiga muziki walimpa kipaza sauti mtu yeyote aliyependa kuimba na ndipo walipoanza kuimba muziki huo katika lugha ya Kiswahili na kufanya nyimbo kama muziki kukua na kufanya vijana wengi kujiunga. Vijana hao waliubadilisha jina muziki huo na kuuita Bongo Fleva. Bongo Fleva hujumuisha aina mbalimbali za nyimbo za kizazi kipya nchini Tanzania ambazo ni *rap, rythym na blues (R&B), dance hall, raga*, zuku *(zouk*). Bongo Fleva

ni nyimbo zilizorekodiwa kikompyuta na vifaa vingine vya kielektroniki. Nyimbo hizi zinatumia vionjo vya kiridhimu, mapigo, midundo na sauti kutoka nchi za kimagharibi na kiafrika. Nyimbo za Bongo Fleva zinachanganya vionjo mbalimbali vya kitamaduni, kimuziki na kifasihi vya ndani na nje ya Tanzania ili kutengeneza nyimbo zenye upekee (Perullo, 2003; Mangesho, 2003; Masonga, 2005; na Omari, 2009). Pamoja na wataalamu mbalimbali kushughulikia nyimbo za Bongo Fleva, suala la nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa halijashughulikiwa vya kutosha na hilo ndilo lililo mpa nafasi mtafiti kulishughulikia na kuziba pengo hilo.

Nyimbo za Bongo Fleva zina mashiko sana katika jamii yetu kwa sasa. Mashiko haya ni kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Hata hivyo, kuna watu wanaobeza nyimbo hizi kutokana na kwamba wanaona zinapotosha jamii, hili linajidhihirisha sana kutokana na uchezaji, mavazi, mitindo ya maisha na matumizi ya lugha katika uimbaji wa nyimbo hizi. Pamoja na hayo wasikilizaji wanapaswa kupembua kile tu kilicho kizuri na kuachana na kisichofaa. Nyimbo hizi zinapendwa sana na sehemu kubwa ya jamii ya watanzania. Kwa wanafasihi, mashairi ya Bongo Fleva ni muhimu kwani ni sehemu ya kipera cha Fasihi Simulizi ya Kiswahili (Msuya na Lupokela 2010). Hata hivyo, hawajajadili suala la nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii.

Nyimbo za Bongo Fleva katika jamii zimekuwa zikitumika kuburudisha na kuelimisha wanajamii katika taratibu za maisha ya kila siku, kama tangu zamani nyimbo zilivyotumika. Nyimbo ziliambatana na shughuli za kila siku kama vile kilimo, uvuvi, kutwanga na shughuli nyingine katika jamii.

2.6 Pengo la Utafiti

Mapengo yanayojitokeza katika maandiko pamoja na wataalamu kuchambua mambo mbalimbali katika maandiko yao, suala la nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa Mabadiliko ya Jamii halijashughulikiwa kwa kiwango cha kutosha. Hivyo uchunguzi wa dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii haujaelezwa kwa kiwango cha kutosha.

Pia kazi hizo hazijaonesha nyimbo za Bongo Fleva za kutosha zihusuzo rushwa. Zaidi mbinu za kifani zinazotumika katika kuwasilisha nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa hazija chunguzwa ili kuzibainisha kwa uwazi. Kwa hiyo, utafiti huu unakusudia kuziba mapengo hayo.

SURA YA TATU

MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sehemu hii inajadili mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti kwa ujumla, eneo la utafiti, jamii ya watafitiwa, mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti, pamoja na njia zilizotumika kuchambua data za utafiti zilizo kusanywa.

3.2 Utaratibu wa Utafiti

Utafiti huu umetumia data za uwandani na katika kimaktaba. Mtafiti alikusanya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kutoka sehemu mbalimbali, kisha kuzichambua na kuzibainisha dhima zinazopatikana katika nyimbo hizo. Kwa kiasi kidogo utafiti umefanyika uwandani ambako mtafiti alifanya mahojiano na watu wa makundi mbalimbali wanaosikiliza na wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa ili kupata data zitakazosaidia katika utafiti huu.

Pia, mbinu ya ufafanuzi wa data imetumika kutoa matokeo ya utafiti. Data zote zilizokusanywa kutoka kwa watafitiwa walioko uwandani baada ya mahojiano zimechunguzwa na kuhakikiwa na kisha kutolewa taarifa katika maandishi kwa ajili ya tafiti zijazo.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika Mkoa wa Mbeya. Mkoa huu ulichaguliwa kutokana na kuwepo kwa watafitiwa wa makundi yote yaliyotarajiwa kutafitiwa. Pia ni eneo ambalo mtafiti anakoishi, hii ilimsaidia kupunguza gharama za maisha.

3.4 Walengwa wa Utafiti

Watafitiwa walikuwa ni watu wa rika mbalimbali wanaosikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika Jamii.

3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Jamii iliyolengwa ili kutoa taarifa za utafiti huu ilijumuisha makundi yafuatayo:

a) Watu mbalimbali wa rika mbalimbali wanaosikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika Jamii. Idadi ya watafitiwa ilikuwa thelathini, na;

b) Wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

3.4.2 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli inaakisi sifa za populesheni yote pale ilipochukuliwa. Katika utafiti huu, usampulishaji ulifanyika katika kuteua mada ya utafiti, maeneo ya kukusanyia data za utafiti na watu husika katika kupata data za msingi. Utafiti ulitumia usampulishaji holela katika kuteua eneo lililohusika katika utafiti huu. Uteuzi wa watu ulifanywa kwa usampulishaji wa kinasibu, kwa kuzingatia kigezo cha umri, uelewa wa kina na kuwa mkazi wa eneo teule, kila mtu alikuwa na nafasi sawa ya kushiriki.

Mbinu ya sampuli lengwa ilitumika kuwapata watafitiwa ambao ni wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva; ambapo, watafitiwa walichaguliwa kutokana na sifa zao za usanii wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Sifa hizi ziliwaruhusu kuwa watafitiwa wa kutoa data za utafiti. Kwa upande mwingine, sampuli holela ilitumika kuwapata watafitiwa kutoka katika jamii, ambapo yeyote katika kundi kubwa la watu alikidhi haja na alikuwa na fursa sawa ya kuwa mtoa data za utafiti kutokana na maswali aliyoulizwa na kuyajibu katika mahojiano na mtafiti.

3.4.2.1 Sampuli Lengwa

Wasanii watatu waliwakilisha kundi kubwa la wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zilizotumika katika utafiti kwa kuzichambua ili kupata data za utafiti. Wasanii waliohojiwa na kupata data za utafiti ni hawa wafuatao;

a) Joseph Mbilinyi

b) Joseph Haule

c) Emanuel Bryson

3.4.2.2 Sampuli Holela

Sampuli hii ilihusisha watu mbalimbali wa rika mbalimbali wanaosikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii. Idadi yao ilikuwa thelathini, kwa mgawanyo ufuatao.

3.4.2.2.1 Sampuli ya Wanafunzi

Vijana kumi na tano; wa kike nane na wa kiume saba wa eneo lililotafitiwa walihojiwa. Vikundi vitatu vya wanafunzi watano kila kimoja walifanya majadiliano na mtafiti ili kutoa mwanga kuhusiana na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa katika jamii.

3.4.2.2.2 Sampuli ya Vijana

Vijana kumi wanaosikiliza na wenye ufahamu kuhusu nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa; watano wa kike na watano wa kiume kutoka sehemu mbalimbali za eneo la utafiti. Hawa walihojiwa kwa nyakati tofauti ili kutoa data za utafiti.

3.4.2.2.3 Sampuli ya wazee

Wazee watano, wawili wanawake na watatu wanaume wenye ufahamu juu ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kutoka eneo la utafiti, walihojiwa ili kutoa mwanga wa utafiti wetu na kumfanya mtafiti kupata data za utafiti.

3.5 Ukusanyaji wa Data

Kipengele hiki kinaelezea zana mbalimbali zilizotumika katika kukusanya data na zoezi la ukusanyaji wa data kutoka uwandani/ eneo la utafiti.

3.5.1 Zana za Kukusanyia Data

Zana zilizotumika kukusanyia data za utafiti huu zilikuwa ngamizi (*computer*), radio, kinyonyeo (*flash*), simu, maswali ya usaili (hojaji), vijidaftari, kalamu, kamera, na kinasa sauti.

Picha 1: Baadhi ya zana zilizotumika katika kufanikisha mchakato mzima wa uandishi wa utafiti huu. (Chanzo: Utafiti, 2013)

Zana hizi zilitumika kukusanyia data kwa sababu utafiti huu ulijumuisha watu wenye tofauti za upeo na maeneo tofauti ya kijiografia. Hii yote ililenga kurahisisha utunzaji wa data mbalimbali toka kwa watu mbalimbali. Data kutokana na matukio mbalimbali zilichukuliwa na kutunzwa katika kamera na kinasa sauti.

3.5.1.1 Redio na Kinyonyeo (*Flash*)

Redio na kinyonyeo vilitumika katika kurekodi na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa ili kumsaidia mtafiti kuzisikiliza na kuziandika kwa lengo la kurahisisha tendo zima la uchambuzi ili kupata data kusudiwa.

3.5.1.2 Maswali ya Usaili (Hojaji)

Haya ni maswali ya ana kwa ana au kwa njia ya simu kati ya mtafitiwa na mtafiti pamoja kufanya mahojiano, ambapo mtafiti aliandaa maswali yote yanayotakiwa katika utafiti katika karatasi na kumuuliza mtafitiwa kwa mpangilio mzuri. Pia maswali hayo yaliruhusu uhuru wa mtafitiwa kujibu maswali. Njia hii ilitumika kukusanya data toka kwa wasanii na wasikilizaji mbalimbali wa rika mbalimbali wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii.

Katika kuieleza mbinu hii ya ukusanyaji wa data, Seidman (1991) amenukuliwa na Ntiluhoka (2007) akisema kuwa:

> *Interview is a common and important method in qualitative research. It refers to an exchange of views between two or more people on topics of mutual interest see the centrality of human interaction.*
>
> Mahojiano ni mbinu muhimu inayotumika katika utafiti unaotumia mbinu za kifafauzi/ kitaamuli. Inahusisha kubadilishana mawazo kati ya watu wawili au zaidi kuhusu mada fulani inayotafitiwa, mbinu hii inasisitiza umuhimu wa kuhusisha mawazo toka kwa watu tofautitofauti wakati wa kukusanya data za utafiti (Tafsiri ya mtafiti).

3.5.1.3. Daftari na Kalamu

Zana hizi zilitumika katika kuchukulia data wakati wa mahojiano baina ya mtafiti na mtafitiwa. Data ziliandikwa katika vijidaftari maalumu, na baadaye kutumika kutolea taarifa ya utafiti baada ya uchambuzi.

3.5.1.4 Kamera na Kinasa Sauti

Kamera ilitumika katika kuchukulia picha tuli, na kinasa sauti kilitumika kurekodi sauti za watu mbalimbali waliohojiwa wakati wa mahojiano. Picha tuli katika kamera, na sauti zilizorekodiwa katika kinasa sauti zilimsaidia mtafiti katika kuzichambua na kuzitathimini data zilizopatikana wakati wa utafiti.

3.5.1.5 Simu ya Mkononi

Kifaa hiki kilikuwa muhimu sana kwani kilitumika katika kumuunganisha kimawasiliano mtafiti na watafitiwa kila ilipowabidi kuweka miadi ya kukutana ili kuweza kuitimiza adhima ya mahojiano kwa ajili ya kupata data za utafiti zilizokusudiwa na utafiti.

3.5.1.6 Ngamizi (*Computer*)

Zana hii pia ilitumika katika kutunzia data kutoka kwenye kamera na kinyonyeo (*flash*) zilizopatikana uwandani. Hii ilifanyika kila mtafiti alipotoka uwandani kwa mahojiano na watafitiwa. Kitendo hiki kiliruhusu kupatikana kwa nafasi ya kutosha katika kamera na kinyonyeo kwa ajili ya zoezi la siku iliyofuata.

3.5.2 Mbinu zilizotumika katika Ukusanyaji wa Data

Sehemu hii inaelezea mbinu za utafiti zilizotumika katika upatikanaji wa data za utafiti ambazo ni data za maktabani pia data za uwandani.

> Katika utafiti unaojihusisha na maisha halisi ya jamii mara nyingi inabainika kuwa data anazokuwa nazo mtafiti mkononi hazitoshi na kwa hali hiyo lazima ukusanyaji wa data za uwandani ufanyike ili kukidhi mahitaji muhimu kitaarifa/ kidata kuna mbinu mbalimbali katika kukusanya data za msingi kutokana na hali halisi ya gharama hasa kifedha, muda na rasilimali anazoweza kupata mtafiti. (Kothari, 2004:17)

Katika kutafuta data za msingi za uwandani kwa ajili ya utafiti, Mtafiti alitumia mbinu mbalimbali mfano utafiti wa nyaraka, mahojiano binafsi na majadiliano katika vikundi.

3.5.2.1 Udurusu wa Nyaraka

Upitiaji wa nyaraka mbalimbali za watafiti ni mbinu inayohusu usomaji wa kina wa nyaraka hizo toka maktabani au katika mitandao mbalimbali ya kijamii. Nyaraka hizo zinaweza kuwa ni vitabu, majarida, tasinifu za watafiti wengine kwa madhumuni ya kuchunguza jinsi watafiti hao walivyojadili juu ya nyimbo na dhima zake kwa jamii. Mapitio ya nyaraka hizo yalimpa mwelekeo mtafiti kwa kumwonyesha kama kuna pengo lililohitajika kuzibwa kutoka kwenye tafiti zilizotangulia. Upitiaji wa kazi mbalimbali za waandishi uliambatana na uhakiki, uchambuzi na utoaji wa maoni juu ya kile ambacho watafiti wamebainisha ili kutumia mawazo yao kuboresha utafiti huu.

3.5.2.2 Mahojiano

Mbinu hii ya usaili ilitumiwa na mtafiti kwa ajili ya kupata data kutoka kwa watafitiwa. Usaili wa ana kwa ana na kwa njia ya simu kwa watafitiwa ambao haikuwezekana kuwapata kwa urahisi na kuweza kufanya usaili ulitumika. Mtafiti aliwauliza watafitiwa wote maswali yaliyoandaliwa kwa mfumo uleule kutoka

mtafitiwa mmoja hadi mwingine. Watafitiwa walijibu maswali kama walivyoulizwa, hii ilimsaidia mtafiti kupata data husika.

3.6 Mchakato wa Ukusanyaji na Udhibiti wa Data

Ili kufanikisha zoezi la utafiti, Mtafiti aliomba ruhusa kutoka kwa mamlaka zinazohusika ili kuruhusiwa kufanya utafiti katika maeneo mbalimbali yaliyolengwa. Hii ilimwezesha kuruhusiwa kukusanya data katika maeneo yaliyokusudiwa. Vilevile, mtafiti aliomba ridhaa ya watu binafsi ili watafitiwe ikiwa ni pamoja na kupigwa picha na kurekodiwa sauti. Aidha kufuatwa kwa maadili ya utafiti kuliwahakikishia kwa pamoja mtafiti na watafitiwa wote, utunzaji wa siri za data zilizotolewa baina ya watu wa pande hizi mbili. Data kutoka eneo la utafiti zilikusanywa kwa ridhaa maalum kutoka kwa watafitiwa kwa kutumia vifaa kama vile hojaji, kamera, kinasa sauti.

3.7 Uchakataji wa Data

Baada ya zoezi la kukusanya data kukamilika. Mtafiti alisikiliza, kuziangalia picha jongezi na kuziandika katika karatasi nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zilizokusanywa kutoka uwandani. Uchambuzi wa data zilizopatikana uwandani kwa kutumia hojaji, na picha ulianza, ambapo mbinu ya ufafanuzi wa mawazo yaliyojitokeza katika data hizo ulitumika. Mawazo ya utafiti yalichambuliwa na kuwekwa katika makundi kwa kufuata malengo ya utafiti huu. Kila lengo liliunda mada ndogo ndogo zenye kubeba mawazo yanayofanana na lengo hilo. Mawazo ya kila lengo yalifafanuliwa kwa kina kutoka kwenye nyimbo husika yakilinganishwa na uhalisia wa maudhui yake. Tendo hili lilimsaidia mtafiti kuzielewa nyimbo zinazojibu maswali yaliyoandaliwa kwa ajili ya kukidhi haja ya utafiti.

3.8 Vikwazo vya Utafiti

Mchakato mzima wa utafiti huu ulikabiliwa na baadhi ya vikwazo mbalimbali. Baadhi ya vikwazo hivyo ni kama vile kutopatikana kirahisi kwa watafitiwa kutokana na kuzongwa na majukumu kadhawakadha ya kijamii. Hata hivyo mawasiliano kwa njia ya simu ilitumika ili kukabiliana na kikwazo hiki. Kikwazo kingine kilikuwa baadhi ya watafitiwa kuhitaji pesa nyingi ili waweze kutoa taarifa za utafiti. Katika hili elimu na ushawishi wa mtafiti kwa watafitiwa ulichukua nafasi zaidi ili kukidhi tatizo hili. Vilevile, watafitiwa wa utafiti kutokuwa tayari kupigwa picha ambazo zingezidisha uhalisia wa mambo katika utafiti huu. Baadhi ya picha zilipatikana na kutumika kama kielelezo cha utafiti. Pia ukosefu wa fedha kilikuwa kikwazo kingine cha utafiti huu, kwani ilichangia sana mtafiti kutofika baadhi ya maeneo kwa ajili ya kupata taarifa na hii ilitokana na ufinyu wa vyanzo vya mapato vya mtafiti mwenyewe na hii iliathiri hatua mbalimbali za utafiti huu. Njia ya mawasiliano kwa simu ilitumika zaidi ili kupata data hizo, na kufanya utafiti kukamilika salama.

SURA YA NNE

MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Mjadala huu umegawanyika katika sehemu kuu tatu kulingana na maswali makuu yaliyouongoza utafiti huu. Sehemu ya kwanza inaonesha nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa katika jamii. Sehemu ya pili inajadili dhima zinazojitokeza katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Sehemu ya tatu inajadili kuhusiana na mwitikio wa jamii juu ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

4.2 Nyimbo za Bongo Fleva Zihusuzo Rushwa

Mnenuka (2010/2011), akiwanukuu watalaamu mbalimbali anasema kuwa wanafasihi na watalaamu mbalimbali wa sanaa wanakubali kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya sanaa na jamii. Kutokana na uhusiano huu, maudhui ya kazi za kisanii huakisi mtazamo, upeo na utamaduni wa jamii. Wasanii hujikuta wakitunga kazi zinazoakisi jamii kwa kudhamiria au kutokudhamiria (Blommaert, 2006). Muziki wa Bongo Fleva, kama zilivyo sanaa nyingine, hauna uwezo wa kupingana na ukweli huo. Kutokana na athari hizo, muziki wa Bongo Fleva huzungumzia masuala mbalimbali yanayoihusu jamii kijamii, kiuchumi na kisiasa (Omari, 2009). Hii inadhihirika pale U-marx unaposema kuwa Fasihi ni umbo maalumu, umbo hilo hupatikana katika hali yoyote ya jamii. Pia, hii ni kwa sababu ya mahusiano maalumu ya kitabaka, kiutamaduni, kisiasa na kijamii ambayo hubebana na msingi uliopo. Athari hizo zinatokana na sababu mbalimbali zikiwemo zile zinazohusisha aina ya muziki wenyewe. Kwa mfano, wasanii wengi wa muziki wa kufokafoka hujitambulisha kwa kudai haki na kukemea uovu wa aina yoyote ile katika jamii. Nyimbo za utongoaji mashairi vilevile, huelezea uovu na kuhamasisha matendo ya

kistaarabu katika jamii. Kwa ujumla, masuala yote yanayojadiliwa katika muziki wa Bongo Fleva hutokea katika jamii kwa namna na viwango mbalimbali.

Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zilizotumika katika utafiti wetu ni zile ambazo zimeimbwa na wasanii mbalimbali kwa kutalii na kujadili mambo mbalimbali ikiwemo rushwa kwa lengo la kuleta mabadiliko katika jamii. Mtafiti katika kukidhi haja ya utafiti alikusanya na kusikiliza idadi ya nyimbo za Bongo Fleva sabini na tano (75) na kubaini idadi ya nyimbo za Bongo Fleva ishirini na sita (26) za wasanii (wametajwa mbele) zinakidhi haja ya utafiti huu, na ndizo zilizotumika katika utafiti.

Picha 2: Mtafiti akiwa katika moja ya maktaba za muziki zilizopo katika maeneo ya Mwanjelwa Jijini Mbeya (Chanzo: Utafiti, 2013).

Nyimbo za Bongo Fleva zifuatazo hapo chini zimekusanywa, kuchambuliwa maudhui yaliyomo kisha kubainika kuwa na sifa za kukidhi haja ya utafiti wetu. Pamoja na kuzungumzia mambo mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni pia zimejadili rushwa ambalo ni tatizo linaloisumbua jamii ya kitanzania kwa kiwango kikubwa:

1. “2030”- Roma Mkatoliki ft Story
2. “Mr President”- Roma Mkatoliki
3. “Tanzania”- Roma Mkatoliki
4. “Police man”-Ferooz Mrisho
5. “Mtazamo”- Solo Thang ft Profesa Jay, Afande Sele
6. “Miss Tanzania”- Solo Thang
7. “Mr Politician”- Nakaya Sumari
8. “Albino Fulani”- Mwana FA ft Sugu
9. “Nauza kura yangu”- Bonta
10. “Nang’atuka”- Profesa Jay
11. “Ndiyo Mzee”- Profesa Jay
12. “Siyo Mzee”- Profesa Jay
13. “Rushwa”- Mapacha
14. “Bei ya mkaa”- Weusi
15. “Ridhiwani”- Izzo B
16. “Traffic huyo”- Wagosi wa Kaya
17. “Joto hasira”- Lady Jay Dee
18. “Darubini kali”- Afande Sele
19. “Wizi mtupu”- Kala Jeremiah
20. “Mwalimu angekuwepo”- Kala Jeremiah ft Nakaya Sumari
21. “Hapo zamani”- Sugu
22. “Mikononi mwa Polisi”- Sugu
23. “She is my # 1”- Nemo ft Omy Dimpoz
24. “Majanga”-Snura
25. “Sumu ya teja”- Vitalis Maembe
26. “Fununu”- Young D ft Ben Paul, Mwana F.A

4.3 Dhima ya Nyimbo za Bongo Fleva Zihusuzo Rushwa kwa Mabadiliko ya Jamii

Maadili na malezi ni nguzo muhimu sana katika mwenendo mzima wa maisha ya binadamu. Historia ya jamii zetu inaonesha kwamba suala la maadili na malezi lilizingatiwa sana na lilifundishwa tangu maisha ya utotoni. Miongoni mwa mbinu zilizotumika kufundishia ni nyimbo. Hivyo utafiti huu una lengo la kuonesha dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii. Hata hivyo nadharia ya U-marx inaamini kuwa mabadilko hayafanyiki kwa urahisi, yanapaswa yafanywe hatua kwa hatua. U-marx unajidhihirisha pia kihistoria, kuwa mabadiliko katika mfumo wa jamii hutokea wakati jamii inapofikia hatua fulani ya maendeleo inayoibua migongano kati ya muundo wa juu wa utawala na muundo msingi. Migongano hiyo huibuka kutokana na mahusiano ya kinyonyaji kati ya pande hizo mbili. Mabadiliko huanza kutokea kwenye upande unaoathirika.

Nyimbo za Bongo Fleva zina mashiko sana katika jamii yetu kwa sasa. Hii ni kutokana na mabadiliko ya mfumo wa maisha kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kama tutakavyojadili mbele. Kwa wanafasihi, mashairi ya Bongo Fleva ni muhimu kwani ni sehemu ya kipera cha fasihi simulizi ya Kiswahili. Hata hivyo kuna mawazo tofauti kwa wanajamii kuhusu nyimbo hizi. Baadhi ya watu wanaona kuwa nyimbo hizi hupotosha jamii. Mawazo haya hutokana na uchezaji, mavazi, mitindo ya maisha na matumizi ya lugha katika uimbaji wao. Mulokozi (1996) anatuambia kuwa, ikumbukwe kwamba fasihi inaweza kuelimisha na kupotosha jamii pia, pale isipotumika vizuri. Kwa hiyo ni jukumu la jamii kupembua yale mambo yaelimishayo na kuyatumia kwa maendeleo ya jamii ya kitanzania.

Picha 3: Baadhi ya wanafunzi walioshiriki mjadala kuhusu nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Wanafunzi hawa ni kutoka shule ya sekondari Sinde iliyopo katika halmashauri ya Jiji la Mbeya (Chanzo: Utafiti, 2013).

Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinaweza kutumika kusisitiza maadili na makuzi yenye kumjengea mtu tabia njema inayokubalika kwa jamii. Hii inawezekana kwa kupata ujuzi, mafunzo, tabia na mwenendo unaofaa kwa jamii. Nyimbo za Bongo Fleva hupendwa na vijana wengi nchini Tanzania, hivyo ni rahisi kupitisha mafunzo muhimu na kuwafikia. Tangu kale nyimbo zimekuwa zikitumika katika kuburudisha, kuelimisha, kuonya, kuadili, kuarifu, kuomboleza, kubembeleza, kutia hamasa, kuchapuza kazi, kupitisha thamani za jamii, na kutumika kama rekodi ya matukio ya kihistoria. Zifuatazo ni dhima zinazojitokeza katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika kuleta mabadiliko kwa Jamii:

4.3.1 Kuelimisha

Jamii inatambua kwa kiasi kikubwa mchango wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazotumika katika kuelimisha jamii juu ya wajibu wake katika kujiletea mabadiliko. Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinaweza kutumika kama njia ya kufikisha ujumbe kwa jamii kueleza matumaini, masononeko, kukata tamaa na matarajio.

Utafiti umebaini juu ya utawala bora kwamba ili jamii iendelee kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ni lazima iwe na viongozi bora ambao walipatikana kwa njia halali. Kiongozi mwenye maadili na makuzi bora tangu utotoni hufanya kazi yake kwa masilahi ya jamii nzima. Na inapotokea kiongozi huyo hakuenenda sawasawa na matakwa ya jamii kwa kuiingiza nchi pamoja na jamii kwa ujumla wake katika hasara. Hata kujinufaisha yeye binafsi kinyume na kiapo cha kazi yake, ni vema aachie ngazi ili kutoa nafasi kwa watu wengine wenye mapenzi mema na wenye uwezo wa kuutumikia umma. Katika kulizungumzia hilo, msanii Joseph Haule (Profesa Jay) katika wimbo wake “Nang’atuka” anasikika akisema.

Wimbo: “Nang’atuka”- Profesa Jay

Napiga goti natubu kwa Mungu wangu na jamii
Nimefanya maovu mengi kwa kutumia cheo
Nikaamini cheo dhamana mnisamehe (mnisamehe)
Nang’atuka (nang’atuka)
Mola wangu nisamehe
Nimeshaikosea jamii nikajiita Mungu mtu nikajiita nabii
Nang’atuka
Mwenyezi kumbuka na nafsi hii napiga goti natubu

Daima nitakuenzi

Nimeshaikosea jamii nikajiita Mungu mtu nikajiita nabii

Nang'atuka

Mwenyezi kumbuka na nafsi hii napiga goti natubu

Daima nitakuenzi

Muda sasa umewadia ndugu zangu

Watanzania mambo niliyoyafanya hayapaswi kusimuliwa

Tangu nilipoomba kura kwenye ndio mzee

Mkanipa na kusababisha uchumi ulegee

Kura zikawa kula nikaishi kwa milungula

Wimbo "Nang'atuka" wa Profesa Jay, unazungumzia namna alivyokuwa kiongozi na kushindwa kuutendea haki umma kwa kutumia madaraka aliyopewa baada ya kuomba kura kwa ahadi lukuki na kuchaguliwa na wananchi. Matendo yake katika uongozi wake anaamini hayakumpendeza Mungu na hata jamii kwa jumla. Kwani alitenda maovu mengi kwa kutumia cheo, akaamini cheo ni dhamana, akaishi kwa milungula, daima alishiriki kutetea majambazi kwani walimpooza kila walipofanya kazi. Pia, aligawa vyeo kwa hila, aliwapora mali wote waliomzidi kwa utajiri, alisababisha uchumi ulegee, mambo ya muhimu aliyafanya kuwa ya mwisho. Zaidi, akawa muumini mzuri wa mauaji na vitisho, pamoja na mengine mengi kiogozi huyo anamuomba radhi Mungu wake na jamii ili apate kusamehewa na kwa kutambua hayo kiongozi huyo anaachia ngazi kuwapisha wengine ili waweze kuonesha uwezo wao wa uongozi.

Katika wimbo huu msanii amesawiri matendo yanayoweza ambatana na siasa katika mataifa mbalimbali pindi uchaguzi unapofika. Hivyo, msanii anajaribu kuelimisha

viongozi nini wanapaswa kufanya pindi inapotokea kuna udhaifu katika utendaji wao. Kung'atuka au kujiuzulu sio udhaifu kama wanavyoweza kuamini walio wengi. Hii inadhihirisha kujitambua na kuonesha kuwajibika katika jambo lililojitokeza na kuwafanya uliokuwa ukiwaongoza kuwa na imani na utendaji wako. Pia, wanajamii wanapaswa kuwa na uelewa juu ya hatua wanazopaswa kuchukua kwa viongozi wa aina hiyo. Vilevile serikali iangalie katiba ili iwape nafasi wananchi kuchukua maamuzi magumu pindi inapotokea upuuzwaji wa taratibu. Katiba iweke vifungu vya sheria vinavyowaruhusu wananchi kuwashitaki au kuwaondoa kwenye nafasi zao viongozi wazembe katika kuwatumikia wananchi waliowaweka madarakani.

Pia katika wimbo "Trafiki" ulioimbwa na kundi la wagosi wa kaya. Wasanii hawa wanaielimisha jamii jinsi jeshi la polisi kitengo cha usalama barabarani (trafiki) kinavyofikia hatua ya kupindisha sheria za barabarani katika kuwatumikia raia wake na kuwanyanyasa. Katika kuthibitisha hilo wasanii hawa wanatumia mistari ifuatayo hapa chini.

Wimbo: "Trafiki"- Wagosi wa Kaya

Si unajua trafiki ni usalama barabarani

Hatukatai tunawapongeza kwa jinsi mnavyotusaidia

Ila msibishe mnatunyanyasa mnavyotufanyia barabarani

Unajua mnalipaka matope jeshi la polisi

Juzi nilimsikia mtu anasema anapiga *fix*

Hivi nyie mnajua au mnawasikia hawa matrafiki

Ngoja niwaeleze maana mie sipendi unafiki

Wakikamata gari hawapeleki kituoni

Breki ya kwanza kichochoroni

Insuarance wanabandua funguo wanazichukua

Manaake dereva ushuke kwenye gari eti umfuate

Ni rushwa hiyo

Hawawezi kukuachia mpaka umkatie chochote

Wenye magari mtasema mimi nadanganya ndo hivyo wanavyotufanyia

Wasanii hawa wameanza kwa kuwapongeza askari hawa kwa nafasi yao na utendaji wao wa kazi. Ijapokuwa baadaye wasanii wanajaribu kueleza udhaifu wa kitengo hiki katika jeshi, kinapo kuwa katika utendaji wake katika kutimiza wajibu wake wa kila siku. Kauli hiyo ni mafundisho kwa pande zote mbili yaani jeshi kwa upande wa kwanza na raia kwa upande wa pili. Suala la msingi tunalolipata hapa ni kwamba pande zote mbili zinapaswa kuelewa ni lipi jambo halikubaliki kutendeka na trafiki au raia katika jamii.

4.3.2 Kuonya

Jamii inaona kuwa wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa wanatunga na kuimba nyimbo za kuonya watu wanaopenda kupokea rushwa katika jamii yetu. Nyimbo za Bongo Fleva zinakuwa na nafasi kubwa ya kuzungumzia namna ya utoaji wa haki na jinsi haki hiyo inavyoweza kupindishwa na vyombo vyenye mamlaka ya kusimamia haki katika jamii. Moja ya nyimbo za Bongo Fleva zenye mwelekeo huo ni “Mr Policeman” ulioimbwa na msanii Ferooz Mrisho. Wimbo huu unajadili kwa kiasi kikubwa juu ya polisi wanavyo kiuka haki katika utendaji wao wa kazi za kulinda raia na mali zao. Katika wimbo huu, msanii analia na jinsi watuhumiwa wa makosa ya ubakaji wanavyoweza kuachiwa kwa mazingira tatanishi. Katika wimbo huu anasema,

Wimbo: “Mr Policeman”- Ferooz Mrisho

Unathamini wenye mali

Tabaka la chini ukituona *shallow (shallow)*

Ushalo uliopo tayari kujenga Taifa pasipo na shali

Mr police police policeman

Tunakudisi kudisi kitaani

Mr popopo *policeman* tunakudisi kudisi kudisi mtaani

Juzi ulikamata mbakaji

Leo yuko huru

Tuulize mahakama au jaji?

Kwenye mataa yazidi nusu saa

Ajali mbaya imetokea unalewa *bar*

Tunaita mwizi! mwizi! jizi!

Unaukaribisha usingizi

Ulivyonikuta na majani

Ukanipiga pingu kisha ukanisweka ndani

Jamani mimi nilisha puuuna aaah!

Ukanichukulia mapene bila tuhuuuma aaah!

Masela madawa ya kulevya yanakua kila kukicha

Masela wananyeta tena cha ukucha

Uko mbele na sima unakula unataka ushibe eeeh!

Wimbo “Mr Policeman” wa Ferooz Mrisho umetumia maneno kama wenye mali kumaanisha watu matajri, *shallow* ukimaanisha dhaifu, na disi ukimaanisha kumchukia mtu. Mengine ni majani ukimaanisha bangi, puna ukimaanisha shinda bahati nasibu, mapene ukimaanisha fedha. Masela ukimaanisha vijana, masela

wananyeta tena cha ukucha ukimaanisha vijana wanalewa madawa kwa kipimo cha ukucha ambacho msanii anaona ni kidogo, na majemedari ukimaanisha watu wenye nguvu. Kwa hiyo, msanii anazungumzia namna watu wa kitengo cha usalama akiwataja polisi katika utendaji wao wa kazi kuwa wanathamini watu wenye mali na kuwapuuza watu wasio na mali ambao wapo tayari kujenga taifa pasipo vurugu. Pia, anazungumzia uzembe wa polisi katika utendaji wao wa kazi kama kukamata wahalifu na kuwaachilia kwa mazingira tata, kuwaandikia watu kesi kwa lengo la kuhitaji fedha, kuchukua fedha kwa watu au kuwaadhibu watu pasipo tuhuma, kutowajibika kwa wakati pindi wanapoarifiwa matatizo yanayohitaji msaada wao.

Katika wimbo huu tunaona waziwazi kwamba msanii anajaribu kutoa changamoto kwa makundi yanayohusika na ulinzi wa raia na mali zao inapofikia yanakuwa na utendaji mbovu. Msanii anashauri yafanye hima kurekebisha na kuboresha utendaji wa majukumu yao ya kila siku, ili kurejesha imani iliyopotea kwa wananchi waliokosa matumaini na imani kwa vyombo vyao vya dola. Watendaji hawa wanapaswa kuelewa kuwa mabadiliko huanza na mtu binafsi au mtu mmoja mmoja kisha kusambaa kwa jamii nzima. Hatua za makusudi zikichukuliwa na kila mwanajamii tunaweza pata jamii yenye maadili na mwelekeo wenye kuleta mabadiliko ya kiwango kikubwa kinachohitajika katika jamii yetu. Hata hivyo, nadharia ya U-marx ambao ni falsafa yakinifu inayoangalia ulimwengu na vilivyomo kama vitu halisi na kwamba binadamu ndiyo chanzo cha mabadiliko.

Zaidi, katika kuonya jamii, msanii Roma Mkatoliki anajaribu kuionya jamii kwa yale mambo ambayo inakwenda kinyume na vile inatakiwa kama anavyotuambia katika ubeti hapo chini.

Wimbo "2003"- Roma

Msiwaue wachimbaji wadogo Geita inalia

Kaburu mmempa migodi UDSM tuna *Engineer*

Umepewa kontena la kondom muihonge dhahabu

Mv Spice imezama Tv inaonesha taarabu

Kamanga waiweke lami ili tuvuke Busisi

Dereva usinitoe kafara ili kutimiza ahadi ya bosi

Katika sehemu ya wimbo hapo juu msanii anaonya wale waliopewa nafasi ya kuwatumikia wananchi kutenda haki kwa wote na kutotumia nafasi hizo kwa maslahi binafsi. Msanii anaonya kitendo cha wachimbaji wadogo kutopewa haki ya kujishughulisha katika maeneo ya uchimbaji madini kwa uhuru. Wageni kupewa migodi na wazalendo wenye sifa za kufanya hizo kazi kunyimwa pamoja na nchi kutumia gharama kubwa kuwaandaa wataalamu hawa. Nchi kubadilishana mipira ya kondomu na madini ya dhahabu kitendo ambacho msanii anakichukulia kama ni hongo kwani thamani ya vitu hivi viwili hailingani. Vilevile msanii anaonya kitendo cha watu waliopewa dhamana ya kutumikia wengine kushindwa kufanya hivyo. Msanii anazungumzia suala la Televisheni ya Taifa inapoonyesha muziki wa taarabu badala ya kuwaonesha wananchi tukio la meli inayozama kutokana na uzembe wa wale waliopewa nafasi.

4.3.3 Kuadili

Jamii inasema nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinaiadilisha jamii juu ya umuhimu wa kupata elimu ya uraia na sheria. Wakati tulionao unahitaji watu wenye ujuzi wa mambo mbalimbali tokana na kusikiliza nyimbo, kusoma vitabu, makala, majarida, nakadharika. Kwa mfano tukiangalia wimbo wa "Ndiyo Mzee" ulioimbwa

na msanii Joseph Haule maarufu kwa jina la Profesa Jay. Unajaribu kuiadili jamii juu ya kujitambua na kuweza kuelewa haki zao hasa vipindi vya uchaguzi vinapofika kwani wagombea katika kampeni hutoa rushwa, huahidi ahadi za uongo, ahadi zisizotekelezeka. Baada ya kupata nafasi hushindwa kuwajibika kutekeleza ahadi hizo kama anavyoeleza msanii katika mistari ifuatayo:

Wimbo: "Ndiyo Mzee"- Profesa Jay

Ni mambo madogo tu.
Nadhani nitarekebisha
Mkinipa visiku vichache tu uchumi utapanda ile ghafla bin vu
Nataka mpaka Matonya afundishe Chuo Kikuu
Nchi ya Tanzania itang'aa ile kishenzi
Na nitahakikisha kila *bar maid* anamiliki benzi
Wanafunzi mtafanyia *practical* mwezini
Kwenye hospitali nitamwaga dawa kama mchanga
Na nitafungua akaunti kwa kila mtoto mchanga
Mabomba yatatoa maji na maziwa kwa nchi nzima
Watu wa vijijini mtasahau habari ya visima

Wimbo "Ndiyo Mzee" wa Profesa Jay unazungumzia namna viongozi wetu wakati wa kampeni za kuomba kura ili waweze kuchaguliwa katika nyadhifa wanazogombea, hutoa ahadi nyingi na kubwa kutekelezeka na hivyo pindi wakichaguliwa hushindwa kutekeleza. Ahadi hizi hujenga mazingira ya kutoa na kupokea rushwa kwa wahusika yaani wagombea na wapiga kura wao ili waweze kuchaguliwa na kuwachagua katika chaguzi.

Ukiangalia mistari ya wimbo huu utagundua kwamba wagombea wa uongozi hutumia matatizo ya wananchi kama mitaji yao ya kuwapatia nafasi wanazozitaka kwa kuwachagua. Hii hutokea pale wananchi wanapoamini kuwa wagombea wanaweza kuwa suluhu ya matatizo yao pasipokuelewa kuwa wagombea hawana uwezo wa kutatua matatizo yao kama wanavyotamba majukwaani na kinachofanyika ni kutengeneza mazingira ya rushwa. Utafiti unawataka wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi pindi wanapokuwa katika kampeni za kuomba kuchaguliwa wanapaswa kuahidi vitu wanavyojua kuwa wana uwezo navyo katika kuvitekeleza. Vilevile, kuonesha uelewa wao kwa wananchi juu ya mfumo na utendaji wa Serikali katika kuwaletea wananchi huduma za jamii. Mathalani maji, afya, barabara, pembejeo, umeme na vinavyofanana navyo ili kuweza kuahidi vitu vinavyowezekana. Mgawanyo wa huduma za jamii kwa wananchi unategemea kiasi kilichopo na uhitaji wake yaani nani anastahili kupewa kwa wakati huo.

Hata hivyo, katika wimbo “Mikononi mwa Polisi” msanii Joseph Mbilinyi anayejulikana kwa jina la Sugu analiadili jeshi la Polisi kuwatendea haki raia pale wanaposhukiwa kutenda makosa katika jamii. Raia watendewe vitendo vya kiungwana na polisi badala ya kuwanyanyasa kwa kuwapiga, kuwanyang’anya vitu katika mifuko yao, kiwafunga pingu hata wakosaji waliotayari kutii amri ya polisi. Haya yanapatikana katika wimbo ufuatao:

Wimbo “Mikononi mwa Polisi”- Sugu

Polisi ni polisi hata kama ni *Central au police post*

Polisi hakuna dogo kuingia ni bure kutoka kitu kidogo

Hata kama kesi ni ndogo

Msinipige pale mnaponikamata mmenikuta sijakata kuwafuata

Nipelekeni kituoni mbona mnanipeleka uchochoroni

Na sipendi kinisachi mifukoni

Haya nitajieni kosa langu

Mmekuta bangi getoni kwangu?

Nifungeni pingu mikono yangu

Mungu anajua

Sisi hatutaki kuwa na chuki na ninyi

Mimi ni binadamu kama nyie

Nyie ni binadamu kama sisi

Na sisi tunakosea kama nyie

Siku ikifika mtakufa kama sisi kitu cha maana kwenye maisha ni raha

Kama raha inakwisha basi hata shida itakwisha

Utafika wakati pingu tutaona bangili

Afande ataniita nitaona shida kusimama

Polisi ni mahali salama sasa mbona sio salama mnatangaza kiama

Katika wimbo huu tunaona msanii anavyoelezea sifa za jeshi letu la Polisi kwa raia pindi wanaposadikika kutenda makosa. Polisi hutumia nafasi hizo kuwakamata na kuwaomba rushwa kwenye mazingira ya kificho. Hata hivyo, kuwafanyia vitendo vya kinyama raia wenzao kama kuwachapa, kuwafunga pingu, kuwapekua kwenye mifuko na kuchukua vilivyomo. Pia, kuwataka raia kutoa chochote ili waachiwe huru pale wanapotuhumiwa na kuwekwa mahabusu. Hivyo, kutokana na haya jeshi la polisi halina budi kuchukua hatua za makusudi katika kuhakikisha linafanya mapinduzi ya kweli katika utendaji wa majukumu yake ya kila siku. Kwa sababu, U-

marx unaamini kuwa mbinu kubwa ya mabadiliko ni kuchunguza jadi na kuunda upya mtazamo kuhusu yaliyopita kutokana na ithibati za kihistoria, kisha kidhihirisha uhalisia wa kazi fulani kama kielelezo cha jamii kwa njia ya kuelewa uhalisia. Hivyo, jamii inapaswa kutumia nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kama kielelezo cha mabadiliko. Hii itasaidia kujijengea sifa ya kuaminiwa na raia wake na hata kupendwa badala ya kuchukiwa kama asemavyo msanii.

4.3.4 Kukemea

Jamii inaona kuwa watunzi na waimbaji wa nyimbo za Bongo Fleva wameguswa kwa kiasi kikubwa kuhusu tatizo hili, na hawako nyuma katika kukemea rushwa. Hivyo mara kwa mara wamekua wakitunga na kuimba kuhusu madhara ya adui rushwa. Wasanii wanakemea na kutoa changamoto kuhusu mustakabali wa Taifa la kesho litakalo kuwa limejengeka kwa misingi ya rushwa. Katika wimbo “Rushwa” ambao umeimbwa na Mapacha. Wasanii hawa wanasisitiza kuwa rushwa ni adui wa haki hivyo kama jamii inataka haki ni lazima kutokomeza rushwa kwanza, kama wanavyosema katika ubeti huu.

Wimbo: “Rushwa”- Mapacha

Hii vita ni ngumu sababu wanaotoa rushwa ni wale wenye mabavu
Wanaolimbikiza mali kama vile makaburu
Masikini wanabakia wanaugulia maumivu
Taifa la kesho sijui litarithi nini
Kama vyote vizuri wanataka wavimiliki
Mikataba wanayosaini nayo haiwekwi wazi
Wanaendelea kuficha mchezo wa kamari
Wananchi hawaelezwi, *which is very bad*

Wanaendelea kutoa wengine wanapokea

Hakuna cha kungojea matajiri wanajizolea

Kisa wanayo pesa

Toka mdogo nasikia jina rushwa

Kuwa ni adui wa haki na hakuna wa kumgusa

Mbona hamchukui hatua inayoendelea kukua

Asante TAMWA kwa kutupa nafasi ya kuweka wazi

Huyu adui wa haki rushwa adui wa haki

Huyu rushwa adui wa haki, hatumtaki

Wimbo “Rushwa” wa Mapacha unazungumzia ugumu uliopo katika suala la kutokomeza rushwa. Utabaka unaozungumzwa na nadharia ya U-marx unajidhihirisha hata katika rushwa kama wimbo unavyoeleza. Ugumu unatokana na kuwa wanaotoa rushwa ni watu wenye nafasi kiuchumi na kiutawala, wanaojilimbikizia mali, vizuri vyote wanamiliki wao. Mikataba wanayoisaini hawaiweki wazi kwa walio wengi, watu hawa hawaogopi kutoa rushwa kwa sababu fedha wanayo na hakuna wakuwagusa. Wakati hayo yote yanatendeka masikini wanaendelea kuumia. Lakini wasanii wanalaumu kwa wahusika kutochukua hatua huku rushwa ikiendelea kukua. Pia, wimbo unawashukuru wale wote wanaounga mkono mapambano dhidi ya adui rushwa kama vile TAMWA.

Wasanii hawa wanaelezea masuala mbalimbali ambayo utendaji wake unaashiria rushwa, kama vile kusaini mikataba ya kitaifa bila ya kushirikisha wananchi, wenye nacho wanazidi kujilimbikizia mali, wananchi kutoelezwa mambo yanayowahusu katika nchi yao. Pamoja na kuonesha athari za rushwa, wasanii wa Bongo Fleva wanaonekana kuzipongeza taasisi na makundi ya kijamii yanayounga mkono vita

dhidi ya adui rushwa kama vile chama cha wanahabari wanawake Tanzania (TAMWA). Hata hivyo, kama jamii hatuna budi kuelewa kama suala la kupambana na rushwa sio la watu wachache bali linaihusu jamii yote; na kwamba, kila mwanajamii anawajibu wa kushiriki katika kuitokomeza rushwa.

Utafiti umebaini pia dhima ya kukemea rushwa iliyotapakaa katika jamii ambayo inatokana na watu wachache kupenda kujinufaisha binafsi kutokana na nafasi walizopewa baada ya kuaminiwa na jamii au wale waliowateua kutokana na nafasi zao kijamii. Hilo linaonekana katika ubeti wa wimbo Tanzania wa msanii Roma Mkatoliki kama anavyosema.

Wimbo "Tanzania"- Roma

Ukabila na rushwa maofisini ndio swadakta
Alikuwa Dkt wa mifugo leo waziri wa soka
Amenunua vyeti kwa kupata stashahada
Na elimu za kuunga unga na Digrii za kikuda
Taaluma isiyo na future kwa tuliosoma sayansi
Maghorofa yanayodondoka kwa kufoji kandarasi
Namwaga chozi kwa hela ya mama ntilie
Mumy don't cry Dad futa machozi usilie (naam)
Real so kind nakuona umepanda mori kama morani wa kimasai

Katika wimbo huu tunaona msanii anavyoeleza suala la ukabila na rushwa lilivyotawala katika ofisi nyingi katika nchi yetu, kwamba walioshikilia nafasi kwenye maofisi wengi wao wamepata nafasi kwa kujuana au kwa kutoa rushwa. Wengine kupewa nafasi za kuongoza vitengo ambavyo si vya taaluma zao na hii ndiyo sababu ya ufanisi hafifu wa vitengo hivyo kama vile kuanguka kwa maghorofa

kutokana na kughushi kandarasi. Kwa maana hiyo, ni muhimu kufanya kazi kwa kuzingatia uwezo na taaluma za watendaji wetu kwa mafanikio ya taifa letu.

4.3.5 Kuarifu

Pia, jamii inaiona kazi kubwa ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii kuwa ni kuarifu serikali na jamii kwa ujumla, watu mbalimbali wanavyoonesha utendaji wao mbovu katika maeneo yao ya kazi na hii inaonesha wazi kuwepo na kukithiri kwa vitendo vya rushwa katika jamii. Kwa mfano, matukio ya kusaini mikataba hewa na kuachiwa huru kwa watuhumiwa wa makosa mbalimbali katika mazingira tatanishi tunaweza kuyaona katika wimbo wa “Mr Policeman” ulioimbwa na msanii Ferooz Mrisho, katika mistari ifutayo,

Wimbo: “Mr Policeman”- Ferooz Mrisho

Juzi ulikamata mbakaji

Leo yuko huru

Tuiulize mahakama au jaji?

Kwenye mataa yazidi nusu saa

Ajali mbaya imetokea unalewa *bar*

Tunaita mwizi! mwizi! jizi!

Unaukaribisha usingizi

Ulivyo nikuta na majani

Ukanipiga pingu kisha ukanisweka ndani

Jamani mimi nilisha puuuna aaah!

Ukanichukulia mapene bila tuhuuuma aaah!

Masela madawa ya kulevya yanakua kila kukicha

Masela wananyeta tena cha ukucha

Wimbo “Mr Policeman” wa Ferooz Mrisho katika kuarifu umezungumzia mambo yanayotendwa na watumishi wa serikali kwa kutowajibika ipasavyo. Kwa mfano, polisi wanapokamata mhalifu hata hajafikishwa mahakamani unamkuta yupo huru. Ajali mbalimbali zinatokea au wahalifu wanapokuwa wamekamatwa na raia wema na kwa kuwa ushahidi wa kipolisi unahitajika basi, kuchelewa kufika kwa polisi katika maeneo yanakotokea matukio ni kusababisha matatizo kwa wahanga. Vilevile, unazungumzia kuhusu watendaji wa serikali hao kuchukua mali za watu wasio na tuhuma, kuwapiga watu wakati hakuna uthibitisho wa makosa yao. Pia, watendaji hao kujishughulisha na matendo ya uhalifu kama kutamani wake za watu na kushiriki katika uporaji wa mali za watu badala ya kuwalinda watu na mali zao.

Katika sehemu ya wimbo hapo juu tunaona jinsi watendaji wetu wanavyojenga mazingira ya kutoa na kupokea rushwa. Kuachiwa kwa wahalifu, kukawia kwenda katika eneo la tukio pindi wanapoarifiwa tatizo, kuchukua fedha kutoka kwa raia kwa njia zisizo halali. Hayo yote yanaashiria uwepo wa mazingira ya rushwa katika maeneo ya kazi na hili msanii anaamua kuiarifu serikali na umma kwa ujumla na kuwataka pia wahusika wa mambo haya kuchukua hatua za makusudi katika kuleta mabadiliko kwa jamii.

Utafiti umebaini pia dhima ya kuarifu katika wimbo wa “Tanzania” ulioimbwa na msanii Ibrahim Mussa anayejulikana kwa jina la Roma Mkatoliki. Msanii anajaribu kuarifu jamii suala la rushwa namna lilivyosambaa na hata kupiga hodi katika nyumba za ibada. Katika nyumba hizi suala hili limeathiri hata utukufu wa mahekalu yaliyo mengi na wote waliomo ndani yake, akijadili hilo msanii katika sehemu ya wimbo huu anasema.

Wimbo "Tanzania"- Roma

Nakuabudu miungu watu ili mradi wapate pesa mbele ya madhabahu

Rwakatare, Askofu Kakobe wanadondoka mbele ya Altare

Wameshatoa ushuhuda wa uongo

Imekuwa biashara waumini wamepewa hongo

Wanaandika *proposal* za uongo wapate zali

Huu ni ufisadi wana*pretend* ujasiria mali

Ona polisi wanakuwa matajiri

Vigogo wanatoa namba za simu wapewe rushwa

Stil wanaanzisha vitengo vya kulea wagonjwa wa UKIMWI

na wito hawana

Wanaanzisha wapate faida kiuchumi

My God what's wrong?

Katika wimbo hapo juu msanii anajaribu kueleza namna rushwa ilivyosamba mpaka makanisani ambako waumini hupewa hongo na wenye makanisa au viongozi wa makanisa hayo ili waweze kutoa ushuhuda wa uongo ili kuwaaminisha waumini uwezo wa kimungu walionao wachungaji katika kuwaombea waumini wao. Pia wachungaji kuwaabudu waumini wenye nafasi nzuri kiuchumi ili waweze kuyachangia makanisa yao, kifupi makanisa yamekuwa mitaji kwa wachache hao. Polisi wanakuwa matajiri kutokana na kujipatia fedha kwa njia isiyo halali kutoka kwa raia wema. Viongozi wanatoa namba za simu wapewe rushwa kupitia mifumo ya kimtandao inayotumika katika kusafirisha fedha kama vile M- pesa, Tigo pesa na Airtel money. Wengine wanatumia njia za maandishi ili kujipatia fedha ambazo hatimaye huonekana ni njia haramu za kujipatia pesa kwa mfano kuandikia miradi ya

kulea watoto yatima, kulea wagonjwa ya UKIMWI. Hayo yoye yanafanyika na watu ambao hawana wito wa kuyafanya mambo hayo.

4.3.6 Kuburudisha

Jamii inaamini kuwa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa katika jamii pamoja na kuwa na dhima nyingi kama vile kuelimisha, kutia hamasa, kuarifu, kukemea, kuadili, kupitisha thamani za jamii na kutumika kama rekodi ya matukio muhimu ya kihistoria pia huburudisha jamii. Wakati mwingine nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa huimbwa kwa hisia za uchungu, msikilizaji hupata ujumbe uliomo katika nyimbo hizo pia huburudisha nafsi. Tukiangalia wimbo unaojulikana kwa jina la "2030" wa msanii Ibrahim Mussa anayejulikana kwa jina la Roma Mkatoliki, katika kiitikio cha wimbo huo, kuna ujumbe vilevile burudani kama inavyosikika hapa chini.

Wimbo: "2030"- Roma

Tanzania eeeh!
Mwanangu kua uyaone Rais acha kisirani gonga muhuri tuwahi
Nchi yangu eeeh!
Mwanangu kua uyaone rafiki hasira za mkeo hazifai barabarani
(hazifaii…)
Tanzania eeeh!
Mwanangu kua uyaone wanahonga mashabiki ngoma zao wazi-*request*
Nchi yangu eeeh!

Katika kiitikio cha wimbo wa hapo juu tunaona msanii anavyojaribu kutoa masikitiko yake kwa wasanii wenzake wanaotoa rushwa kwa wasikilizaji ili waweze kuomba nyimbo zao zichezwe katika vipindi vya radio na televisheni mbalimbali.

Pia, msanii anawaasa watu kuwa na busara katika maeneo yao ya kufanyia kazi na kuachana na hasira zinazotokana na matatizo binafsi na zaidi watende haki kwa kuwasaidia wale wote wanaowatumikia pasipo na ubaguzi wa aina yeyote unaojali kabila, rangi, jinsi, wala ukanda. Vilevile wale walio pewa nafasi za kuwatumikia wananchi kutokuwa na urasimu katika utendaji wao wa kazi.

4.3.7 Kutia hamasa

Jamii inakubaliana na mchango wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa na wasanii mbalimbali nchini. Nyimbo hizi zinawatia hamasa watunzi na waimbaji wa nyimbo kujituma katika utunzi na uimbaji wa nyimbo na kutojihusisha na utoaji wa hongo kwa watu wanaohusika na promosheni ya nyimbo hizo na badala yake juhudi na maarifa vitumike kukonga nyoyo za mashabiki, kuendana na soko la muziki, pia kumudu ushindani katika uwanda wa muziki.

Katika wimbo uitwao “mtazamo” ulioimbwa na msanii Msafiri Kondo maarufu kama Solo Thang akiwashirikisha Joseph Haule (Profesa Jay) na Seleman Msindi (Afande Sele) wanatoa hamasa katika mistari ifuatayo.

Wimbo: “Mtazamo”- Solo Thang ft Profesa Jay, Afande Sele

Natamani kuwa huru mnyonyaji asinidhuru
Wanaitwa maMC hawajui mitindo huru
Huu mtazamo wangu naona vingi vioja
Yaani watangazaji sasa ndio mameneja
Vidato sita nilivyopitia ndivyo vinavyonisaidia
Mbunifu ukizingatia hata wakinibania ni kipaji tu ni mtazamo tu.
Yes!

Ma-*underground* wanafanya *rap* inang'ara

Lazima muwe vinara imara kwenye msafara

Rap na mazingaombwe *all time* haviendani

Msitegemee hailee iwaokoe kwenye fani

Ni vema ukafikiri kabla ya kufanya maamuzi

Tazama mbele usije ukanywa chai kwa mluzi

Kabla hujaingia kwenye fani lazima upite depo

Vinginevyo ndugu yangu utakuwa unapaka rangi kwenye upepo

Kama unapata moja kwanini usipate na mia

Hiyo inawezekana kwa wote walio na nia

Kwanini msipate sioni sababu za msingi kuomba kwenye hadhara

Kama unakipaji iweje ufe na njaa?

Wimbo "Mtazamo" wa Solo Thang akishirikiana na Profesa Jay na Afande Sele umetumia maneno kama ma- *udergrround* ukimaanisha chipukizi, mazingaombwe unamaanisha uchawi, *hailee* unamaanisha bangi, *depo* unamaanisha chuo cha sanaa. Wimbo unazungumzia namna wasanii wanavyoweza kuwa huru katika fani yao, kutokana na maMC kutokuwa na taaluma ya sanaa, watangazaji kuwa mameneja hivyo kufanya kazi kwa upendeleo. Hivyo, msanii anawatia hamasa wasanii wenzake kuwa vitu muhimu ni taaluma, kipaji, ubunifu, nia, jitihadi na maamuzi sahihi vinatosha kumfanya msanii kung'aa kwenye fani, msanii anawaasa chipukizi kujituma katika fani na kutotegemea mazingaombwe pia hailee (bangi) iwainue kwenye sanaa.

Katika mistari ya hapo juu tunaona jinsi wasanii hao wanavyojaribu kutoa hamasa kwa wasanii wenzao kuepukana na rushwa kwa kutumia vipaji vyao ikiwa ni pamoja

na kujituma, kutumia vipaji walivyonavyo, kuiheshimu hiyo fani na kuichukulia kama ndio ajira yao. Kwa kufanya hivyo wataweza kukimu mahitaji yao ya msingi na ya jamii kwa ujumla kupitia nyimbo za Bongo Fleva.

Naye msanii Emmanuel Bryson anayejulikana kisanii kama Izzo B, katika wimbo wake unaoenda kwa jina la "Ridhiwani" anawahamasisha wasanii na jamii kwa jumla kutambua haki zao. Hii itawasaidia kupambana ili wasiibiwe na wale waliopewa nafasi za kuwatumikia. Hii inaweza kudhihirishwa na dondoo la wimbo hapa chini:

Wimbo "Ridhiwani"- Izzo B

Nizungumzie haki zetu muziki tunaibiwa
Bungeni atuwekee watu tumechoka kuibiwa
Wazee wanalalamika hawajalipwa mafao yao
Kazi kweli walichapa sasa nani afute machozi yao
Wabunge hawakai majimboni mjini wamehamia
Kama kampeni afanye mapema kuwashitua
Ugonjwa usio na tiba tupeleke Loliondo
Wanasaini tu mikataba mahakamani

Katika wimbo huo msanii anadokeza mambo mengi yanayoashiria makundi mbalimbali ya jamii yasivyotendewa haki na wachache wenye dhamana. Kama vile, wasanii kuibiwa kazi zao, Bungeni kuwepo wabunge wanaojitambua na kuwajibika ipisavyo, mafao ya wastaafu yalipwe. Mengine wabunge wakae majimboni ili kujua matatizo ya wananchi na tendo la kusaini mikataba lifuate taratibu. Msanii anawataka jamii kutambua kuwa hawatendewi haki na wale waliowapa nafasi ya

kuwatumikia. Kwa maana hii anawahamasisha kuchukua hatua stahiki pindi wapatapo nafasi mfano katika kufanya chaguzi wachague wenye sifa na kuachana na rushwa.

4.3.8 Kupitisha Thamani za Jamii

Jamii inakubaliana na wazo la kuwa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii zina dhima ya kupitisha thamani za jamii. Nyimbo huimbwa kwa lengo la kuelimisha, kuburudisha, kutia hamasa katika mambo mbalimbali, kutokana na hayo tunaweza kuona kuwa vizazi vipya vinarithi mambo hayo kutoka vizazi vilivyotangulia na kwamba nyimbo za Bongo Fleva ni kitambulisho cha jamii ya watanzania. Katika wimbo “Hapo zamani” ulioimbwa na msanii Joseph Mbilinyi anayejulikana kama Sugu ni mfano mzuri wa nyimbo zinazotumika kupitisha thamani za jamii ambapo vizazi vya kileo hupata kujifunza mambo yaliyopita kupitia nyimbo na sanaa nyingine kadha wa kadha.

Wimbo “Hapo zamani”- Sugu

Hapo zamani hapo zamani
Mambo mengi yalikuwa safi
Hapo zamani hapo zamani
Mambo mengi yalikuwa shwari
Kinyume na sasa kinyume na sasa
Mambo mengi yamebadilika
Kinyume na sasa kinyume na sasa
Mambo mengi yameharibika
Hapo zamani nikikumbuka najiona nipo ndotoni
Nayapenda maisha yangu ya utotoni

Mama yuko jikoni

Nimetoka shuleni nasikiliza tu muziki redioni

Sikumbuki kama tulikuwa na feni

Sasa ni miaka mingi yamepita mambo mengi

Na bado nakumbuka sana pamba za dingi

Alikuwa na afro ana suti inambana chini buga na raizoni

Mama alivaa gauni anavyokwenda kanisani

Sina maana muache kuvaa vimini

Wimbo huo unajadili mambo mbalimbali ya zamani ukiyatofautisha ya sasa ambayo yanaenda kinyume na utamaduni wa Mtanzania. Msanii anasema mambo ya sasa yameharibika, yamebadilika wakati ya mambo ya zamani yalikuwa shwari, yalikuwa safi kinyume na sasa. Msanii anajaribu kueleza mavazi waliyokuwa wakiyavaa wazazi wake kwamba baba yake alikuwa akivalia suti ya kubana chini buga, kiatu aina ya raizoni na alikuwa na afro na kwa upande wa mama alikuwa akivaa gauni refu lenye sifa hata akalisifia kuwa lilifaa kanisani hiyo yote ni mitindo ya zamani ya uvaaji ambayo vijana wameirithi na kuifanya mitindo ya kileo.

4.3.9 Ukombozi

Utafiti umebaini mchango wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya Jamii. Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zina mchango wa kuikomboa jamii kifikra ili iweze kijitambua na kuweza kutoa maamuzi yenye hekima na busara na ambayo hayataweza kuifanya jamii kujutia maamuzi yake. Katika kipindi tulicho nacho na hasa kuelekea kwenye chaguzi mbalimbali ambazo wagombea hutumia nafasi hizo kuomba nafasi za kuwatumikia wananchi kwa ahadi lukuki. Ahadi hizo mara nyingi huwa ni zile zisizotekelezeka, za uongo na wakati

mwingine ahadi hewa. Wakati mwingine wagombea wa uongozi huo hutoa rushwa za vitu mbalimbali kama vile kanga, kofia, mashati, chakula n.k hivyo vyote huwa ni katika kushawishi wananchi ili kuwapatia nafasi za kuongoza. Msanii anayejulikana kwa jina la Bonta kwa kulijua hilo anaimba wimbo anaouita "Kura yangu" katika wimbo huu msanii anajaribu kuikomboa jamii kupitia wimbo huu kwamba ni muhimu kufikiri kabla ya kutenda. Mistari ifuatayo hapa chini inathibitisha hili:

Wimbo: "Kura yangu"- Bonta

Hospitali iwe mlangoni

Sitaki kurudia leo

Nasimama tena strong kama Cheyo

Shangazi wa Bongo alifariki kwa kuzalia nyumbani

Zahanati iko mbali baiskeli ilikuwa mbovu

Siwezi ondoa hilo kovu kwa moyo wa masikini

Kama mimi mwenye kovu la wovu

Kwa kweli migomo haiwezi kuisha kama shirika la reli

We have to look a people beyond a colour

Beyond a religion beyond a tribe

Just see the true nature,

Sitaki tena pilau wala vipande vya kanga

Sitaki tena sabuni wala kofia ya yanga

Nataka kuuza kura yangu thamani ya *diamond*

Awe tayari kuinunua

I can't let my gold go to

Sababu wataniua kama Malima wa Kigoma

Wataichukua hakika haitarudi kama kwa Kolimba ilivyokuwa

Wimbo “Kura yangu” wa Bonta unazungumzia juu ya thamani ya kura kwamba unatakiwa kufikiri juu ya thamani ya kura kwa maisha yako na watu wengine. Msanii katika wimbo wake anazungumzia umuhimu wa kumchagua mtu atakayeweza kuwasaidia watu wake kwa kuwaletea maendeleo kama vile kutengeneza mazingira rafiki kwa binadamu yenye huduma za msingi mathalani, huduma za afya, elimu, usafiri, maji, na barabara. Msanii anatuonesha anavyojutia uamuzi wake mbaya katika kumchagua kiongozi aliyewarubuni kwa kuwapa pilau, vipande vya kanga, sabuni, na kofia. Kwani, kwa kufanya hivyo inasababisha vifo kutokana na huduma za afya kuwa mbali na usafuri kutokuwepo. Sasa anataka kuiuza kura yake kwa thamani ya shaba ili kumpata kiongozi atakayejenga mazingira rafiki kwa maisha ya watu wake anaowatumikia na zaidi anashauri kumchagua mtu kwa kuangalia uwezo wake wa utendaji na sio kuangalia rangi, kabila, dini, ukanda.

Katika wimbo huu, msanii anajaribu kuifanya jamii itambue thamani ya kura kwa kila mwenye umri wa kupiga kura na kuweza kuitumia vizuri nafasi hiyo. Anajaribu kuwafanya wanajamii kufananisha thamani ya kura na pilau, kanga, kofia, vipande vya sabuni, na vifananavyo. Kura kwake yeye ina thamani ya *diamond* ambayo ni madini yenye thamani kubwa. Anawataka jamii kutafakari namna ya kuitumia kura katika kupata huduma muhimu kwa binadamu, kwa mfano uwepo wa zahanati, maji safi, elimu, ajira, usafiri, na pembejeo. Hivyo vyote vitapatikana kwa kuitumia kura vizuri kwanza kwa kushiriki katika chaguzi mbalimbali; pili, kuchagua kiongozi bora atakaye wajibika kwa maslahi ya jamii na sio kwa maslahi binafsi; tatu, awe jasiri na anayejua wajibu wake katika kuwatumikia jamii.

Vilevile, utafiti umebaini dhima ya ukombozi katika wimbo “Mtazamo” ulioimbwa na msanii Solo Thang akiwashirikisha Profesa Jay na Afande Sele. Wasanii hawa

wamejadili suala la ukombozi kwa jamii kwamba binadamu anatakiwa kujikomboa kifikra, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ili kujitambua na kuweza kujua haki yake katika kila analolifanya wakati wote wa uhai wake. Hayo yamebainishwa na maneno yaliyomo katika sehemu ya wimbo hapa chini.

Wimbo "Mtazamo"- Solo Thang ft Prof. Jay, Afande

Unakuwa mtumwa ili upewe promo kuuza
Au kama ni binti ukalale kwa ma*produzer*
Mapromota wanauma so hawajui na kupuliza
Na siku wakipuliza ujue kidonda kishaoza
Natamani kuwa huru mnyonyaji asinidhuru
Wanaitwa maMC hawajui mitindo huru
Huu mtazamo wangu naona vingi vioja
Yaani watangazaji sasa ndio mameneja
Vidato sita nilivyopitia ndivyo vinavyonisaidia
Mbunifu ukizingatia hata wakinibania ni kipaji tu ni mtazamo tu
Msikasilike washikaji haya ni mawazo

Katika wimbo hapo juu tunaona wasanii wanaeleza jinsi rushwa ilivyotapakaa katika kazi za sanaa, kuwa msanii unatakiwa kuwa mtumwa ili upewe nafasi ya kuitangaza kazi yako ya kisanaa na kama msanii ni wa kike basi atatakiwa kulala na maproduzer ili apate nafasi hiyo. Pia watangazaji nao wamekuwa mameneja kwani kwa nafasi zao za kucheza nyimbo mbalimbali katika vyombo vya habari ili kuzitangaza nyimbo hizo, kuburudisha jamii na pia kufunza jamii basi nao huchagua nyimbo za wasanii wanaowapenda au waliotoa kitu kidogo na kuzicheza huku wakiziacha kazi za wasanii wengine. Wasanii hawa wanawataka wasanii wenzao na jamii kwa jumla

kutumia vipaji, maarifa, na taaluma zao kuhakikisha wanafanya kazi za uhakika ambazo zinamvuto wa kuhakikisha zinamvutia kila mtu na kufanya watu wazipende na kuzicheza pasi na kutoa chochote mahali popote.

4.3.10 Kudhihaki Uoga

Jamii inasisitiza suala la wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kuwa kazi yao ni kubwa katika jamii pamoja na nyingine nyingi, pia suala la kudhihaki uoga kwa kuwajengea ujasiri wanajamii ni muhimu na linapaswa kupewa kipaumbele. Suala la kudai haki ambalo linatafsiriwa na watu mbalimbali kama uchochezi, fujo na mengine yanayofanana nayo. Hili linatakiwa kuelezwa na wasanii pale wanapopaza sauti zao kupitia nyimbo na kuwafanya wanajamii kutambua haki zao, kujitambua wao binafsi na kuelewa ni wakati gani wanakosea na wakati gani wanakuwa sahihi. Kwa kuwa nyimbo hupendwa na husikilizwa na watu wa rika mbalimbali, basi wazo hilo litawafikia wengi na kufanya wengi wao kupata hisia mpya. Msanii Ibrahim Mussa anayejulikana kwa jina la Roma Mkatoliki katika wimbo wake “2030”, anadhihaki uoga walionao wanajamii kama tunavyoweza kuona katika mistari hapa chini.

Wimbo: “2030”- Roma Mkatoliki

Watanzania tuna uoga sio amani tunadanganywa
Amka kifikra damu yako iwe chachu ya ukombozi kama Dkt Ulimboka
Mkinga usimuue mama ili uongeze kipato
Utajiri upo kaburini watu wamekufa na ndoto
Leo Ridhiwan hafanani na Makongoro
Dah sina hela ya kiroba Rashid nigongee ugoro
Suka akaiangusha roli ya mafuta yote magendo

Waziri anauza pembe za ndovu na meno ya tembo

Nchi imejaa misitu uhaba wa madawati

Tunakula vitu feki wa-*TBS* mko wapi?

RPC usitume kikosi ili uishushe CHADEMA

Mahali ilipo damu ya Mwangosi Iringa kasemeni amina

Okoa saratani mipakani zuia wakimbizi

Kuliko kumwaga pesa kwenye tume za uchunguzi

Muhimbili naumwa goti eti Dkt kanipasua kichwa

Mbeya wanapigwa nyundo ili raia wauze mabucha

Amana wanawatelekeza watoto wanalia

Mwananyamala wanatuua na hawaendi jela

Jela anakwenda Kajala

Wimbo “2030” wa Roma Mkatoliki unazungumzia uoga tulionao Watanzania na kuaminishwa kuwa tuna amani. Msanii anatuasa kujituma katika kazi na sio kuamini njia za mkato ili kuinua vipato vyetu kama vile kuroga ndugu ili kupata utajiri, kupiga nondo watu ili uuze nyama mabuchani. Hata, madereva kuangusha magari (roli) baada ya kuuza mizigo iliyokuwemo ndani ya gari. Pia, msanii anazungumzia watu kuwa wazalendo na nchi yao kwa mfano watendaji wa serikali kutoruhusu vitendo visivyokubalika katika nchi mfano watu wanaohusika na udhibiti wa chakula kutoruhusu chakula kisicho cha kiwango kuliwa na binadamu kutokana na kuwepo kwa rushwa. Viongozi wa nchi kujihusisa na biashara ya pembe za ndovu, nchi kuwa na uhaba wa bidhaa fulani wakati malighafi inazo na kuchukuliwa na wageni. Pia msanii anazungumzia pia suala la watu wenye dhamana kutoa maamuzi ya mabavu kwa walio chini yao ili kuzuia haki za vikundi fulani au watu fulani kwa masilahi

binafsi. Vilevile, anasisitiza haki itendeke kwa kila binadamu kutokana na kosa alilolitenda bila kujali alichonacho.

Katika wimbo huu, msanii anaweka wazi tabia za uoga tulizonazo Watanzania na kuaminishwa kuwa tunaamani, msanii anatutaka kuamka kifikra na kuwa chachu ya ukombozi kwa binadamu. Msanii anatutaka kujituma katika kazi na kuachana na njia za mkato za kuinua vipato vyetu. Kuwa wazalendo kwa kushiriki katika kuzilinda rasilimali za nchi na wananchi kwa kuweka wazi wale wote wanaojishughulisha na ubadhirifu wa mali za umma iwe kwa kutumia vyeo vyao au kwa kutumia njia za mkato. Vilevile msanii anazungumzia suala la kuchukua tahadhari kabla ya kutokea kwa matatizo na umakini katika utendaji wa majukumu yetu ya kila siku. Kwa mfano, anazungumzia suala la kuzuia saratani, kuzuia wakimbizi mipakani, madaktari kutoa tiba tofauti na matatizo waliyonayo wagonjwa, mahakama kutotoa haki sawa kwa raia kwa kuangalia nafasi na vipato vyao. Hatimaye huishia kuunda tume za uchunguzi zinazotumia fedha nyingi suala lisilo la lazima, hivyo suala la msingi ni watendaji kuwa makini na kutimiza wajibu wao ipasavyo na inawezekana.

Dhima ya kudhihaki uoga imejitokeza pia katika wimbo “trafiki” ulioimbwa na kundi la Wagosi wa Kaya. Katika wimbo huu, wasanii wanajaribu kuelezea jinsi mambo yanavyoenda barabarani kitu ambacho ni ukiukwaji wa taratibu na sheria za barabarani na hili linafanywa na jeshi la polisi kitengo cha usalama barabarani. Katika kuonyesha haya, wasanii wanasema:

Wimbo "Traffic"- Wagosi wa Kaya

Ni wengi sana wenye magari wasio wapenda matrafiki

Wachache wanabakia kutaka urafiki wakipita hawakamatwi

Mkono tu wanawapungia wako radhi kusumbuka leseni kuwatafutia

Mnaleta sana usumbufu mabasi ya mikoani

Mabasi mengine hamkamati kwanini?

Elezeni kama mabasi ni ya mkubwa fulani

Waswahili wanasema mficha kidonda hapati dawa

Hapa hatugombani ila tunawekana sawa

Tunapiga sana kelele juu ya hii Rushwa

Vishilingi 2000 vitakupeleka wapi?

Unachezea bure kibarua kiote nyasi

Kazi ya *traffic* haiendani kabisa na urafiki

Sheria njiani tumeweka je si itakuwa ni unafiki

Katika sehemu ya wimbo hapo juu wasanii wanadhihaki uoga walio nao polisi wa usalama barabarani pale inapofikia wakati mwingine kushindwa kukamata baadhi ya magari yenye matatizo na yanatembea barabarani, kwasababu labda ni ya mkubwa fulani, ndugu au rafiki na wakati mwingine kwa sababu ya pesa waliyo nayo wenye magari hayo.

Wasanii wanadhihaki uoga huo na kuwataka polisi hao kufuata taratibu na sheria za barabarani kwa kuwa zipo na kufanya kinyume chake itakuwa haina maana ya kuweka alama, sheria na kanuni za barabarani. Zaidi wasanii wanashauri polisi hao kuacha kuchezea kazi kwa kuchukua rushwa tena za shilingi elfu mbili tu ambazo ni ndogo ukilinganisha na thamani ya kazi zao wanazozifanya.

4.3.11 Kutumika kama rekodi ya matukio muhimu ya kihistoria

Utafiti umebaini kuwa nyimbo za Bongo Fleva zinatumika kuelezea matukio ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii yaliyotokea katika vipindi tofautitofauti na kuifanya jamii kukumbuka mambo mbalimbali yaliyokwisha kutokea nyakati zilizopita kwa kusikiliza nyimbo hizi. Wimbo “Mikononi mwa Polisi” ulioimbwa na msanii Joseph Mbilinyi anayejulikana kama Sugu unasawiri kipengele hiki kwani unatukumbusha tukio lililotokea miaka kadhaa huko nyuma na kutufanya kukumbuka na hata kizazi cha baadaye kujua kutokea kwa jambo hili. Sehemu ya mistari ya wimbo iliyodondolewa hapo chini inathibitisha hili; inasema:

Wimbo Mikononi mwa Polisi- Sugu

Nyimbo hii ni kwa marehemu Michael Sikupya
Mwanafunzi wa Iyunga Mbeya aliyeuawa mikononi mwa polisi
Sio yeye tu wengi wanakufa kimakosa mikononi mwa polisi
Wengi wanajeruhiwa nani wa kulaumiwa
Mikononi mwa polisi
Niko mikononi mwa polisi
Maisha yangu bado ni mikosi
Niko ndani nimechoka
Polisi wamenipiga damu inatoka mwili mzima

Wimbo huu uliimbwa mwaka 2000-2001 unazungumzia hali halisi ya namna jeshi letu la polisi linavyofanya kazi katika kuwalinda raia na mali zao kama jukumu hili linavyowataka ikiwa ni utaratibu na sheria za kazi yao. Lakini polisi wetu kuna wakati hukiuka taratibu na sheria za kazi zao ambapo hufikia wakati hutumia nguvu katika kutatua matatizo yanapotokea kwa baadhi ya raia kwa mfano kunapotokea

migomo kama vile mashuleni na vyuoni, maandamano ya mikusanyiko ya watu kuyataja kwa uchache. Wimbo huo unatukumbusha kifo cha mwanafunzi aliyejulikana kama Michael Sikupya aliyekuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Iyunga ya Mkoani Mbeya aliyeuawa mikononi mwa polisi mwaka 2000, baada ya kutokea mgomo na baadaye vurugu katika shule hiyo, na baada ya polisi kwenda kutuliza vurugu hizo iliripotiwa kifo cha mwanafunzi kutokana na matumizi ya nguvu kubwa ya polisi hao

4.4 Lugha

Kwa kawaida katika kazi yoyote ya kisanaa hasa ya kifasihi inazingatia sana lugha inavyo tumika. Katika kazi ya kisanaa lugha inayotumika ni ile yenye mvuto, na yenye kusisimua hisia za wasomaji na wasikilizaji. Lugha lazima isawiri yale ambayo wahusika wanayabeba, lugha ya fasihi mara nyingi huwa ni ile inayomfikirisha msomaji au msikilizaji ili kuibua hisia za watu. Msanii wa kazi ya kifasihi huweza kutumia ama lugha fiche au lugha wazi.

4.4.1 Lugha fiche

Jamii inatambua umuhimu wa matumizi ya lugha fiche katika kazi za kifasihi, hususani nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Wasanii hutumia lugha fiche kwa malengo mbalimbali. Kwanza, kwa kutumia lugha fiche huzipa nyimbo hizo uhai yaani kuzifanya ziendelee kudumu kwa muda mrefu, kwani huwafanya wasikilizaji mbali na kuburudika pia kutafakari kilicholengwa na msanii wa wimbo katika jamii halisi. Pili, matumizi ya lugha fiche katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa huwa na lengo la kiusalama kwa maana ya kwamba katika kanuni za kiuandishi au kiuimbaji kuna wakati msanii hapaswi kuweka mambo wazi wala kutaja majina ya watu pasipo na ridhaa yao kwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Tatu, matumizi ya lugha fiche huwa na lengo la kuongeza ladha ya wimbo kwa wasikilizaji wake. Kwa mfano ukiangalia wimbo “Miss Tanzania” ulioimbwa na msanii Msafiri Kondo anaejulikana kwa jina maarufu Solo Thang ametumia lugha fiche ili kumfikirisha msikilizaji au msomaji, kuuelewa anahitaji kuwa na tafakari ya kina.

Wimbo: “Miss Tanzania”- Solo Thang

Baba yake alikuwa mkoloni

Kipindi ulimrithi mwali

Mchonga alikata utepe

Lakini hakuvinjari sababu alikuwa *busy*

Kumlinda na geti kali

Kumbe wenzake wanabinjuka

Kushituka akakaa mbali

Demu alikuwa na heshima kabla haijatangazwa ruksa

Chukua chako mapema

Ukimkonyeza tu umegusa

Anakifua kimebetuka sio maziwa ni madini

Kayaacha wazi watu wanashika hapo ndio ananiudhi mimi

Watu wanagonga tu ikulu tena kwa mitindo huru

Kavukavu bila kinga

Hajali vinavyodhuru

Kwa shangingi amedata

Hana woga wa kunguru

Anapenda sana chapaa

Wimbo “Miss Tanzania” wa Solo Thang unazungumzia nchi ya Tanzania tangu kipindi cha ukoloni mpaka awamu ya nne ya uongozi. Kwamba, Tanzania ilikuwa chini ya uongozi wa kikoloni kipindi Mchonga (Mwalimu J.K.Nyerere) anairithi nchi na ndiye alikuwa kiongozi wa kwanza mzalendo kuiongoza. Yeye alijikita katika kuilinda na nchi wakati huo nchi ilikuwa na heshima, aliposhituka wenzake wanaitumia vibaya akang’atuka.

Baadaye, ilitangazwa ruksa kufanya kila kitu. Hiki ni kipindi cha uongozi wa Rais Alli Hassan Mwinyi, ambapo kila aliyehitaji nafasi alipewa; nchi ilikuwa tajiri maziwa pia madini. Kukawa na uhuru hakuna ulinzi watu wanachukua bila wasiwasi wowote. Watu wanaingia ikulu bila kizuizi cha aina yeyote bila kujali madhara yatakayotokea. Nchi haina woga; kila mtu ni rafiki na haichagui, ushuru na kodi havitoshi kuendeshea nchi. Tanzania ni nchi maarufu Afrika kwa kuwa na rasilimali nyingi kama vile mlima Kilimanjaro, madini kama vile dhahabu, almasi, tanzanaite, na shaba; maziwa, ardhi kivitaja kwa uchache.

Hata Benja hakutoka kapa, hiki ni kipindi cha uongozi wa Rais Benjamini Mkapa, msanii anasema pia katika kipindi hiki nchi ilikuwa bado haijatulia. Nchi inanuka na kunukia rushwa, na katika kiitikio msanii anakiri kuipenda nchi yake ila vitendo vyake hatojivunia, kwani sifa yake kubwa ametulia kifani cha mnyama anaekamuliwa na kila mtu pasipo usumbufu wowote. Msanii anatuambia angependa Tanzania iwe nchi ya mfano kama Flaviana Matata. Huyu aliwahi kushiriki mashindano ya urembo nchini Tanzania (Miss Tanzania) na ni mwanamitindo maarufu nchini Tanzania. Juzijuzi kaopolewa na handsomeboy, hiki kipindi cha Rais Jakaya Mrisho Kikwete

Katika wimbo huo tunaona msanii ametumia lugha fiche. Ili msikilizaji aelewe kinachoimbwa anahitaji tafakuri ya kutosha. Lengo la kutumia lugha fiche kwenye wimbo huu ni ufundi wa msanii kwa kufuata maadili ya kisanaa na usalama kisheria na kwa kufanya hivyo, amefanikiwa kufikisha ujumbe kwa jamii kusudiwa.

4.4.2 Lugha wazi

Vilevile jamii inakiri kuwepo kwa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zilizo wazi yaani zinazoeleweka kirahisi kwa kila msikilizaji au msomaji wa kazi ya kifasihi hiyo. Katika hali ya kawaida kazi yoyote ya kifasihi huwa na lengo la kuelimisha, kuburudisha, kuonya, kuarifu, kukemea uovu, kutia hamasa, kudhihaki uoga, kukuza lugha na mambo mengine yanayofanana na hayo. Hivyo, msanii mahiri wa kazi ya kifasihi hufanya kazi ya kuchagua lugha wazi na inayokubalika na kuifanya jamii ipate funzo kutokana na kazi yake ya kifasihi. Hata hivyo, tatizo linajitokeza katika kuelewa nyimbo hizo kutokana na waimbaji kuimba kwa haraka na kufanya maneno mengine kutosikika kirahisi hivyo kutoeleweka kwa wasikilizaji. Miongoni mwa wasanii wanaoimba kwa haraka ni pamoja na msanii Ferooz Mrisho katika wimbo wake “Mr Policeman”.

Wimbo “Mr Policeman”- Ferooz Mrisho

Unathamini wenye mali

Tabaka la chini ukituona *shallow (shallow)*

Ushalo uliopo tayari kujali kuja na Taifa pasipo na shali

Mr police police policeman

Tunakudisi kudisi kitaani

Mr popopo policeman tunakudisi kudisi kudisi mtaani

Juzi ulikamata mbakaji

Msanii katika wimbo huu uimbaji ni wa haraka sana kiasi cha kumtaka msikilizaji wake kuwa makini sana ili kuweza kuelewa kinachoimbwa katika wimbo huu, maneno yanayotumika yanaeleweka kwa Wasikilizaji.

4.4.3 Kuchanganya lugha

Suala la kuchanganya lugha katika kazi ya kifasihi kipera cha nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa, huwa na makusudio mbalimbali. Mathalani, wasanii huchanganya lugha katika kazi zao ili kuleta ujumi wa kisanaa, kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Pia, kutambua nafasi ya lugha nyingine katika mawasiliano, kuongeza ladha katika wimbo huo, kutambulisha utamaduni wa msanii/ mwimbaji. Vilevile, hutumika kama tasfida ya maneno yasiyokuwa ya kawaida ili kupunguza ukali wa maneno ambayo yangetumika katika nafasi hiyo, wakati mwingine kuficha mhusika wa tendo analolizungumzia msanii au mwimbaji. Sio hivyo tu bali pia hutumika katika kukuza msamiati kwa kutohoa maneno kutoka lugha nyingine na baadaye kusanifishwa na kuwa maneno ya lugha kuu (Kiswahili) kutokana na kupata mashiko kutoka kwa watumiaji wa lugha hiyo.

Wimbo “Kura yangu” ulioimbwa na msanii Bonta ni moja ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zilizotumika katika utafiti huu. Katika wimbo huu, uimbaji wake unachanganya lugha. Wimbo umechanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kama unavyoonekana hapa:

Wimbo “Kura yangu”- Bonta

Zahanati iko mbali baiskeli ilikuwa mbovu
Siwezi ondoa hilo kovu kwa moyo wa masikini
Kama mimi mwenye kovu la wovu

Kwa kweli migomo haiwezi kuisha kama shirika la reli

We have to look a people beyond a colour

Beyond a religion beyond a tribe

Just see the true nature

Natembea juu ya mbigili na kokoto

Natembea juu ya zuria jekundu

Ni rangi ya damu yetu watanganyika wa Kigoma

Ni rangi ya damu yetu watanganyika wa Ruvuma

Katika wimbo huo, msanii anajaribu kueleza jinsi raia wenye sifa ya kupiga kura wanavyopaswa kutumia nafasi hii vyema. Ikiwa ni pamoja na kumwelewa kwa kina mgombea anayetakiwa kuchaguliwa kabla ya kumpigia kura, asichaguliwe kwa kuangalia rangi ya mtu wala dini yake isipokuwa aangaliwe uwezo wake wa kuwatumikia watu waliomchagua na kuwaletea maendeleo. Madhara ya kumchagua mtu asiye na uwezo hatima yake ni wananchi kukosa huduma za kijamii, mathalani, huduma za afya, barabara, elimu n.k. Kukosekana kwa huduma za msingi husababisha vifo kwa wanawake wakati wa kujifungua. Msanii, anasema kuwa kitendo cha kuitumia vibaya nafasi ya kupiga kura huishia kuwapeleka kwenye nafasi za maamuzi watu wasio na uwezo wa kuwatumikia watu.

4.5 Mwitikio wa Jamii kuhusu Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo Rushwa

Utafiti unaonesha kuwa mwitikio wa jamii kuhusiana na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika kuleta mabadiliko kwa jamii upo. Jamii inasikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa na wasanii mbalimbali na kuzielewa. Hii inatokana na namna wanavyotoa maelezo kuonesha kufahamu dhana ya rushwa, kueleza mazingira ya rushwa yalivyo hususani yaliyoimbwa katika nyimbo

tulizozitumia. Pia wanavyojaribu kutueleza namna rushwa inavyobarikiwa na watu waliopewa nafasi za kuwatumikia wananchi. kwa kuzipatia majina mbalimbali ili kutoonesha ukweli wake, kwa mfano takrima, kunyosha mkono, maji, kitu kidogo na mengine yanayo fanana na hayo.

Utafiti unaonesha kuwa mwitikio wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii ni wa kutosha. Katika hili, U-marx huchukulia fasihi kama umbo maalumu ambalo hupatikana katika historia, na mbinu kubwa ya U-marx ni kuchunguza jadi na kuunda upya mtazamo kuhusu yaliyopita kutokana na ithibati za kihistoria, kisha kudhihirisha uhalisia wa kazi kama kielelezo cha jamii kwa njia ya kuelewa uhalisia. Hata hivyo, jamii inatambua umuhimu wa nyimbo hizo kwa kuwa zinatumika katika kuwasemea matatizo yao mbalimbali yanayowazunguka ya kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Nyimbo hizo pia hutoa mawazo na mwelekeo wa kupata suluhisho la matatizo hayo. Jamii inaamini kuwa kama nyimbo hizo zikipewa kipaumbele na makundi mbalimbali ya jamii na jamii kwa jumla katika mapambano dhidi ya rushwa zinaweza kuleta mabadiliko tunayoyataka.

Utafiti pia unaonesha kuwa mwitikio wa jamii kuhusu nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa ni mzuri. Hii ni kutokana na kuwakubali wasanii wanaojishughulisha na uimbaji wa nyimbo hizo kama ndiyo kioo cha jamii. Pia kutokana na kuwa mstari wa mbele katika kufichua maovu katika jamii ikiwa ni pamoja na yanayohusiana na rushwa.

Zaidi utafiti unaonesha kuwa mwitikio wa jamii kuhusu nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii ni mkubwa kwani watafitiwa tuliowahoji walieleza thamani kubwa ya ujumbe unaobebwa na nyimbo za Bongo Fleva mbalimbali zinazoimbwa na wasanii tofautitofauti katika jamii. Ujumbe huo

unakuwa na lengo la kuelimisha jamii kwa mawanda mapana ya kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa na kijamii. Hii ni kutokana na wimbo mmoja kukusudiwa kuelimisha jamii katika mambo mbalimbali kama masononeko, kukata tamaa, matarajio na furaha.

4.6 Mabadiliko ambayo Jamii inayapata kutokana na Kusikiliza Nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo Rushwa

Uchunguzi wa utafiti unaonesha kuwa kuna kiasi cha kutosha cha mabadiliko chanya juu ya rushwa yapo katika jamii kutokana na uelewa tuliouona kwa watafitiwa wetu tuliofanya nao mahojiano. Watafitiwa walionesha kuelewa uwepo wa mabadiliko ya jamii kutokana na kusikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii. Jamii inaingiwa na woga wa ama kutoa au kupokea rushwa, kutoa taarifa kwa mamlaka zinazohusika na udhibiti wa ama utoaji au upokeaji wa rushwa katika jamii. Kuwakamata wale wote wanaojihusisha na kutoa na kupokea rushwa katika jamii, pia kuielewa dhana nzima ya rushwa, mazingira ya utoaji na upokeaji wa rushwa kuwa siyo ya wazi kwa uelewa wao mazingira ya kutoa na kupokea rushwa yanapokuwa ya kificho tafsiri yake ni kwamba jamii inafahamu rushwa na athari zake. Hata hivyo, U-marx unajidhihirisha katika hilo pale unapoamini kuwa mabadiliko hayafanyiki kirahisi, yanapaswa yafanywe hatua kwa hatua. Kwa maana hiyo nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinaweza kutumika kama sehemu ya elimu kwa jamii na hata ikapata mabadiliko kama inavyooneshwa hapo chini.

Mosi, ni kuingiwa na woga wa kutoa na kupokea rushwa katika jamii, ishara ya mabadiliko chanya inayoyapata jamii kutokana na kusikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii. Kutokana na suala la rushwa kuwa adui wa haki kwa jamii na kupigiwa kelele kwa kiasi kikubwa na jamii kwa lengo la kulitokomeza

kabisa, kwani uwepo wake ni tatizo kwa watu katika jamii. Woga huo hujitokeza pale inapotokea kuwa utoaji na upokeaji wa rushwa huwa kwenye mazingira yasiyo ya wazi kutokana na wahusika kuelewa kuwa tendo hilo halikubaliki katika jamii. Hivyo watoaji na wapokeaji wa rushwa huitumia nafasi ya kutoa na kupokea rushwa kwa kificho sana ili kuficha na kutotambulika kwa usalama wao.

Pili, kupanuka kwa urazini wa kutoa taarifa kwa mamlaka zinazohusika na udhibiti wa rushwa katika jamii kwa mfano polisi, mahakama, na TAKUKURU. Katika kuonesha mabadiliko yaliyopatikana kwa jamii kutokana na kusikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Suala la kutoa taarifa pindi inapobainika kuwepo kwa tendo ovu la kutoa na kupokea rushwa katika jamii kwa mamlaka zinazohusika ili ziweze kufuatilia na kuchukua hatua stahiki kwa wale waliojihusisha na tendo hilo, ikiwa ni njia mojawapo ya kukomesha utoaji na upokeaji wa rushwa katika jamii.

Tatu, kushiriki katika kuwakamata wale wote wanaojihusisha na ama kutoa au kupokea rushwa na kuwafikisha katika mamlaka zinazohusika na udhibiti wa rushwa, kama vile polisi, mahakama, na TAKUKURU kwa hatua za kisheria. Hii ni hatua mojawapo ya kuonesha mabadiliko chanya yanayopatikana kwenye jamii kutokana na kusikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii. Kutokana na uelewa huo jamii inatoa rai kwa Serikali na vyombo vyake vya dola vyenye dhamana ya kushughulikia rushwa kama vile TAKUKURU, polisi na mahakama kutobweteka pindi yanapotokea matatizo ya utoaji na upokeaji wa rushwa. Vilevile jamii inaona kuwa mfumo katika Serikali ni tatizo pia kutokana na Serikali kuwa na mfumo wa kutotekeleza na kutofuatilia kesi za rushwa pindi zinaporipotiwa. Suala la urafiki, undugu, ukanda, ukabaila, rangi huchukua nafasi na kufikia hatua wanaochukuliwa hatua na wanaofungwa ni watu masikini tena wenye

kesi za rushwa ndogondogo ambao wanatoa ni wale wanaolazimishwa kutokana na matatizo yao, na wale wanaopokea ili kukidhi mahitaji yao kutokana na hali ngumu ya maisha wanayoishi. Mfumo pia unashindwa kushughulikia wale wote wanaojishughulisha na ama kutoa au kupokea rushwa kubwa kutokana na wanaojishughulisha na rushwa hizo ni watu wenye nguvu katika Serikali. Katika kuthibitisha hilo wasanii mapacha na wimbo wao “Rushwa” wanasema.

Wimbo: Rushwa- Mapacha

Hii vita ni ngumu sababu wanaotoa rushwa ni wale wenye mabavu
Wanaolimbikiza mali kama vile makaburu
Masikini wanabakia wanaugulia maumivu
Taifa la kesho sijui litarithi nini
Kama vyote vizuri wanataka wavimiliki
Mikataba wanayosaini nayo haiwekwi wazi
Wanaendelea kuficha mchezo wa kamari
Wananchi hawaelezwi, *which is very bad*
Wanaendelea kutoa wengine wanapokea
Hakuna cha kungojea matajiri wanajizolea
Kisa wanayo pesa toka mdogo nasikia jina rushwa
Kuwa ni adui wa haki na hakuna wa kumgusa
Mbona hamchukui hatua inayoendelea kukua
Asante TAMWA kwa kutupa nafasi ya kuweka wazi
Huyu adui wa haki rushwa adui wa haki
Huyu rushwa adui wa haki, hatumtaki

Utafiti umebaini pia kuwa kutokana na kusikiliza na kuzielewa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa jamii inapata ujasiri wa hata kuweza kuhoji juu ya vitendo vinavyohusiana na ama kutoa au kupokea rushwa katika mazingira yanayowazunguka. Vitendo vinavyoendeshwa na watu waliopewa nafasi za kuwatumikia wananchi katika sekta mbalimbali za umma au binafsi. vitendo hivi vinawanyima haki wanajamii wenye kipato kidogo ambao hawawezi kikidhi matakwa ya wenye dhamana hizo.

Utafiti umebaini kuwepo kwa kasi kubwa ya jamii kwa kujikomboa kifikra kutokana na kusikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Kujitambua huko kunawasaidia wanajamii kutambua athari za adui wa haki rushwa kwa maendeleo ya jamii husika na hivyo kuwa mstari wa mbele katika kupinga vitendo viovu vya kutoa na kupokea rushwa.

Utafiti umebaini kuwepo kwa mabadiliko makubwa kutokana na kusikiliza nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa hii ni kutokana na wanajamii wengi kushiriki katika kutoa elimu juu ya uraia ambapo rushwa nalo ni suala linalojadiliwa kwa kina wakati uliopo. Kutokana na hili, raia wengi wameamka kwa kiasi kikubwa na kushiriki katika kuelimisha jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Mathalani, kwenye makala mbalimbali kama vile zinazokusanywa na Haki Elimu, kushiriki midahalo mbalimbali ya hadhara inayoandaliwa na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali mfano Haki Elimu, kushiriki katika kuandika insha zinazohusiana na rushwa.

SURA YA TANO

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii yenye sehemu tano, imetoa hitimisho kuhusu utafiti huu. Sehemu ya kwanza imebeba muhtasari wa tasnifu hii, ya pili inadokeza utoshelevu wa mkabala uliotumika katika uchambuzi wa data za utafiti huu, ya tatu inazungumzia mambo mapya yaliyoibuliwa na utafiti huu, ya nne inatoa uchambuzi kuhusu mambo mapya ambayo yameibuliwa na utafiti wetu, na ya tano inatoa mapendekezo kuhusiana na maeneo yaliyogusiwa na utafiti wetu.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti ulijikita katika kuchunguza dhima ya nyimbo za Bongo Fleva kwa mabadiliko ya jamii, ambapo nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo Rushwa zilizokusanywa na kuchunguzwa ili kubaini dhima zinazopatikana.

Lengo letu kuu lilikuwa kuchunguza dhima ya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa kwa mabadiliko ya jamii, ambapo vipengele vilivyotuongoza kwenye utafiti huu kwanza ilikuwa kukusanya nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa zinazoimbwa na wasanii mbalimbali katika jamii. Pili, kuchunguza na kuainisha dhima zinazopatikana katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa. Tatu, kuchunguza mwitikio wa jamii kuhusiana na nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

Sura ya kwanza imetoa mwanga kuhusiana na dhana nzima ya Bongo Fleva huku tukieleza maana ya Bongo Fleva, sifa za Bongo Fleva, matawi ya Bongo Fleva na faida za Bongo fleva.

Sura ya pili hii imejadili hoja mbalimbali ambazo zinaweza kutoa mwanga katika uhusiano uliopo kati ya Fasihi Simulizi, ushairi na nyimbo. Baadaye, tumeangalia dhima zinazopatikana katika nyimbo mbalimbali kwa kufuata historia ya nyimbo tangu zamani zikiwemo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika jamii.

Sura ya tatu imejadili kuhusu mbinu na vifaa vilivyotumika maktabani na uwandani, mbinu na vifaa vilivyomwezesha mtafiti kupata taarifa lukuki kutoka kwa watafitiwa. Sampuli na usampulishaji ulifanyika na kupata sehemu ndogo sana kuwakilisha sehemu kubwa na kukidhi haja ya utafiti huu baada ya mbinu ya ufafanuzi wa data kutumika katika utafiti huu.

Sura ya nne imewasilisha data zilizopatikana kutoka uwandani. Hapa nyimbo zenyewe zimewasilishwa na kujadiliwa. Pia, imejadili dhima zinazopatikana katika nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa, pamoja na mwitikio wa jamii kuhusu nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa.

Sura ya tano imetoa muhtasari, hitimisho la tasnifu pamoja na mapendekezo. Pia imetoa maoni kutokana na utafiti uliofanyika.

5.3 Utoshelevu wa Mkabala tulioutumia

Mkabala wa Kimarx umetusaidia kubaini matukio mbalimbali ya kihistoria kwa sababu msingi wa Umarx huchukulia fasihi kama umbo maalum linalopatikana katika historia. Mbinu kuu ni kuchunguza jadi na kuunda upya mtizamo kuhusu yaliyopita kutokana na ithibati za kihistoria kisha kudhihirisha uhalisi wa kazi fulani kama kielelezo cha jamii. Mbinu hizi zilitupa unyumbufu wa mawazo.

5.4 Mchango Mpya wa Utafiti huu

Mchango wa kwanza ni kuziweka nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa katika maandishi na kuzifanya kutambulika kwa jamii inayoizunguka.

5.5 Maoni na mapendekezo

5.5.1 Maoni na Mapendekezo Kutokana na Utafiti huu

Utafiti unapendekeza mambo mawili ambayo ni kuhusu kuienzi fasihi na kuhusu mitazamo hasi juu ya Bongo Fleva kama ifuatavyo:

5.5.1.1 Kuhusu Kuienzi Fasihi

Kutokana na umuhimu wa Fasihi katika jamii nyingi za kiafrika, zikiwemo za kitanzania ni vema fasihi ikapewa kipaumbele ili kuipa uhai zaidi. Hata hivyo juhudi za kuienzi fasihi ya Kiswahili kwa Tanzania zinaonekana kutokana na vyuo vikuu kuanza kutoa shahada ya uzamili na hata uzamivu kwa lugha ya Kiswahili. Mnamo mwaka 2008, vyuo vikuu vya Dodoma na Dar es Salaam vilianza kutoa mafunzo tajwa kwa lugha ya Kiswahili. Utaratibu huu unapaswa kupongezwa kwani unatoa nafasi ya wanafunzi kubobea katika fasihi ya Kiswahili kinyume na awali ambapo Fasihi ilifundishwa na kusomwa kwa lugha ya Kiingereza. Hii ilifanya utamaduni wa Mwafrika hususani Mtanzania kupotea kutokana na utamaduni wa Mtanzania kuwa katika lugha ya kigeni. Hivyo basi mkazo zaidi unatakiwa kwa wataalam wa fasihi kuendelea kuvifanyia tafiti vipengele mbalimbali vya fasihi ikiwa ni pamoja na nyimbo za Bongo Fleva.

5.5.1.2 Kuhusu Mtazamo Hasi juu ya Bongo Fleva

Utafiti katika uchunguzi wake umegundua kuwa jamii bado inakuwa na mtazamo hasi juu ya nyimbo za Bongo Fleva kupitia vipengele mbalimbali, kwa mfano katika maleba, uchezaji na lugha inayotumika.

a) Maleba

Maleba ni aina yoyote ya mavazi yanayovaliwa na wasanii wawapo katika sanaa kwa lengo la kuleta burudani na wakati mwingine kuleta funzo tegemeana na lengo la msanii mwenyewe. Wasanii wa kiume huvalia mashati au fulana kubwa, viatu vikubwa au vyenye visigino virefu na suruali zinazobana, kusuka nywele na kuvaa hereni. Wakati kwa wasanii wa kike huvalia nguo zinazowabana na fupi na pengine kuacha baadhi ya sehemu za miili yao wazi, kama vile mapaja, tumbo, na mgongo. Uvaaji huu unaifanya jamii kutopenda kusikiliza nyimbo hizi na hata kuona picha zinazoigizwa na wasanii hawa, hii ni kutokana na kuona kwamba muziki huu ni wa wahuni na haupaswi kuigwa na jamii. Pendekezo la Utafiti kwa wasanii wa Bongo Fleva kuvaa mavazi yanayolinda utamaduni wa Mwafika katika kazi zao ili kuwavutia mashabiki wao.

b) Uchezaji

Wachezaji katika nyimbo ni wahusika ambao hutumika kufikisha ujumbe, kuburudisha watazamaji na wakati mwingine huwa waimbaji pia. Wakati wakiwa jukwaani, uimbaji wao huenda sambamba na matendo ya mwili, yaani matumizi ya viungo vya mwili. Katika hili, waimbaji na wachezaji huzitumia sehemu za miili yao kwa kuzizungusha katika kucheza, mathalani, kuzungusha mikono, mabega, kichwa, na kiuno. Hata hivyo Utafiti unapendekeza wasanii wetu katika hatua za uandaaji wa

sanaa hiyo, kujikita katika kuenzi Utamaduni wa Mwafrika zaidi kuliko ule wa kigeni.

c) Lugha inayotumika

Mtazamo hasi kuhusu lugha ya matusi inayotumika katika nyimbo za Bongo Fleva ijapokuwa sio zote zitumiazo lugha ya matusi. Utafiti unashauri wasanii kujitambua na kuelewa kuwa wao ni kioo cha jamii na wanapaswa kutumia lugha ambayo itakubalika na jamii pasipo kuwa na shaka. Matumizi ya lugha ya matusi katika kuimba, hayana lengo la kuielimisha jamii bali kudharirisha utu wa mtanzania na jamii kwa ujumla wake.

5.5.2 Mapendekezo ya Mtafiti

Mapendekezo ya mtafiti yamegawanywa katika makundi: la kwanza, ni kwa Serikali; la pili, kwa wasanii wenyewe; na la tatu, ni kwa watafiti wajao. Kama inavyoainishwa hapo chini:

a) Mapendekezo kwa Serikali

Serikali ihamasishe na kukitilia mkazo kipengele hiki cha nyimbo za Bongo Fleva kwa kuwaunga mkono wasanii wa Bongo Fleva kwani nyimbo zao zinabeba na kusambaza ujumbe mbalimbali ukiwa na lengo la kuionya, kuelimisha na kuifundisha jamii maadili mema kupitia usanii wa Bongo Fleva. Matatizo ya ndani na nje ya jamii zetu yamekuwa mengi kiasi kwamba bila ya msaada kama wa wasanii hawa hatuwezi kupata suluhisho la matatizo kama rushwa, magonjwa, mapenzi, manyanyaso na mengine yanayofanana na hayo ambayo yamekuwa tishio kwa jamii.

Pia, serikali iwaache huru wasanii na kukubali kujifunza kutoka kwao badala ya kuwatisha, kufungia kazi zao zinazokuwa na mrengo wa kuisuta serikali kwa maovu yake, kwa mfano wimbo *Hatunaga* wa msanii Suma Lee, wimbo *Roma Viva Roma* wa msanii Roma Mkatoliki zimefungiwa. Hii yatokana na ukweli kuwa wao ndio kioo cha jamii wenye kazi ya kuleta mabadiliko kwenye jamii kutokana na mafundisho wanayokusudia kuyatoa. Serikali inapaswa kuyachukulia kama changamoto yale yote yanayozungumzwa na wasanii katika kazi zao kisha kuchukua hatua stahiki ili kutatua. Vilevile, serikali ijiweke jirani na kundi hili la sanaa kwa kuwafanya wasanii kutambua miiko ya jamii, na kuwahamasisha kutambua umuhimu wa kuwa na kitengo cha uhariri na faida zake kwao na kwa jamii pia.

b) Mapendekezo kwa wasanii wenyewe

Muhimu kwa wasanii kuunda na kuanzisha kitengo cha uhariri wa kazi zao ili kizihakiki kabla ya kuziingiza sokoni. Hili litawahakikishia usalama wa kazi zao kimaadili na kuifanya fani hii kupendwa na kuheshimiwa na watu wa rika mbalimbali.

c) Mapendekezo kwa watafiti wajao

Kutokana na mkanganyiko uliopo katika makundi ya nyimbo zinazowekwa pamoja na kuunda kundi moja la Bongo Fleva, ni vema wataalam waendelee kukifanyia utafiti kipengele hiki cha nyimbo za Bongo Fleva ili kuainisha makundi mbalimbali ya nyimbo za Bongo Fleva zinazoweza kuwekwa pamoja na kuunda kundi moja.

Aidha tafiti zaidi zinahitajika katika kutafiti juu ya wasanii wa nyimbo za Bongo Fleva kuchanganya lugha katika uimbaji wao. Hapa swali la kujiuliza ni hili Je, kwa nini wasanii hupendelea kuchanganya lugha katika nyimbo zao? Je wasanii wa mataifa mengine wana utamaduni huu? Maswali haya na mengine mengi yanatoa nafasi ya kuwepo kwa tafiti nyingine zaidi katika nyimbo za Bongo Fleva.

MAREJELEO

Blommaert, J.(2006). "Applied Ethnopoetics". *Narrative Inquiry* 16(1):181-190

Finnegan, R. (1970). *The Oral literature of Africa*, Oxford University Press, Nairobi.

Kadallah, R.T. (2010). "Muziki wa Bongo Fleva na Changamoto za Kimaadili katika Jamii", katika *mulika*, toleo Maalumu la Muziki wa Kizazi Kipya, Na.29/30.

Kezilahabi, E. (1981). *Ushairi na nyimbo katika utamaduni wetu*, Tanganyika Publishing House, Dar es Salaam.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology, Methods and Techniques*, Second Revised Edition, New Age International (P) Ltd, Publishers

Majembe, A.K. (1998). "Language Use in the Tanzania Hip Hop Scene", Research Paper, (Unpublished), Dar es S alaam: University of Dar es Salaam.

Mangesho, P. (2003) "Global Cultural Trends: The case of Hip Hop Music in Dar es Salaam", Unpublished MA Dissertion, University of Dar es Salaam.

Mnenuka, A.(2010/2011). "Taswira ya Mwanamke katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano kutoka katika Nyimbo Teule", katika *mulika*, Toleo Maalumu la Muziki wa Kizazi Kipya, Na 29/30

Msokile, M (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam University Press. Dar es Salaam.

Mulokozi, M.M (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

_____(1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Dar es Salaam.

Msuya M.B na A.P. Lupokela (2010/2011). "Dhima ya Bongo Fleva katika Maadili na Malezi kwa Jamii", katika *mulika*, Toleo Maalumu la Muziki wa Kizazi Kipya, Na 29/30.

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi*: Printpark (T) Limited, Dar es Salaam.

Nkwera, F. (1978). *Fasihi na Sarufi kwa Sekondari na Vyuo*, Printpark (T) Limited, Dar es Salaam

Ntiluhoka, G. (2007). "Availability and Suitability of Study Materials Provided to Students Learning Thruogh Distance Education: Acase study of the Open University of Tanzania", Unpublished Report (MA.Dissertation), University of Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Omari, S. (2009). "Tanzanian Hip Hop Poetry as Popular Literature". Unpublished PhD (Literature) Thesis. University of Dar es Salaam.

Perullo, A. (2003) "The Life That Live" Popular Music Agency and Urban Society in Dar es S alaam Tanzania. Indiana Univesity.

Sekile, R.(2001). "Utamthiliya kwenye Matambiko ya Jamii ya Wanyakyusa", (haijachapwa), Chuo Kikuu Dodoma, Dodoma.

Senkoro, F.E.M.K (1982). *Fasihi*. KAUTTU Limited: Dar es Salaam.

Simiyu, W.F. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi Kwa Shule*, Vyuo na Ndaki, Serengeti Bookshop Tanzania.

Songoyi, E.M (1989). "The Arts and The State of Tanzania: A Study of Two Singers, Kalikali and Mwinamila". M.A Dissertation, University of Dar es Salaam.

_____2005). "The form and Content of the Wigashe Dance song of Sukuma" (PhD) Thesis: University of Dar es Salaam.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press: Nairobi.

Wafula, R na Njogu, K (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. The Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi;* Misingi *na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishing, Nairobi.

_____ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Focus Publications, Nairobi, Kenya.

VIAMBATISHO

A: HOJAJI KWA WASIKILIZAJI WA BONGO FLEVA KATIKA JAMII.

1. Je, unafahamu nyimbo za Bongo Fleva?
2. Kwa nini nyimbo hizi zinaitwa Bongo Fleva?
3. Je, ni wasanii gani wa nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa unaowafahamu?
4. Je, ni nyimbo zipi za Bongo Fleva zihusuzo rushwa unazozifahamu?
5. Je, katika nyimbo hizi tunaweza pata dhima gani?
6. Je, nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa hutumia lugha fiche?
7. Ikiwa hutumia lugha fiche, unadhani kwa nini waimbaji huamua kutumia lugha fiche?
8. Katika kusikiliza au kuimba nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa huwa kuna ugumu wowote unaoupata katika kuelewa kile kilichomo?
9. Je, jamii ina mwitikio gani kuhusu nyimbo za Bongo Fleva zihusuzo rushwa?
10. Je, kuna mabadiliko yoyote chanya ambayo jamii inayapata kutokana na kusikiliza nyimbo za Bong Fleva zihusuzo rushwa?

B: NYIMBO ZA BONGO FLEVA ZIHUSUZO RUSHWA.

MTAZAMO-SOLO THANG ft PROF J, AFANDE SELE

Ubeti wa Kwanza

SOLO: Ya! Ya!

Hakuna S bila O, L bila O
Mwingine aitwa Thang bila Solo shupavu
Awajibike kama Prof Jay, Afande
Ni ukuta wapi chochoro
Hakuna S bila O, L bila O
Mwingine aitwa Thang bila Solo shupavu
Awajibike kama Prof J, Afande,
Ni ukuta wapi chochoro,
Hiyo naghani ni mtazamo wa fani,
Ile dhana ni uhuni wanaleta wa katuni
Kuna kurap na kuvata marepa na marapa
Katuni tungo tata wapi ulipo we japo
Unakuwa mtumwa ili upewe promo kuuza
Au kama ni binti ukalale kwa maproduzer
Mapromota wanauma so hawajui na kupuliza
Na siku wakipuliza ujue kidonda kishaoza
Natamani kuwa huru mnyonyaji asinidhuru
Wanaitwa maMC hawajui mitindo huru
Huu mtazamo wangu naona vingi vioja
Yaani watangazaji sasa ndio mameneja
Vidato sita nilivyo pitia ndivyo vinavyo nisaidia
Mbunifu ukizingatia hata wakinibania ni kipaji tu ni mtazamo tu
Msikasilike washikaji haya ni mawazo

Korasi

PROF J: Ni mtazamo zamo MC usiogope kivuli
Bora ukemee mabaya na usifie mazuri
Ni mtazamo zamo MC usikwepe umande
Okoa sanaa ya bongo ili uchumi upande

Ni mtazamo zamo MC usiogope kivuli
Bora ukemee mabaya na usifie mazuri
Ni mtazamo zamo MC usikwepe umande
Ni mtazamo rap iakuwa ni mikingamo

Ubeti wa pili

Sasa watoto wadogo wanajiita watu wa makamo
Wanakwenda hatua mbili wanarudi kumi na moja kuongeza
Bila kuzingatia hatua zao walizo poteza
Hao ni mafukara wa akili zao na uwezo wao
Wasiotambua lini na nini hatima zao
Magwiji vichwa chini nadhani wanatunga sheria
Sheria ni msumeno angalia isije ikawarudia
Yes!
Ma-underground wanafanya rap inang'ara
Lazima muwe vinara imara kwenye msafara
Rap na mazingaombwe all time haviendani
Msitegemee hailee iwaokoe kwenye fani
Ni vema ukafikiri kabla ya kufanya maamuzi
Tazama mbele usije ukanywa chai kwa mluzi
Kabla hujaingia kwenye fani lazima upite depo
Vinginevyo ndugu yangu utakuwa unapaka rangi kwenye upepo
Kama unapata moja kwanini usipate na mia
Hiyo inawezekana kwa wote walio na nia
Kwanini msipate sioni sababu za msingi kuomba kwenye hadhara
Kama unakipaji iweje ufe na njaa?
(Rudia korasi)

Ubeti wa tatu

AFANDE: Asante Prof J, Majani na Ulamambe
Umegusa napopataka
Nami kwenye mtazamo kuna jambo nataka kuweka
Maana kila kukicha MCs wanaongezeka

Nasema very nice

Yes!

Rap kama dhehebu MCs kama wafuasi

Wingi wa wasanii inaonesha ni dini safi

Yaani imekubalika

Waumini tupo wengi lakini bado nashaka

Sijapata uhakika wote tumesadiki au wengine ni feki

Mmetumwa kama mamluki manake hamna maana

Mnarap na mnavyorap mistari imekosa vina na yenye vina haina maana

Kila mnapo kaa mnapenda kusengenyana

Mnapenda kutetana na mnapenda kulumbana

Mimi naogopa sana kwa jinsi navyo elewa mtatukanana

Mwisho mkaja chinjana na wote tunaorap tuonekane hatuna maana

Wapi ilipo taarab ilikuja kwa kishindo

Kwa ajili ya malumbano mwishoni ikafa kibudu

Shabiki piga simu changia mawazo yako

Nani tutamlaumu kama rap ikisizi kwa kuendekeza upuuzi

Nani tumchune ngozi

Produzer anayerekodi ama labda DJ anayepiga kwenye kipindi

Wengi wanapenda rap japo rap haiwapendi

Waungwana wanaiacha pumbavu hawaambiliki

Hivi ni lazima wote tuwe wanamuziki

Mi nadhani ngetosha wengine mbaki mashabiki

Huu ni wangu mtazamo mashabiki msijenge chuki

(Rudia korasi)

MR POLICEMAN-FEROOZ ft MAUNDA

Ubeti wa kwanza

FEROOZ: Unathamini wenye mali

Tabaka la chini ukituona shalo (shalo)

Ushalo uliopo tayari kujali kuja na Taifa pasipo na shali

Mr police police policeman

Tunakudisi kudisi kitaani

Mr popo po policeman tunakudisi kudisi kudisi mtaani

Juzi ulikamata mbakaji

Leo yuko huru

Tuulize mahakama au jaji?

Kwenye mataa yazidi nusu saa

Ajali mbaya imetokea unalewa *bar*

Tunaita mwizi! mwizi! jizi!

Unaukaribisha usingizi

Ulivyo nikuta na majani

Ukanipiga pingu kisha ukanisweka ndani

Jamani mimi nilisha puuuna aaah!

Ukanichukulia mapene bila tuhuuuma aaah!

Masela madawa ya kulevya yanakua kila kukicha

Masela wananyeta tena cha ukucha

Uko mbele na sima unakula unataka ushibe eeeh!

Acheni ulimwengu wa majemedari washibe

Oooh! Oooh!

(Rudia korasi)

Ubeti wa pili

Hands up! Hands up!

Mikono juu anakuandikia kesi

Wote *hands up! hands up*!

Mikono juu! Anahitaji *cash*

Hakuna kithibiti kosa la uzushi unapiga mtu mpaka anashindwa kuishi

Umeharibu hata kwa wangu wa ubani mpenzii

Eti mimi ni tapeli kudumu naye siwezi

Kumbe moyoni unamtamani

Kutamani wake za watu yatakutokea puani

Kwenye radiocall ukiwa na wenzako

Pande zote mnitafute mkaanza msako

Nikiwa kwenye pilika nahangaika na njia

Wakatokea masela waliokata tama wote tukatambaa

Nikakimbilia kwa hofu kwa polisi nao nusura wanitoe mnofu

Nikakimbilia kwa hofu kwa polisi nao nusura wanitoe mnofu

(Rudia korasi)

Ubeti wa tatu

MAUNDA: Shali shali shali oooh!

FEROOZ: Mambo unapeleka holela holela

Kila kitu holela holela

Wakushi majita sio uzushi sio dawa masela wako jela aaah!

MAUNDA: Shali shali shali oooh!

FEROOZ: Mambo unapeleka holela holela

Kila kitu holela holela

Wakushi majita sio uzushi masela sio uzushi pia nao wako jela

MISS TANZANIA-SOLO THANG

Ya!

Aha!

Miss Tanzania aha!

You know how we do

We love you!

Yes lahaula!

Ubeti wa kwanza

Baba yake alikuwa mkoloni

Kipindi ulimrithi mwali

Mchonga alikata utepe

Lakini hakuvinjari sababu alikuwa busy

Kumlinda na geti kali

Kumbe wenzake wanabinjuka

Kushituka akakaa mbali

Demu alikuwa na heshima kabla haijatangazwa ruksa

Chukua chako mapema

Ukimkonyeza tu umegusa

Anakifua kimebetuka sio maziwa ni madini

Kayaacha wazi watu wanashika hapo ndio ananiudhi mimi

Watu wanagonga tu ikulu tena kwa mitindo huru
Kavukavu bila kinga
Hajali vinavyodhuru
Kwa shangingi amedata
Hana woga wa kunguru
Anapenda sana chapaa
Haitoshi kodi na ushuru
Anakijungu matata laini kama nyanya masalo
Anatingisha Afrika nzima na mlima Kilimanjaro
Usimchezee kwa vidani sio pete sio heleni
Ana miliki tanzanite kama ardhi ya mererani
Sura dhahabu inaita kama amezaliwa geita
Tatizo ndio kicheche kila mwanaume ndio amepita
Hata Benja hakutoka kapa huyu demu hajatulia
Kama rushwa ndio kikwapa ananuka na kunukia
Nakupenda ila hujatulia vitendo vyako sitojivunia
Sifa yako kubwa umetulia (wanakamua)
Miss Tanzania
Nakupenda ila hujatulia vitendo vyako sitojivunia
Sifa yako kubwa umetulia (wanakamua)
Miss Tanzania
Bora angebaki kuwa model kama Flaviana Matata
Ila demu amejiachia kisa anaendekeza bata
Sitachoka kuwakilisha jinsi alivyoniacha hio
Juzijuzi kaopolewa na *handsome boy*
Kabla ya hapo shoga zake wote kashawaona mabwege
Sababu hawana dira nayeye amesha hongwa ndege
Anafaa kuwa miss dunia maandalizi longolongo
Tatizo anakula sana akijamba ni songosongo
Mara ghafla kanenepa kumbe mimba ni BOT
Kumbe demu aligawa epa watu wamepiga *half* jii
Alizugwa na akaunti hewa kuwadi bwana Balali
Mara mdomo nae kazimwa bila hata picha ya kabuli

Kinacho mponza huyu shawty utulivu sifuri
Ila hakuna anae pinga kwamba huyu demu ni mzuri
Mixer siasa na biashara demu amesha kuwa chotara
Mishe za Dar akimaliza mjengoni anakwenda lala
Kadri miaka inavyo kwenda demu anazidi fulia
Kumbe weupe ni mkorogo ona mwili sasa umefifia
Demu kazidi umalaya wacha mabwana wamteme
Haogopi kuliwa mtungo kisa anagawa umeme
(Rudia korasi)

Ubeti wa pili

Wadaku walisha mfuma anakula denda na Richmond
Dowans akazidi kete akamvisha pete ya *diamond*
Binti maskini akanasa bwana mshenga ndio Lowasa
Shemeji hataki hata picha ndio tabia gani sasa
Ndoa ilifungwa kwa vifijo vigogo wakala pizza
Keki nzima wale wao share yetu sisi giza
Sio hayo demu ana mengi ya kuchukiza
Mali ghafi ashazinadi forsale anajiuza
Mtaani alivuma rumar demu kawa mama huruma
Uchumi umefungwa *drip* maendeleo ndio kila homa
Maliasili ndio kitasa kila ufunguo ndio unapita
Toka ulipovunja ungo nusu karne imeshapita
Mapenzi kafanya mradi anamegwa na mafisadi
Amani kwa time bomb binti amekumbatia radi
Vitendo vyake vibaya vinafanya adharaulike
Tabia katiba sio msahafu ndio useme asibadilike
Mikosi inayo mkuta ndio kwanza anatabasamu
Hajali waliomzunguka kama nao binadamu
Mbagala walimbaka mpaka akamwaga damu
Na juzi Gongo la Mboto kaanza kujamba mabom
(Rudia korasi)
Niko mbali lakini nakuwaza wewe.

2030 –ROMA ft STORY

Ubeti wa kwanza

Tanzania eeeh! Nchi yangu eeeh!

Huwezi kuijenga Roma haikujengwa kwa siku moja

Ila kwa raha leo simba mtoto

Tanga atakuja hata Patcho pia ni mwamba

Ila bado anakata viuno kaskazini bila Tanga

Ni msondo bila Gurumo

Alisema juu ya mwamba atalijenga kanisa na halitatikisika

Waumini tuianze misa mwenye njaa kula kuku aliechinjwa na padre

Walah adhana ikilia

Amka kamwombe allah

Aise mrudie Mungu Masanja kawa Mchungaji

Msujudu Maka na daina tajiri hataki kuhiji maulid

Ubungo kibangu ndo mishahara ya madrasa

Rafiki wa Padri kawa mhasibu wa kanisa

Tenda wanapeana kindugu mwanangu kua uyaone

Familia ilikata dingi na mama alibaki mjane

Sikuwa na damu ya kiarabu kwamba nitarithi mabasi

Dingi hakutupa msingi wa magari tukayafanya tax

Tazama gongo la mboto mtoto kazaa mtoto

Na atalelewa na nani babaake mmemfunga keko

Wape buku waue winga wale watoto wa Moroco

Mungu atazidi kulinda kesho wataiona sabato

Mzee wa pangani kastaafu kajenga banda la uani

Hana uhakika watoto watarithi nini

Ndio chanzo cha kurogana na kutupiana majini

Huyu akipandisha mayana yule maimuna subi

Na pesa ndio ilifanya tusiwe na tanga ndugu

Pesa ilileta ubaguzi kati ya royora na pugu

Pesa ndio iliyochochea bifu kati ya Nice na Dudu

Pesa ndio ilimaliza vita kati ya Ruge na Sugu

Tanzania eeeh! Nchi yangu eeeh!

Mwanangu kuwa uyaone kama nitawahi kuiona Paradiso

Mtunze mama mwanangu kuwa uyaone

Marehemu hufa na chake pigana upate chako

Tanzania eeeh!

Mwanangu kua uyaone mwalimu chezea kibati wanao wasife njaa

Nchi yangu eeeh!

Mwanangu kuwa uyaone elimu imekosa thamani NECTA imevuja kibao

Ubeti wa pili

Aminini nawambieni ujana maji ya moto

Mtoto humzika mama leo mama anamzika mtoto

Ndio maana mama alisema nisimchumbie mmachame

Mula shusha mapanga anaeleta kosa Tarime

Bahari imechafuka leo bahari imechafuka mpemba iheshimu karafuu

Hatari kama nungwi nahodha sio kama kirikuu

Yahee nirushie mtumbwi mwamba sio kichuguu

Hii ni vita ya msambaa mbondei usitie mguu

Ona kipindi cha Bunge Dodoma inanuka ngono

Spika akiahirisha Bunge wengi watausapoti mgomo

Wabunge mnadai posho mhonge dada zetu

Kuna wanafunzi wa mama Salma vyuoni usicheze peku

Wazanzibari hawaioni thamani ya muungano

Ila kulichoma kanisa ndio njia ya kuuvunja muungano

Sioni sababu ya ubaguzi na kuua wasio na hatia

Wakati aliye changanya mchanga umemfukia

Mwisilamu gani unahonga bongo movie mamilioni

Mama anakufa mwisela kakosa *drip* ya kwinini

Ni heri tujenge misikiti ili tutukuze mitume

Anasa za bakulutu unatuza wacheza sebene

Unamweshimu Ramadhan unazini mbele ya Shaban

Kama ilishushwa kuruani twendeni msikitini

Anae dhihaki msahafu pengine kanisa halijui

So kulichoma kanisa kuza *bible* Dubai

Usihofu kumpoteza mmoja ili kumi waishi vema
Watanzania tuna uoga sio amani tunadanganywa
Amka kifikra damu yako iwe chachu ya ukombozi kama Dkt Ulimboka
Mkinga usimuue mama ili uongeze kipato
Utajiri upo kaburini watu wamekufa na ndoto
Leo Ridhiwan hafanani na Makongoro
Dah sina hela ya kiroba Rashid nigongee ugoro
Suka akaiangusha roli ya mafuta yote magendo
Waziri anauza pembe za ndovu na meno ya tembo
Nchi imejaa misitu uhaba wa madawati
Tunakula vitu feki wa-TBS mko wapi?
RPC usitume kikosi ili uishushe CHADEMA
Mahali ilipo damu ya Mwangosi Iringa kasemeni amina
Okoa saratani mipakani zuia wakimbizi
Kuliko kumwaga pesa kwenye tume za uchunguzi
Muhimbili naumwa goti eti Dkt kanipasua kichwa
Mbeya wanapigwa nyundo ili raia wauze mabucha
Amana wanawatelekeza watoto wanalia
Mwananyamala wanatuua na hawaendi jela
Jela anakwenda Kajala
Tanzania eeeh!
Mwanangu kua uyaone Rais acha kisirani gonga muhuri tuwahi
Nchi yangu eeeh!
Mwanangu kuwa uyaone rafiki hasira za mkeo hazifai barabarani (hazifaii…)
Tanzania eeeh!
Mwanangu kua uyaone wanahonga mashabiki ngoma zao wazi-request
Nchi yangu eeeh!
Mwanangu kua uyaone udini wa ma-presenter wapagani unatu-cost
Ubeti wa tatu
Sauti hii itasikika mpaka oldonyolengai
Nikifa naomba nizikwe Tanga na mje kwa shambalai
You can kill me but you can't kill what I'm standing for
Usitamani urithi wa baba zikimshuka CD4 eti sikustahili

Hii ni hatari!

Tuzo inachapa nani?

Ya kaisari mpe kaisari

Hii sio Masaki, Ngaramtoni mama anaiuza dadii

Muziki umejaa stress kila nyumba ni msanii

Yanga wamefukia mbuzi golini

Simba anabundi

Viongozi wana umatemate hawaujali ushindi

Utasikia Chuji kachuja, kiburi

Ulichoma mahindi kapigwa ligi ya jogoo shahidi kamata ufundi kijijini

Tupo wengi mleteni Dkt bingwa anangoma utasikia karogwa twende kwa mganga

Pesa za kujikimu ndo ulichongesha kitanda

Kulea mimba sio mchezo bakijacho hujapanga

Profesa kanyimwa penzi utasikia Caro ka-*disco*

Na Caro analea ndugu kwa pesa ya bodi ya mikopo

Pole mnaotafuta "C" mwaka wanne headmaster kaenda mjini eti shule imeishiwa chaki

Msiwaue wachimbaji wadogo Geita inalia

Kaburu mmempa migodi UDSM tuna *Engineer*

Umepewa kontena la condoms muihonge dhahabu

Mv spice imezama Tv inaonesha taarabu

Kamanga waiweke lami ili tuvuke Busisi

Dereva usinitoe kafara ili kutimiza ahadi ya bosi

Acha kuweka rehani kwenye asasi za mikopo

Bajeti ya kilimo kwanza mkulima silioni soko

Tanga wamekosa nini amkemi acheni umwinyi

Wachaga hawatuwezi ona Manka barishii

Magamba inaua katani

Zitto akiroga Kasulu sisi tunaroga Pangani

Uchafu wa Mrisho unafanya msafi aonekane benchi

Sadiki magazeti waandishi wengi kanjanja

Vijana ndio nguvu kazi wengi wamejaa

Vitimbi mtaani wamekata nia

Majibu ya postmoterm kasha nunua wakili
Na hakimu kapewa kiwanja Kimara apige kufuli
Kucheki doni anainunua kesi
Kapuku anaipeleka mbele kama ngamia kwa hakimu wa kisutu
Tanzania eeeh!
Mwanangu kua uyaone
Nchi yangu eeeh!

NANG'ATUKA-PROF JAY

Ubeti wa kwanza

Napiga goti natubu kwa Mungu wangu na jamii
Nimefanya maovu mengi kwa kutumia cheo
Nikaamini cheo dhamana mnisamehe (mnisamehe)
Nang'atuka (nang'atuka)
Mola wangu nisamehe
Nimesha ikosea jamii nikajiita mungu mtu nikajiita nabii
Nang'atuka
Mwenyezi kumbuka na nafsi hii napiga goti natubu
Daima nitakuenzi
Muda sasa umewadia ndugu zangu
Watanzania mambo niliyo yafanya hayapaswi kusimuliwa
Tangu nilipo omba kura kwenye ndio mzee
Mkanipa na kusababisha uchumi ulegee
Kula zikawa kura nikaishi kwa milungula
Taratibu nikaanza badili mfumo wa sura
Nasisitiza sana masuala ya ajira kumbe mwongo
Nikaanza kugawa vyeo kwa hila
Sholi wangu nikaweka matahira
Nikasababisha uongozi wangu upoteze dira
Ukawa uongozi na sio uongozi bora
Na kila alienizidi kwa mali nilimpora
Mambo yote muhimu niliweka yawe ya mwisho
Nikawa muumini mzuri wa mauaji na vitisho

Mtu asiyeshindwa katika jambo lolote

Daima nitapata chochote katika muda wowote

(Rudia korasi)

Ubeti wa pili

Kwenye wodi ya wazazi hali ni mbaya

Na ndio kimada wangu alienda tibiwa ulaya

Sikujali chochote kwenye afya na kila wakishutumu nilisema hizo ni siasa

Niliwatupa lupango watu wasio na hatia

Ndugu zao wakanililia na kamwe sikuwasikia

Nilikuwa na roho ngumu ya ajabu hata kusimulia

Maana sikuzingatia kwenye masuala ya uraia

Daima nilishiriki kutetea majambazi maana walinipooza kila walipofanya kazi

Hii ilichangia wananchi wangu kusota

Nilikuwa zaidi ya Hitler na kaburu wa Pikdota

Niligawa mali nyingi kwa matajiri wa ng'ambo

Nikazusha mtafaruku kati ya machinga na mgambo

Sikupinga nchi yangu kuwa ya kitu kidogo

Pia nilifurahi kuhararisha hongo

(Rudia korasi)

Ubeti wa tatu

Nilishuhudia watu wakifa kwa njaa kali

Nikakaa kimya na kujifanya sina habari

Siku zote niliamini toa mali upate mali

Nikabebesha masikini magunia ya misumari

Nilisema hakuna uchawi angali ni mshirikina

Nikawa mtakatifu na mswahilina jina

Niliamuru ukizaa mtunze mtoto wako

Yatima sio mtoto wa kwangu

Mtoto wa mwenzako sio mtoto wako

Nikaacha yatima wakiteseka mitaani

Sikujali wazazi wao wameshatoka duniani

Muda sasa umefika nafsi yangu inanisuta

Nashindwa jinsi ya kuyafuta
Damu iliyomwagika sasa nasikia inanuka
Watu waliouwawa kwa hila na visa wanafufuka
Nilifanya unyama mwingi sistahili kusamehewa maisha yangu
(Rudia korasi)

NDIYO MZEE- PROF JAY.

Ubeti wa kwanza

Naam ndugu wananachi
MC wenu babu Ayubu ninawaleteeni habari
Kuhusiana na huyu mgombea wetu bwana Joseph Haule
Mpe kura za ndiyo kwa kuwa yeye ni mpenda watu wote
Ni mpenda amani na mtu mwenye huruma kwa watu wote
Kwa hiyo basi nawaomba ndugu wananchi mumoe kura ya ndiyo (makofi)
Naam basi, hivyo ndugu wananchi eeh tafadhari
Namkaribisha mgombea wetu bwana Joseph Haule ili aje kuzungumza na wananchi
Karibu,
Ok ok naitwa Joseph Haule mwana wa msolopagazi
Nadhani nimeletwa kuokoa hiki kizazi
Mimi ni mwanasiasa niliyebarikiwa na Mungu
Nimeletwa kwenu waungwana niwapunguzie machungu
Mimi ni mteule kusini mwa jangwa la Sahara
Ndiyo maana nimetunukiwa cheti cha juu cha utawala
Nina hekima kuliko mfalme Suleiman msiwe na wasiwasi
Na hii nitadhihirisha pindi mtakaponipa nafasi
Actually, nimedhamiria kuwasaidia
Taifa lenye nguvu duniani liwe Tanzania
Jamani makofi tafadhari basi jamani (makofi)
Ni mambo madogo tu, nitarekebisha mkinipa visiku vichache tu uchumi utapanda ile ghafla bin vu
Nataka Matonya afundishe Chuo Kikuu
Nchi ya Tanzania itang'ara ile kishenzi
Na nitahakikisha kila barmaid anamiliki benzi

Si mtafurahi dada zangu jamani? Ndiyo!
Basi endeleeni kunisifu kwa nyimbo na mapambio
Nipeni hiyo nafasi jamani hamuoni hali ni mbaya?
Nataka kuigeuza Tanzania kama Ulaya
Cha kwanza nitakachokifanya nitafuta umasikini
Wanafunzi mkafanyie practical mwezini
Kwenye mahosipitali nitamwaga dawa kama mchanga
Na nitafungua akaunti kwa kila mtoto mchanga
Mabomba yatatoa maji na maziwa nchi nzima
Watu wa vijijini mtasahau habari ya visima
Nitafadhiri wachawi waweze kutengeneza ndege
Kila mtu awe na yake makonda na wapiga debe
Si mtafurahi watanzania jamani?
Ndiyo mzee
Sikweli nakubalika jamani?
Ndiyo mzee
Basi mimi ni mkombozi wenu jama?
Ndiyo mzee
Na nitafuta shida zenu zote
Ndiyo mzee
Hivi ni nani ni vijimambo tu
Ndiyo mzee
Na vinanikera kweli kweli mimi
Ndiyo mzee
Basi hali itabadilika sawa!
Ndiyo mzee
Na hatamu nitaishika ok!
Ndiyo mzee

Ubeti wa pili

Wafanyakazi wa serikali nashangaa hamna magari
Yaani hata mikweche, ha! ha! Hii ni hatari
Na nina mpango wa kuongeza mishara iliyo minono

Mara mia moja ya ile ya mwanzo iliyofanya fanya mfanye migomo
Nitawapa nyumba nzuri na majumba ya kifahari
Watu watashangaa mtakapopita kila mahali
Mkulima kila mmoja nitampatia trekta
Nadhani hiyo ndiyo itasaidia kunyanyua sekta
Mtauza nafaka zenu bilioni kwa mabilioni
Watu midomo wazi kama wameshikwa ugoni
Walimu zawadi zenu mh nimezificha moyoni
Nadhani mtazimia siku mkizitia machoni
We acha tu, mtafurahi ninyi
Ila hapa hapamfai mtu mwingine niwekeni mimi
By the way polisi wote mi nawasifu
Jinsi mnavyokwenda sahani moja na wahalifu
Sasa kila mmoja nitampatia helkopta
Nadhani hiyo ndoto wote hamjawahi kuota
Raia wa Tanzania mtalala mlango wazi
Infact nina uhakika wa kudhibiti ujambazi
Nitajenga barabara tano tano chini na juu
Natajenga kumbi nyingi sana za starehe baharini
Napenda kuitwa mshumaa kumulika wenzangu
Na mtakaoyumba kiuchumi tutagawana vya kwangu
(Rudia korasi)

Ubeti wa tatu

Ndugu wagombea kuna mtu ana swali kutoka kwa mgombea?
Nauliza hivi kuna mtu ana swali kutoka kwa mgombea?
Basi ajitokeze ili aweze kuuliza swali
Nyie ndugu huyu msimpe kura
Sio mzuri mwongo tu mnafiki na ni kiburi kimsuli
Anaongopea sana sijui kazaliwa muda gain
Asubuhi au alasiri?
Au wakati wa mvua zile za kipindi kile
Amepitapita school lakini mambo yake si mazuri
Wala tusimtegemee atatuangamiza

Labda angesubiri kwanza uchaguzi umekwisha
Tumemfuma wenyewe kwa Kalumanzila anasafishwa
Kalumanzila akamwambia ‘eee shida yako?’
‘Eleza *faster faster* kabla ya jinni halijapanda’
Eeh tya hajakaa vizuri mashetani si yakamwanza
Kakurupuka kwa kasi ya kimbunga amejichanja
Tulisikia akisema kwa sauti kubwa ya kukaripia
‘Sya waungwana mnisaidie ndo nitamweza’
Uongo mtupu babake ameliwa
Waungwana wamempeleka chau mpaka kaibiwa
Yupo hamna tafu na bifu amewehuka
Hajatulia huyu mpepeeni uuuuh uuuuh
Ni sauti iliyosikika kutoka kwa mzee wa pembeni
Sijui msaidizi mganga au mpelelezi
Na kwa taarifa yako uongozi hupati ng’oo
Labda urudi kwenu uende ukavunje tunguli
Na hao waganga wako waeleze hupati kitu hapa hata utoe chapaa eeeh eeeh.
Je, wananchi mmenisikia
Ndiyo mzee
Kuwa huyu jamaa hatufai
Ndiyo mzee
Na inafaa kumchukia
Ndiyo mzee
Hatumtaki aondoke zake
Ndiyo mzee
Tusikubali na maneno yake
Ndiyo mzee
Tunahakikisha hatumchagui
Ndiyo mzee
Kwa sababu jamaa ni mnafiki
Ndiyo mzee
Asitufanye tuwe na dhiki
Ndiyo mzee

SIYO MZEE- PROF JAY

Ubeti wa kwanza

Nawashukuru sana wananchi kwa kuweza kunipa kura
Nashanga nimeitwa ghafla kwenye kikao cha dharura
Kikao kinaashiria kina maswali juu yangu
Hii inatokana na ndiyo mzee na ahadi yangu
Naona watu ni wengi wananchi walio na maana
Najaribu kutafakari nini kinawachanganya
Nipo tayari kujibu maswali yenu zamu kwa zamu
Watakaouliza maswali na ningependa niwafahamu
Naitwa sajenti Byemero kwa niaba ya jeshi la polisi
Nilikuwa nauliza zile helkopta zetu vipi?
Nafikiria kwanza kuanzisha chuo cha marubani
Vinginevyo mtapata ajali nyingi sana angani
Baiskeli hamjui kuendesha helkopta mtaendeshaje?
Kila mtu aendeshe yake huko angani itakuwaje?
Mheshimiwa sisi wakulima ulituahidi matrekta
Na siku zinayoyoma tu mbona hujatuletea?
Wakulima mngeendelea tu kutumia jembe la mkono
Serikali haina hela bajeti imefika kikomo
Naona kilimo cha mkono kinaendelea vizuri
Jamani kazeni mikono endeleeni kukaza misuli
Wananchi tupo pamoja hapo? (Siyo mzeeee)
Watanzania tunaelewana kule? (siyo mzeeee)
Washika dau na wapiga kura pale? (siyo mzeeee)
Eeh ? (siyo mzeeee) Eti? (siyo mzeeee)
Wakulima tupo pamoja pale? (siyo mzeeee)
Wanafunzi tupo pamoja kule? (siyo mzeeee)
Ma-*barmaid* na mapolisi pale? (siyo mzeeee)
Ma-*barmaid* ondoeni hofu kilio chenu nimekisikia
Mabenzi yenu yapo bandarini tayari yameshawadia
Nimemchagua kiranja ili anipe idadi yenu
Niwape funguo muondoke na magari yenu

Ulituahidi utatujengea barabara tano tano juu na chini
Hizo zote hatutaki tunataka moja tu ya baharini
Kila siku tunapita barabara zinakuwa mbaya
Umeyafumbia macho mheshimiwa huoni haya?
Barabara ya mkwekwe nimesha mwaga kifusi
Baada ya wiki mbili itakuwa safi kama Urusi
Makandarasi wanafanya kazi kutoka China na Madagascar
Kuhusu vibarabara naomba muondoe shaka
Eeh vipi mabomba kutoa maji na maziwa nchi nzima?
Jamani naomba muulize maswali ya kiutu uzima
Mabomba kutoa maji na maziwa haiwezekani
Mlininukuu vibaya nasisitiza haiwezekani
Mzee hali ni mbaya si tungegawana vya kwako?
Kwenye kampeni zako si ilikuwa ahadi yako?
Eeh! Kugawana vya kwangu hilo suala litakuwa gumu
Familia inanitazama ebo! nina majukumu
Imeandikwa kila mtu atabeba msalaba wake
Kila mbuzi ale kwa urefuwa kamba yake
Mbona mnaniuliza maswali mengi kunikomoa?
Jamani watanzania tunajenga tunabomoa?
(Rudia korasi)

Ubeti wa pili

Wafanyakazi wa serikali sasa ninyi magari ya nini?
Daladala chungu mzima mnaweza kuwahi kazini
Nasema mnapenda sana starehe kuliko kazi
Na hiyo ndiyo sababu mnaharibu hiki kizazi
Wanafunzi niliwaahidi mtafanyia practical mwezini
Kabla ya kuwapeleka huko mi nilifanya utafiti
Nimegundua huko mwezini kweli kuna baridi kali sana
Na pia kuna vitisho kuwepo kambi za Osama
Mkinichagua tena mtakwenda huko mapema
Na nitatekeleza kila neon ninalosema

Sema nimesongwa na haka kamuda
Mkiniongezea muda kila kitu babu kubwa
Wengine kimya na maswali yamepungua
Yeyote mwenye swali ningependa kumtambua
Naona mnanong'ona wengine mmekunja sura
Hii inaonesha mmeridhika kunipa kura
Nadhani ngugu zangu tuko pamoja (Aah wapi!)
Jamani tupunguzeni jazba basi kidogo (Hatutaki)
Sasa watanzania mbona mnaanzisha vurugu
Nadhani mmesahau watanzania wote ni ndugu
Eeh? Jamani nasema hivi kikao kimeahirishwa
Jamani maafande… Afande Miraji… Afande Mzafalu…
Afande nani Gondwe njooni mtusaidie.

(Rudia korasi)

NAUZA KURA YANGU-BONTA

Ubeti wa kwanza

Pale kwa bibi hapafanani na Arusha
Pale kwa bibi hapafanani na Ilala
Pale kwa bibi hapafanani na Mwanza Mwanza
Pale kwa bibi hapafanani na Kinondoni
Hospitali iwe mlangoni
Maji safi sitaki rushwa nataka maendeleo siwezi pembejeo
Kosa nililofanya sitaki kurudia leo
Nasimama tena strong kama Cheyo
Shangazi wa Bongo alifariki kwa kuzalia nyumbani
Zahanati iko mbali baiskeli ilikuwa mbovu
Siwezi ondoa hilo kovu kwa moyo wa masikini kama mimi mwenye kovu la wovu
Kwa kweli migomo haiwezi kuisha kama shirika la reli
We have to look a people beyond a colour
Beyond a religion beyond a tribe
Just see the true nature
Natembea juu ya mbigili na kokoto
Natembea juu ya zuria jekundu

Ni rangi ya damu yetu watanganyika wa Kigoma
Ni rangi ya damu yetu watanganyika wa Ruvuma
Ni rangi ya damu yetu watanganyika wa Mtwara
Hawataki kuongea wananena kwa ishara
Achana na sara hasara unayopata ni kubwa
Yote ma-*concious*
Pale kwa bibi hapafanani na Arusha
Pale kwa bibi hapafanani na Ilala
Pale kwa bibi hapafanani na Mwanza Mwanza
Pale kwa bibi hapafanani na Kinondoni
Nauza kura yangu shilingi ngapi?
Nauza kura yangu shilingi ngapi?
Nauza kura yangu shilingi ngapi?
Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Ubeti wa pili

Sitaki tena pilau wala vipande vya kanga
Sitaki tena sabuni wala kofia ya yanga
Nataka kuuza kura yangu thamani ya *diamond*
Awe tayari kuinunua
I can't let my gold go to
Sababu wataniua kama Malima wa Kigoma
Wataichukua hakika haitarudi kama kwa Kolimba ilivyo kuwa
Check up waende London
Mwananyamala yetu sisi
Wabishi yetu sisi
Umasikini wetu sisi
Nanuka zege mzoga wa fisi
Anakupa mswaki anakung'oa jino
Wanachimba madini sisi wanatuachia mashimo
Nauza kura yangu bwana mkubwa
Ukiona hilo sababu ndio ilifanya kasubi ikazinduliwa
Listen my brother African freedom does not stop at political independence

We have to cross bourders

Siwezi kuwekwa kizuizini kama chief Abiola

Ikibidi sina budi sababu mtanzania ameonewa kwa makusudi

This is not good

Huwezi kuona mbele hata Yesu akirudi

Tongotongo la zege limeganda toka juzi wanaziba juu, chini moshi unatoka

Wanaongea bila kona wala nukta wanapaka mafuta

Pale kwa bibi hapafanani na Arusha

Pale kwa bibi hapafanani na Ilala

Pale kwa bibi hapafanani na Mwanza Mwanza

Pale kwa bibi hapafanani na Kinondoni

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Hip hop is always short like woman stress

To check our interest

And flow to cover the sight let us try and cover them

See the message and wrong be carefully large baby

Pale kwa bibi hapafanani na Arusha

Pale kwa bibi hapafanani na Ilala

Pale kwa bibi hapafanani na Mwanza Mwanza

Pale kwa bibi hapafanani na Kinondoni

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

Nauza kura yangu shilingi ngapi?

TANZANIA- ROMA.

Yeah !

My people

To day I'm free

Yes and I'm singing because I'm free

I don't care

Ubeti wa kwanza

1961 Kambarage alikuwa mwamba pasipo kumwaga damu
Akaing'arisha disemba
Rest in peace, Maria anakulilia
Kiroho upo nasi ila mwili umeshapotea
Uling'atuka ngali twakuhitaji
Hukutamani madaraka ukamwachia Alhaji
Na sasa wanagombania Ikulu tama zao mbichi
Kwa lugha za kampeni zao madaraka wanayatamani
Kila kitu nginjinginji
Wema wafa mapema wabaya mbona hamdanji
Ukabila na rushwa maofisini ndio swadakta
Alikuwa Dkt wa mifugo leo waziri wa soka
Amenunua vyeti kwa kupata stashahada
Na elimu za kuunga unga na Digrii za kikuda
Taaluma isiyo na future kwa tuliosoma sayansi
Maghorofa yanayo dondoka kwa kufoji kandarasi
Namwaga chozi kwa hela ya mama ntilie
Mumy don't cry Dad futa machozi usilie (naam)
Real so kind nakuona umepanda mori kama morani wa kimasai
Hii ndio Tanzania
Nchi yenye udongo wenye dhambi
Wanalisaka sana taji la ushindi
Biblia wanashikilia wanakemea wanagombania ufalme na umalkia
Watanzania wanakarama ya ufisadi
Dini zetu wazifanyia miradi
Tanzania taifa lilopotea kwa ahadi zao bandia

Ubeti wa pili

Laiti Mungu angeamua daily tuhudhurie mazishi naamini tungejifunza jinsi gani tuishi

Eva kumbuka Gomora, Adamu kumbuka Sodoma

Kisha wote tuswali asije Nuhu na Safina

Na nyumba za ibada wanazifanyia madhambi

Kasumba za misimu wapate taji la ushindi

Wanatumia miamvuli ya dini kuuza madawa ya kulevya

Wakitoa mapepo kwa nguvu za giza

Wanavunja amri ya sita ndani ya makanisa

Na kuabudu miungu watu ili mradi wapate pesa mbele ya madhabahu

Rwakatare, Askofu Kakobe wanadondoka mbele ya Altare wamesha toa ushuhuda wa uongo

Imekuwa biashara waumini wamepewa hongo

Wanaandika proposal za uongo wapate zali huu ni ufisadi wanapretend ujasilia mali

Ona polisi wanakuwa matajiri

Vigogo wanatoa namba za simu wapewe rushwa

Stil wanaanzisha vitengo vya kulea wagonjwa wa UKIMWI na wito hawana

Wanaanzisha wapate faida kiuchumi

My God what's wrong?

Heri wenye moyo safi anajua Mathayo

Waliingiliwa na majambazi wakavunja wakaiba kisha wakakutana bar wagawane ten percent

Pesa kweli mwanaharamu ilimponza mpaka Petro

Baada ya jogoo kiwika akagundua kamkwaza kristo

Najaza *vocal* na *bible* mkono wa kushoto naililia Tanzania

Machozi yanafunga macho.

(Rudia korasi)

Ubeti wa tatu

Nasikiasikia tu ufisadi ufisadi na wanavyo ongezeka ndio wananipa midadi

Pesa za serikali wanazianzishia miradi

Wanamiliki migodi na nyumba kama sinagogi

Walipakaziwa kesi wamenajisi watoto wakafungwa bila hatia hukumu za kipilato
Wanaiba mamilioni hawachomwi wala hawafungwi
Mtoto wangu nyundo mbili jela kwa kuvuta bangi
Shida si ndio zimemfanya avute yupi anastahili kifungo yeye au
Nidhamu ya woga sipendi kuipalilia siwezi fumbia macho ni dhambi nazoshuhudia
Najua msema ukweli hufa mapema sijali
Kama mlimuua Amina kwangu chuma cha reli kwanza kwetu mimi nimeaga
Na babu kanichinjia ng'ombe nikanywa damu kani-bless
Nije town nitete wanyonge
Malipo duniani wanao kufa mokomoko hawakujua dunia mapito
Maisha yako fair yangekuwa kama Corlina mtetezi ndio anaonewa kama Sarafina
Madereva wao mademu wanawatafutia
Wanatelekeza damu zisizo na hatia
Wake zao wanatembea na vijana wadogo bila nidhamu kisa waume zao wako busy na dini haramu
Thamani ya magari yao inajenga shule ya kijiji
Na watoto hawana elimu wanachunga ng'ombe kwa bibi
Nasimama kidete kama mlima sayuni
Mithili ya yule
Kwa pigo hili naamini nimempiga bao shetani
(Rudia korasi)

MR PRESIDENT- ROMA

Ubeti wa kwanza

Ikulu ni mahali patakatifu
Ikulu ni mahali patakatifu
Mimi sikuchaguliwa na wananchi wa Tanzania kuja kupageuza kuwa pango la walanguzi
Ahaa!
Yes!
Bongo Records
We are here for revolution
Mr President Well come to white house

Mi ndio Roma mkatoliki mwenye asili ya kiyahudi
Mpare wa milimani salamu yetu urewedi
Wewe ni mkwere wa Chalinze ambaye hutamsahau mnyakyusa Mwakyembe
Aliwafundisha Monduli siasa aliye kula kiapo
Agano jipya la wakorinto sio sabato
Mwenye siasa za Plato kama Zitto
Mwenye wito wa apolicapito
Za Kambi katoto msaka ndoto
Shujaa kama Mrisho Mpoto
Jasiri kama Mandela
Busara kama Nyerere
Alie jificha mapangoni mithili ya tangu kale
Kwa kutumia ndulele kama vita ya majimaji nife kama Kinjeketile
Hatutaki siasa za kale siku hizi tunawahi kubalehe
Nawapa pole wakazi wote wa Tandale kwa Mtogole
Asante wameniita Ikulu kisa eti nina nyota
Mvi sio busara ila naomba amani itawale
Ikulu yako ina thamani zaidi ya Falme za kiarabu
Cha ajabu hawaithamini inapoteza thawabu
Taifa lilikutabiri tangu ukiwa waziri JK wa pili utakuja ongoza hii serikali yenye vilio kote kama akina mama wa galilaya
Kutafuta mkombozi wasipandishe kodi
Wetu ni umafia na beautiful lier
Nilikuwa na ndoto hizi tangu galilaya ila bado haija ni-inspire
Mtamwaga na lami
Wanafunzi mtaleta migogoro (vipi)
Bado!
Morogoro na Tanga (vipi)
Bado!
Dodoma!
Bado!
Kigoma!
Bado!

Maisha bora kwa Tanzania, nyie wenyewe mlituambia

Manesi?

Bado!

Polisi?

Bado!

Ajira kwa vijana maendeleo kwa akina mama na watoto?

Bado!

Kina mama!

Bado!

Ubeti wa pili

Inafahamika ulipewa nchi ingali imeshachafuka na uongoze familia ya kizazi cha nyoka

Na ulikubali kubeba msalaba huu wa ukombozi

Jikaze ndio changamoto zisikutoe machozi

Sita sahau uchaguzi wa mwaka 2005 nilichomwa na jua nikingoja upite nipunge mkono

Trafic aliepangwa saa moja ukapita saa saba akiwa na stress za mwanae shuleni kafukuzwa ada leo

Mna nyumba, mashamba mnaviwanja

Mi nasaga na *rhumba* mshahara wangu haujapanda

Yule *trafic* maisha magumu

Aa mwogopeni Mungu mkisema *is not fair!*

Mnataka mnifunge pingu

Gerezani kesi za wanyonge cheki zinavyopigwa tarehe jamhuri itafuata mkondo

Ee mola wamewasaliti kama Eskaliote mbele ya Yesu mnazareti wa sakramenti ya ekaristi

Bado hawaitaki torati harakati ndio jadi hadi Yuda alichapwa mijeredi

Yuda alikuwa shahidi kwa vinanda na vinubi

Elimu yetu kufaulu ni kwa bahati nasibu

Mikopo ya DESI kimbilio la waliofeli ni ualimu na upolisi

Fisadi tenda ndege ya Rais, magari ya jeshi wote mateka

Scraper kama Lubumbashi

Wanapata alama za juu kwa kumhonga penzi *Proffesor*
Mtunza pesa benki kuu kumbe ulibeba zote
Au unataka 2010 mapinduzi yarejee
Eti utajiri ni mbuga, milima, ziwa Victoria
Piga vita ujinga na umasikini na HIV *career*
Askofu kutawala nchi hatutaki tatizo elimu dunia
Migomo ya chuo kikuu naitupia jicho la tatu
Sitetei mpaka Rutashobya linasema torati
Rest in peace shusha bendera ipepee nusu mlingoti
Bungeni hawaijadili bajeti ya walala hoi
Mtu hataishi kwa mkate bali neon sio divai
Tazama timu yako iliyopo madarakani
Chunguza kwa makini alie lia sana msibani
Walimu msipo tuajiri mtatulipa hela zetu (vipi?)
Bado!
Mitihani si mliahidi itakuja (vipi?)
Bado!
Nachingwea na Mbeya (vipi?)
Bado!
Tabora?
Bado!
Mtwara?
Bado!
Maisha bora kwa kila mtanzania
Ni nyie wenyewe mlituambia
Machinga?
Bado!
Wakulima?
Bado!
Ajira kwa vijana na maendeleo kwa akina mama, wazee?
Bado!
Vyuo vikuu?
Bado!

Ubeti wa tatu

Huu sio wakati wa kuwaua maalbino

Angalau mapinduzi kama Marcio Marximo usihangaike

Mngemtafuta Roma hakimu wa getho sauti ya mamlaka

Alofikishwa kwa mdomo keko baada ya kukemea ufisadi na sera za Karamagi aliekula jasho letu kwenye migodo ya Buzwagi

Utazuia vipi ongezeko la wimbi la ukeketaji wakati Ngariba ndio diwani wa kata mwenye kijiji

Hongera ulipima UKIMWI na mtanzania tusimpige kibao tu Mwinyi

Hayature anagundua wakati anasoma madrasa

Muda wa kujadili kesi ya Manji na Mengi hayo ya Mungu haya ya Kaisari

Jadili mambo ya msingi teacher alipo jiita mtabiri Tanganyika wakati wote vipofu na pentekoste ubatizwe maji marefu

Machozi yalimtoka segera wakati watoto hawapati

Wengi wamekimbia shule wapo vijijini wanauza visheti

Wanasomeshwa kwa mtaji wa chapati na uvuvi wa samaki

Wabunge wao wamekaa wanajiita wanaharakati

Rudi kwenu kahamasishe nduguzo hawana taaluma

Wazaramo wamegoma soma stil wanacheza ngoma wanalia kilwa kivinje

Huku wanaocheka ni wabunge alionunua kwa bibi kwa kuhonga doti ya kitenge

Hata wamasai walikuchagua kwa kura nyingi za upendo wakiamini ni mtetezi wa haki wa jimbo la Oldonyosambo

Wambie wenye himaya ya bwawa la Mtera waonyeshe mikataba na eneo la utawala

Mgodi walio kwenda Tarime hawakuwa na shamba darasa na waliotokea Mbagala

Mr President haya ni masihara sina maana utoke wewe kwenye hicho kiti umwachie Professor

Nisamehe kama nakosea maana mimi sio mwanasiasa.

KILIO CHANGU-SOLO THANG

Ubeti wa kwanza

Issue ya kwanza naanza, stone kama Banza

Niite mzanza mi ndo wa kwanza

Tufuge viroboto ogopa kutoa funza

Huwaga nawaponza na mengi hamtojifunza

Dawa ya funza ni sindano

Kila kukicha maradhi na kifo vinawaumbua

Muda mrefu naimba sijapata hata tuzo

Wanapeana ukiwauliza ni mzozo

Sijui sina vigezo labda kamchezo

Mimi nina uwezo na nyimbo ndo vielelezo

Maisha yangu ndo yangu

Ndg zangu sio yangu, navokuwa na shida

Namjua rafiki yangu anaenunua kanda zangu

Nampenda shabiki yangu, anaye nyonya tu redioni simpendi adui yangu

Asonipenda mi simpendi

Haina fagio kwangu

Anae nipenda nam-mind

Hizo ndo sera zangu

Ndugu zangu ndugu zangu ndugu zangu eee

Hiki ni kilio changu

Mi mwenzenu mi mwenzenu ninagundu

Nifanye nini ili nitoke kwenye ukungu

Nipunguzeni machungu

Basi nunueni kanda zangu

Msinipige majungu nipate nini zaidi toka kwa mungu eee

Ubeti wa pili

Wa bahati ndo shachomoa

Bwana hii tenda haiuzwi tena imepoa

Hii nimekopesha labda itaniokoa

Msoto ndo umezidi badala ya kupoa

Masikini wa bahati tajiri wa mikosi

Mfungwa nje ya gereza ndo hukumu ya yangu kesi

Isha pita nyingi nuksi usha tekwa na kikosi

Leo ndo marafiki nasito lipa kisasi

Ama kweli mi ninakipaji ili wanao ndo wanyonyaji

Wananinyonya ndo wanivishe mataji sipati

Najua kuwarubuni majaji na watangazaji ili nikidhi mahitaji
Eti ninashindania gari wameshapanga wampe nani toka awali
Sitorudia kosa hata zawadi waweke meli
Waongeze na ghorofa mbili wanikabidhi na sheli
(Rudia korasi)

Ubeti wa tatu

Ndg yangu ebu nipe tafsiri juu ya jina hili
Kwanini wazazi waliniita mimi msafiri
Ama kwangu haya maisha yana maana safari
Raha ya mateso leo napita majalali
Ona mi sina zali samahani sijala
Mtoto wa marehemu mi mjukuu wa kaburi
Visa ubalozini wamesha nitoa mara mbili
Nifanye nini ili nibadili nami waniite tajiri
Sijui nami nicheze hili nami niwe tajiri ama niwe tapeli
Nimtongoze Rais aniteue kuwa waziri
Au tu niwe mwizi wa kutumia akili ili nipate chance ya kulimbikiza mali
Labda tu nisubiri zali kama la mentali
Mademu mbona nawapata ila nao ndo wali mkali
Wale wa Oyesterbay hawanitaki mtoto mpole
Wenzangu wana misingi ya penenge wanaendesha tu magari
(Rudia korasi)

WIMBO WA TAIFA-KALA ft NAKAYA

Ubeti wa kwanza

Kwanza kabisa nafungua hotuba yenye uzito na uchungu wa msalaba
Mchezo na vipande vya ukahaba
Richmond na ubovu wa mikataba
Kuongelea mtoto wa mtaa
Baba alijificha kwenye kona na kuongelea kahaba anaye jiuza dairly ili apate ugali wa kushiba
Mbona ulisha msusa
Mi sio mwanasiasa subiri tume ichunguze

Lowasa anasubiri ushindi kama Pinda
Au machoni naona giza
Wako *faster* siogopi kufungwa au kudondoshewa vitasa, marungu
Nshapigika huo muziki nilishauchoka
Iko wapi machizi wanaitaka
Sikia napita na mkoko
Angekuwepo ungesemaje ungeonaje
Nia tunayo nguvu tunazo
Uwezo tunao angeonaje

Ubeti wa pili
Usimlaumu dalali kwa kesi ya
Badala anamlaumu kigogo
Dada aliemfundisha kunywa pombe alichanganya na gongo, bia, soda
Alimnyima shangazi kisa alimtosa uroda
Alishafukuzwa ada sister Rozi yupo keko anauza mwili na msokoto
Alikuwa mwizi wamesha mtia moto dada
Simaanishi dada kwamba tumbo moja namaanisha huyo teja
Every time matumbo yanauma kwa kuambiwa ngojangoja
Vijana mko wapi taifa la kesho miyeyusho isiyo na mwisho
Nasimama kupigana mpaka mwisho
Nsha choka nahii mashua ndani ya bahari
Wanakufa kwa UKIMWI
Wasio na mtaji watoto wa mtaa
Wanasafa mahitaji wanasubiri bingo ishuke ili mungu awavike taji
Sikia eti JKT ni chuo
Tunakula nae majani mchicha na ugali
Tufumbe macho tusali wapo wanao sadiki kwamba hajafa
Mikono juu wanachochea maafa
Mweleze *busy* huu ni wimbo wa taifa
(Rudia korasi)

Ubeti wa tatu

Sitamtukuza yeyote kati yao

Vigogo mnaosaini mikataba feki

Msitufanye watoto wadogo tusha komaa kama Zitto Kabwe

Machizi tunaliunga life wakati wanahonga debe kwa mademu

Macho yangu humwona kakaangu anapiga debe

Mara akamatwe akafungwe akanyee debe

Aishi vipi hana kitu

Basi punguzeni ubabe

Tukiandamana hamtaweza chukua ushindi

Tukija kwa mawe mapanga kundi kwa makundi

Pesa za UKIMWI bado zinaliwa za barabara bado mnazipiga chata

Babu yangu kapigika na vita ya Dunia lakini mpaka kafa

Fedha yake anafuatia mnampa tu stori mie naumia

Kastaafu kwenye reli ya TAZARA na bado anazungushwa makato yake ya mshahara

Mama mjamzito anaombwa Rushwa akiwa hana ajifungue kwa shida kwani uongo?

Ananiumiza sana

Nawaza ndugu zangu wasio na pa kulala

Wanatembea nusu uchi kwa machizi sana

Hasa kwa mi kijana na serikali ya undugu sana

Wanawekana kazini kwa kujuana

Mi ni nani sina baba wala mama

Nimekamatwa kesi ya uzururaji acha wanifunge

(Rudia korasi)

Nimeshatikisa nyavu mi ndo MVP

Wakakimbia depo kama polisi wa CCP

Nimewapigisha kuruta kwata la JKT

Ninakipaji mimi kushinda hata THT

Nawapigisha foleni kama wateja wa NMB

Mimi nimesoma PCM na sio PCB

So hata tufungwe mi ni Arsenal sio Man U sio kibonde ni member wa loarn board na TCU

Nchi imeuzwa vigogo wanatuita ATM

Tuwakemee mafisadi wote wa CCM
Wanavua gamba tuwasafishe mbele ya mbele ya CUF, CHADEMA
Muone Makamba JK kwa TFF sawa na yale mapanga ya TMK
Sio zangu sio longolongo kama vile Y2K
Nasio bandia kama kontena la BOT
Situkuzi kilicho feki kama TOT
Mimi ndio Roma nitasimama kama KKT
Asante bongo maDJ wa TVT
Mistari yangu mitamu kama ya TPC
Na kwa hizi flow kama za KCMC
Kodi ya walala hoi wanakula TRA
Miili yao ndio biashara ndani
Toa mikopo ndani ya TIA
Wanatoa mamba hazina uhakika mpaka DNA
Msambaa kauze matunda
Mwela kavue samaki
Mnyakyusa kalime mpunga
Rocky City mikono juu
Mbeya City mikono juu
Mwambieni hatukuogopa tabiri za shekhe Yahaya
Mauti yangemfika bila kumpinga Jakaya
Sirudishi kadi ya chama kama Nakaya
Bado hainiingii akilini hukumu ya babu Sea
Wagonjwa wanakufa mapokezi Dkt anakunywa *value*
Wazazi wanakufa *Labor* wengine ICU
Mgonjwa anakufa mapokezi Dkt anakunywa *value*
Wazazi wanakufa *labor* wengine ICU
Wambieni mi mzalendo nahii ndo mbiu ya mgambo
Wanapitisha mzigo wa magendo
Harakati za Dkt ni katika kuinua michezo
Wamemsaliti mwasiti wamempa tangazo
Lady pepeta hawavai sema ukweli semunge
Mipira hawatumii eti kwa babu kuna kikombe

Mafuta wamepandisha bei kisa wanamiliki sheli
Wachina wanawapa tenda sisi tunanyimwa vibali
Gongo la mboto wanalia misaada wamewatapeli
Kwa ndugu bwaga manyanga ayaokote Magufuli
Pesa za ujenzi wa shule kala na mkewe headmaster
Thamini mabango ya kampeni somesha mtoto veta
Dkt Slaa ni wapi anapata data
Kama umevaa mlegezo Ikulu napiga chapa
Vibaka manzese wanawakamata wanauza bata
Makahaba wanaongezeka boom linapokata
Mali za serikali wanauziana kwa minada
Sie tumepanga foleni
Makonde wanachonga vinyago
Masai kalime
Mnyamwezi karine asali
Mbeya City mikono juu
Iringa mikono juu
Maxcio anapata *stress*
Roma akitua Ubungo
Tanga tunafunga tatu
Tunafunga tano hapa Bongo
Wanafuga rasta ili wapate
Mademu wa kizungu we mchaga kauze mitumba
Muziki ulisha kushinda
Funga pingu mistari yako mieusi
Unajipaka Carorite msahafu sio
People needs popularity
Vuta pumzi tunza baba
Unatakiwa kupiga magoti mbele ya altare ya kasisi
Imamu akivunja ndoa usiukimbie msikiti
Padre akilala na *sister* haibadilishi ukatoliki
Binti ukimpa cotton bud
Mnakamata mateja wakati nyie ndo mnauza madawa

Ili ujue fegi imewaka lazima upige pafu

We baba usimtume mtoto acha utamuua mapafu

Popote umwonapo ng'ombe jua hakosi mmasai

Tongwa ndo ngome kongwe Zanzibar

Ndoto zangu kitambo zilikuwa kwa pazi zikayeyuka nilipopuliziwa

Nenda church na pengine popote utakaponiona nimevaa rozali ujue nipo uncouncious

Sio usharobaro ni ubabe nondo natafuta hela ya kula cheki pale

Kama babu wa Loliondo

Magazeti yanauza skendo za wasanii

Machinga wanauza kopi za CD, COSOTA wamekula blue

Shabiki anaburn nyimbo

Ukumbini anaingia free

Under ground ongeza bidii acheni kucheza bumbum

Mdigo katungue nazi

Msukuma kachunge ng'ombe

We know Tanga is now a city

Tanga mikono juu (Tongwa Records)

Tanga mikono juu!.